# Nipashe

Jumanne Mei 28, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579929

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



Nipashe TESA TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

ELIMISHE HRW: Wasichana waathirika unyanyasaji kingono Kasai

Facebook yafunga akaunti bilioni 3 za watumiaji wake

Dawa za asili kuua wadudu waharibifu shambani zanufaisha wakulima Singida

UKURASA 13



**Waziri wa JK anaswa na Takukuru**

UKURASA 3




# Sakata la makinikia lafufuliwa bungeni

• **Upinzani** wahoji ziliko tril. 424/- za Acacia na tril. 1.6/- za Barrick...*Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli akikaribishwa na mwenyeji wake, Rais Hage Geingob wa Namibia (kulia), alipowasili katika Ikulu ya nchi hiyo, jijini Windhoek jana, kuanza ziara rasmi ya kikazi ya siku mbili. Habari uk.4. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**POLISI WAUA WANANE UJAMBAZI MIKOA MIWILI**

JESHI la Polisi limeua watuhumiwa wanane wa ujambazi katika mikoa ya Dar es Salaam na Ruvuma...

UKURASA WA 4

**MABILIONI YALIVYONASWA UTOROSHWAJI WA MADINI**

SERIKALI imeliambia Bunge kuwa itaendelea kuimarisha udhibiti wa utoroshwaji na biashara haramu ya...

UKURASA WA 5

**MAFURIKO YA BUKOBA YAUA MWANAFUNZI**

MVUA kubwa iliyosababisha mafuriko katika Manispaa ya Bukoba juzi, imesababisha kifo cha mwanafunzi wa...


## MOI sasa yalia na uhaba wa madaktari

UKURASA 2



## Ushahidi wa mtoto wamfunga jela maisha

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA ZASAKA HESHIMA LEO** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Sakata la makinikia lafufuliwa bungeni

### Upinzani wahoji ziliko tril. 424/- za Acacia na tril. 1.6/- za Barrick

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imelifufua sakata la makinikia, ikitaka kujua sababu za kutolipwa kwa Dola za Marekani milioni 700 (Sh. trilioni 1.604) ambazo serikali ilisema itapewa na Kampuni ya Barrick.

Akiwasilisha hotuba yake bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka ujao wa fedha, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Madini, John Heche, alisema makubaliano hayo ya serikali na Barrick bado hayajatekelezwa huku Acacia, kampuni tanzu ya Barrick wakiendelea kuchimba dhahabu nchini.

Heche alisema Machi 2, 2017, Wizara ya Nishati na Madini ilitoa taarifa kwa umma kuwajulisha wafanyabiashara na kampuni zinazojihusisha na shughuli za uvunaji wa madini, kuacha mara moja shughuli za usafirishaji wa makinikia na mawe yenye madini ya metaliki kama vile dhahabu, shaba, nikeli na fedha.

Aliongeza kuwa mbali na katazo hilo, Rais aliunda kamati mbili za uchunguzi wa usafirishaji wa makinikia nje ya nchi na kwamba pamoja na mambo mengine, ripoti zote zilizungumzia hasara kubwa inayopata Tanzania kutokana na sheria mbovu za madini na mikataba iliyoingiwa na serikali na wawekezaji.

Alisema ripoti zote mbili zilijikita katika kubaini viwango vya madini vilivyoko katika makinikia na mikataba ya uchenjuaji ambayo haikuwa wazi.

"Ripoti ya makinikia ya Mgodi wa Bulyanhulu na Buzwagi inaonyesha kuwa Kampuni ya Acacia ambayo ndiyo mmiliki wa migodi hiyo, ilikuwa inadaiwa na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), kiasi

INAENDELEA UK 8



Mshtakiwa Sadock Amani (21) mkazi wa Burega Manispaa ya Kigoma, akiwa chini ya ulinzi wa polisi baada ya Mahakama ya Wilaya ya Kigoma jana, kumhukumu kifungo cha maisha jela, kwa kosa la kumbaka mtoto msichana (5). **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Jela maisha kwa kubaka mtoto wa miaka 5

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya Mkoa wa Kigoma imemhukumu mkazi wa Burega, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Sadock Amani (21), kifungo cha maisha jela kwa kosa la kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka mitano.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kenneth Mutembei, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo bila kuacha shaka.

Hakimu Mutembei alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi watano pamoja na kielelezo kimoja cha PF3 ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo.

Alisema mshtakiwa huyo na mama wa mtoto wamepanga nyumba moja maeneo ya Burega, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, siku ya tukio mama wa mtoto alikuwa kazini na mama mdogo wa mtoto alikuwa ananyonyesha mtoto ndani ndipo mshtakiwa huyo alipomuita mtoto huyo anko na kumwingiza ndani ya chumba chake na kumbaka.

Aidha, alisema mama mdogo wa mtoto huyo (jina limehifadhiwa) alimtafuta mtoto bila kumuona na baada ya kuangalia mlango wa chumba cha mshtakiwa aliona viatu vya mtoto na viatu vya mshtakiwa.

Alisema baada ya kuona viatu hivyo alifungua mlango na kumkuta mtoto akiwa bila nguo na mshtakiwa akiwa anambaka mtoto huyo, ndipo alipomchukua mtoto na kumfungia mshtakiwa huyo ndani hadi askari polisi walipofika na kumchukua mshtakiwa na kumpeleka kituo cha polisi kati kilichopo Mnarani Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Aidha, Hakimu Mutembei alisema askari polisi walimpatia mtoto huyo PF3 na kupelekwa katika Hospitali ya Mkoa Maweni na kufanyiwa uchunguzi pamoja na matibabu.

Alisema mtoto huyo alifanyiwa uchunguzi na daktari na kubaini kuwa alikuwa amebakwa kwa sababu damu zilikuwa zikitoka sehemu za siri.

Aidha, Hakimu Mutembei alisema alipomuuliza mtoto huyo ni nani kakufanyia unyama huo, alisema "mshtakiwa alichukua kojo lake na kuingiza kwenye kojo langu nikasikia maumivu nikali."

Alisema mtoto huyo alikuwa na uelewa

INAENDELEA UK 8

# MOI yakumbwa na uhaba wa madaktari

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa wa mifupa, hali inayosababisha daktari mmoja kutibu wagonjwa 600,000 kwa mwaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicias Boniface, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua mafunzo ya kutibu watu waliovunjika mifupa mirefu, mifupa ya kiuno na kufanya utafiti kwa madaktari 150 kutoka hospitali mbalimbali nchini na nchi za Afrika.

Alisema jumla ya madaktari bingwa wa mifupa waliopo katika hospitali mbalimbali nchini ni 150 hivyo wanahitajika angalau 2,000 ili kutoa tiba na kupunguza msongamano wa wagonjwa.

"Kuhusu idadi ya madaktari bingwa wa mifupa tunao 130 hadi 150 katika hospitali zote nchini na daktari mmoja anatibu wagonjwa 600,000. Ili kuwapunguzia madaktari mzigo huu, wanahitajika angalau madaktari 2,000 nchi nzima," alisema Dk. Boniface.

Alisema chanzo kikubwa cha kuwapo kwa wagonjwa wengi waliovunjika mifupa ni ajali za barabarani zikiwamo za bodaboda ambazo zinachangia kusababisha watu kuvunjika viuno na mifupa mikubwa ya mguu na maeneo mengine.

Alisema kwa siku MOI inapokea majuruhi 12 hadi 15 wa ajali kutoka maeneo mbalimbali nchini, huku asilimia kubwa wakitoka Dar es Salaam na wengi wakiwa ni majeruhi wa ajali za pikipiki.

Dk. Boniface alisema wagonjwa wengine wanatokana na kuanguka kutoka juu ya minazi kwa wakazi wa mkoa wa Pwani na watoto wanaodondoka uwanjani wakati wa kucheza mpira.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa wagonjwa wengi wanaopata ajali za pikipiki wanafikia mguu na kiuno hali inayosababisha kuvunjika eneo hilo.

Kadhalika alisema licha ya kujitahidi kutoa tiba, wanakabiliwa na changamoto ya vifaa tiba kama viungo bandia ambavyo vinatengenezwa nje ya nchi.

Alisema gharama ya kifaa kimoja cha kumwekea mgonjwa kinagharimu kuanzia Sh. milioni moja hadi tatu, hivyo kulazimu wagonjwa kushindwa kumudu.

Kuhusu mafunzo hayo alisema yana umuhimu wa kufahamu namna ya kutibu kikamilifu wagonjwa waliovunjika kwa sababu athari zake ni ulemavu, kushindwa kuendelea na majukumu ya kazi za

INAENDELEA UK 8

HABARI KITAIFA

# Nyalandu akamatwa na Takukuru

**Romana Mallya na Joseph Mwendapole**

ALIYEKUWA Waziri wa Maliasili na Utalii kwenye serikali ya awamu ya nne, Lazaro Nyalandu, amekamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Singida.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Sweetbert Njewike, alilithibitishia Nipashe jana kuwa Nyalandu alikamatwa na Takukuru mkoani humo.

Hata hivyo, kamanda huyo alisema hajafahamu sababu za kukamatwa Nyalandu kwa kuwa taasisi iiyomkamata inajitegemea na ndiyo yenye uwezo wa kueleza sababu.

"Ni kweli Nyalandu amekamatwa, lakini hajakamatwa na polisi bali Takukuru, ni vizuri ukawapigia ili wakueleze sababu za kumkamata ni zipi," alisema.

Nyalandu ambaye kwa sasa ni kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), alikamatwa jana wakati akiwa kwenye kikao cha Chadema, Kata ya Itaja, Jimbo la Singida Kaskazini kilichofanyika mkoani Singida.

Ofisa Uhusiano wa Takukuru, Doreen Kapwani alipopigiwa simu kuthibitisha kukamatwa na Taasisi hiyo, alikiri na kusema uchunguzi unaendelea bila kufafanua uchunguzi gani.

Katibu Mkuu wa Chadema, Vincent Mashinji, alipoulizwa kuhusu tukio la kukamatwa kwa Nyalandu, alisema mpaka jioni alikuwa anashikiliwa na Takukuru na alikuwa hajaambiwa sababu za kukamatwa kwake.

Nyalandu (49) aliingia bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2000 akiwakilisha Jimbo la Singida Kaskazini kwa tiketi ya CCM na mwaka 2005 na 2010 alichaguliwa tena kwenye jimbo hilo.

Novemba mwaka 2010, Rais wa awamu ya nne Jakaya Kikwete alimteua Nyalandu kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara hadi Mei 2011, alipohamishiwa Wizara ya Maliasili na Utalii alikokaa kwa miaka mitatu.

Januari mwaka 2014 nyota ya Nyalandu iliendelea kupaa kwa kuteuliwa na Rais Kikwete kuwa Waziri kamili wa Maliasili na Utalii nafasi aliyoitumikia hadi Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Baada ya kutangaza kuwania urais Desemba 28 mwaka 2014 na kushindwa kwenye hatua za awali, Nyalandu aliamua kuwania ubunge kwenye jimbo lake na alichaguliwa kwa kipindi cha nne ingawa mwaka 2017 aliamua kuachana na CCM na kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Oktoba 30, Nyalandu alitangaza kujiuzulu nyadhifa zake zote ndani ya CCM ikiwamo ubunge akilalamikia baadhi ya mambo ambayo aliona hayaendi sawa ikiwamo suala la Katiba mpya.

Nyalandu alisema amechukua uamuzi huo kutokana na kutokuridhishwa na mwenendo wa siasa nchini Tanzania, ukiukwaji wa haki za kibinadamu, ongezeko la vitendo vya kidhalimu dhidi ya raia na kutokuwapo kwa mipaka baina ya mihimili ya dola.



Waombolezaji wakiaga mwili wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu wa madini ya tanzanite, Thomas Mollel maarufu kwa jina la Askofu, nyumbani kwake katika Kijiji cha Mbuguni, wilayani Arumeru Mkoa wa Arusha jana, kabla ya mazishi yake yaliyofanyika nyumbani hapo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Polisi waua watuhumiwa wanane ujambazi mikoa 2

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi limeua watuhumiwa wanane wa ujambazi katika mikoa ya Dar es Salaam na Ruvuma.

Katika tukio la kwanza, jeshi hilo Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limeua watuhumiwa watatu wa ujambazi, akiwamo mwanamke mmoja, kati ya watano waliokuwa wamepanga kuvamia nyumba ya mtunza fedha za kikundi maeneo ya Kigogo Fresh.

Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa, tukio hilo lilitokea Mei 25, mwaka huu, saa 8:00 baada ya jeshi hilo kupata taarifa ya mipango ya wahalifu hao kutoka kwa wasamaria wema.

Alieleza zaidi kuwa, awali walipata taarifa hizo kuwa kuna kikundi cha majambazi watano wamepanga kuvamia nyumba ya Ally Dastan (66), ambaye mke wake aitwaye Moshi Said (56) ni mwenyekiti na mtunza hazina wa kikundi cha Umoja Group.

"Jeshi la Polisi kupitia kikosi kazi maalum cha kupambana na ujambazi kiliweka mtego katika nyumba ya Ally na ilipofika saa 8:00 usiku majambazi hao wapatao watano walivamia nyumba hiyo na baada ya kugundua kuwa kuna mtego wa polisi walianza kurusha risasi na ndipo askari wakajibu mapigo," alieleza Mambosasa.

Alieleza kuwa katika tukio hilo waliwajeruhi majambazi watatu akiwamo mwanamke mmoja na majambazi wawili walikimbia na baadaye wakiwa njiani kuwapeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), walifariki dunia.

Wakati huohuo, mkoani Ruvuma, watu watano wanaodaiwa kuwa majambazi waliokuwa na silaha za kivita, wameuawa wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma wakati wa mapambano na askari polisi.

Imeelezwa kuwa baada ya watuhumiwa hao kugundua kuwa wanafuatiliwa ndipo walipoanza kufyatua risasi hewani na askari polisi nao walianza kujibu mashambulizi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, alisema kuwa walifanikiwa kuwajeruhi watu hao hao na baadaye walikamatwa na wakati wanakimbizwa katika hospitalini ya serikali ya Wilaya ya Mbinga, walifariki dunia njiani.

Kamanda Marwa alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku katika maeneo ya Momba Mtaa wa Lusaka Kata ya Bethelehemu Mbinga Mjini. Alisema majambazi hao walikuwa wakielekea eneo la machimbo ya migodi ya dhahabu ya Darpori mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, kwa lengo la kufanya uhalifu.

Alisema polisi waliweka mtego na ndipo walijitokeza majambazi hao wakiwa wamepakizana mishikaki kwenye pikipiki mbili na baada ya moja kukamatwa, ndipo walishtukia mtego wa askari kisha walianza kufyatua risasi kwa kuwashambulia askari, askari nao walipojibu na kufanikiwa kuwajeruhi majambazi hao ambao wote walifariki dunia wakiwa njiani wakipelekwa hospitalini.

Alieleza zaidi kuwa katika eneo la tukio kulipatikana na silaha ya kivita aina ya medium mashine gun (MMG) ikiwa na mkanda wenye risasi 16 pamoja na bastola moja aina ya Glock, silaha ambazo majambazi hao walikuwa wamezibeba, huku majambazi wengine wakifanikiwa kutoroka kwa kutumia pikipiki moja.

***Imeandikwa na Mary Geofrey (Dar) na Gideon Mwakanosya, (Songea)***

# Mbunge ahoji utitiri leseni wachimbaji wa tanzanite

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MBUNGE wa Mtwara Mjini, Maftaha Nachuma (CUF), amehoji bungeni sababu za serikali kutoa leseni nyingi kwa wachimbaji wa madini ya tanzanite.

Akichangia bungeni jijini Dodoma jana mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka ujao wa fedha, Maftaha alisema kutokana na wingi huo wa leseni za uchimbaji wa tanzanite, kumekuwa na changamoto ya migogoro inayosababisha wachimbaji kuwa na wakati wakitekeleza majukumu yao migodini.

"Nataka niweze kufahamu utekelezaji ukoje kuhusiana na tanzanite, tuliona kumekuwa na mrundikano wa leseni na kubaini leseni 900 ambazo zimetolewa na wizara.

"Na changamoto kule chini kuna mtobozano, je, pendekezo lile tumefikia wapi? Kule chini wanauona, utekelezaji wake ukoje?" Mbunge huyo alihoji.

"Pia nilitaka kujua One Stop Centre itajengwa Arusha na utaratibu ukoje kwani tatizo ni kubwa sana hasa kwenye uchenjuaji.

"Watanzania wanakosa ajira sababu madini ya tanzanite wanachenjua nje, na kule China zaidi ya watu 6,000 wamepata ajira," alisema.

Mbunge huyo pia aliitaka serikali kulieleza Bunge kuhusu hatua ilizozichukua kudhibiti njia zaidi ya 400 za utoroshwaji wa madini ya tanzanite.

"Waziri atueleze, wakati tunapopitia taarifa, tulielezwa kutokana na utoroshaji Arusha na Kilimanjaro kuna njia za panya zaidi ya 400, hivyo Watanzania tunakuwa wa mwisho kunufaika. Wa kwanza ni Marekani na wanufaikaji wa pili ni Afrika Kusini.

"Wengine ni Wakenya, sisi ni wa mwisho sababu kuna njia nyingi za panya, Kenya imeendelea kwa sababu ya madini, kwa sababu ya utoroshaji wa madini yetu.

Tunadhibitije hizi njia? Naomba utupe maelezo," mbunge huyo alisema.

Katika mjadala huo, Mbunge wa Viti Maalum, Neema Mgaya (CCM), alisema ukuta wa Mirerani mkoani Manyara umeweza kuokoa madini ambayo yalikuwa yakitoroshwa kwenda nje ya nchi.

"Nimpongeze Rais na Mkuu wa Majeshi kwa kujenga ukuta Mirerani wenye Km 235 kwa Sh. bilioni 5.2, tumeona matunda ya ukuta huu, mapato ya tanzanite yameongezeka kutoka Sh. milioni 700 mpaka Sh. bilioni 2.3, hongera sana kwa kazi nzuri," mbunge huyo alisifu.

Mgaya aliishauri serikali kuhakikisha masoko ya madini yanafanya kazi iliyokusudiwa ili kuwasaidia wachimbaji wadogo.

"Ushauri wangu, hakikisheni masoko haya yanafanya kazi iliyokusudiwa, masoko yawasaidie wachimbaji wadogo. Endeleeni kuwatengea maeneo," alisema.

Mbunge huyo pia alihoji sababu

INAENDELEA UK 8

# Mabilioni yalivyonaswa utoroshwaji wa madini

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

SERIKALI imeliambia Bunge kuwa itaendelea kuimarisha udhibiti wa utoroshwaji na biashara haramu ya madini, huku ikieleza jinsi ilivyookoa mabilioni ya shilingi kwa kukamata shehena za madini yaliyokuwa yakitoroshwa na wachimbaji na wafanyabiashara.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini Dodoma jana, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema hadi Februari mwaka huu, Tume ya Madini kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ilikamata shehena kubwa ya madini.

Biteko alisema katika kipindi hicho cha miezi minane ya mwaka huu wa fedha, walikamata karati 66.6 za madini ya almasi yenye thamani ya Dola za Marekani 34,782.52 jijini Dodoma.

"Gramu 77 za madini ya dhahabu zenye thamani ya Sh. milioni 6.3 zilikamatwa mkoani Tabora na kilo 75,957.3 za madini ya vito yenye thamani ya Dola za Marekani 1,795,87.87 zilikamatwa jijini Dar es Salaam," Biteko alibainisha.

Waziri huyo aliongeza kuwa kilo 5.72 za madini ya dhahabu yenye thamani ya Sh. milioni 389.7 zilikamatwa mkoani Geita, gramu 11,445.52 za madini ghafi na karati 1,351 za vito vyenye thamani ya Sh. milioni 206.5 zilikamatwa mkoani Arusha, huku tani 3.7 za madini ya rhodelite yenye thamani ya Dola 50,162.46 zikikamatwa mkoani Morogoro.

Waziri huyo aliongeza kuwa mkoani Mwanza, yalikamatwa madini ya dhahabu kilo 319.594 yenye thamani ya Dola milioni

INAENDELEA UK 26

# Askofu wa Tanzanite azikwa

Na Waandishi Wetu, ARUSHA

VILIO, majonzi na simanzi vimetawala katika kuaga mwili wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini ya tanzanite, Thomas Mollel maarufu kwa jina la Askofu (68).

Mollel alifariki Mei 19, mwaka huu jijini Dodoma, alipokwenda kushuhudia kuapishwa kwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo (CCM).

Mollel alifariki majira ya usiku baada ya kutoka kuoga, na alijipatia umaarufu mwaka 1995, kutokana na kitendo cha kumwaga fedha akiwa ghorofani huku wananchi wakiziokota chini.

Akitoa neno la faraja wakati wa ibada ya mazishi, Mkuu wa Jimbo la Kusini la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Meru, Mchungaji Zakayo Ndeoya Pallangyo, aliwataka Wakristo kupenda kufanya kazi na kutenda kwa jamii inayowazunguka kama alivyokuwa marehemu.

Aliwataka Wakristo kujiwekea utaratibu wa kutoa msaada kwa wanajamii ili kupata baraka kwa Mungu.

"Mimi nampongeza marehemu, alitumia utajiri wake wa fedha alizopata kuwagawia wengine na pia alikuwa mfanyakazi mzuri na nampongeza Rais John Magufuli kwa kauli yake kuwa bila kufanya kazi hupaswi kula," alisema.

Hata hivyo, alionya familia ya marehemu kutogombania mali, bali wamtegemee Mungu katika kipindi kigumu wanachopitia badala ya kujali anasa zilizopo duniani.

"Familia mnapaswa kuwa wanyenyekevu, wasikivu, watii na watu wenye busara katika kipindi kigumu cha majonzi," alise-

INAENDELEA UK 26




Mkuu wa Taaluma wa Shule ya Msingi Hazina, Dennis Nyakerandi (kushoto), akikabidhi zawadi ya vitabu kwa mwanafunzi wa shule hiyo, Salma Mushi, aliyeibuka mshindi wa kwanza katika mashindano ya Hisabati na Sayansi, yalifanyika katika Shule ya Feza, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na kushirikisha wanafunzi zaidi ya 350 kutoka shule mbalimbali. Wengine ni wanafunzi wa shule hiyo, waliofanikiwa kuingia 10 bora katika mashindano hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

2 YEARS WITH THE LORD



115249102

On 24th May, You marked two years since when you were called Glory Husband/Daddy/Brother/ Son and in-law

Life is so ironic, it has been the same in your absence. It takes sadness to know what happiness is, noise to appreciate silence and absence to value presence. Husband/Daddy/Brother/Son you nurtured family value and friendship with great care and consideration.

We believe "Those we love don't go away, they walk beside us every day, unseen, unheard, but always near still loved still missed and very dear.

Until we meet again, Continue to rest in the bosom of the Lord; keep praising at the feet of Jesus.

Amen Shalom

# Walimu Tanzania kufundisha lugha Kiswahili Afrika Kusini

Na Romana Mallya

MARAIS John Magufuli na Cyril Ramaphosa wamekubaliana kuhusu walimu wa Tanzania kwenda nchini Afrika Kusini kufundisha lugha ya Kiswahili.

Katika video fupi iliyopo mitandao ya kijamii, Rais Magufuli alisema Rais Ramaphosa ni mtu mwema na mchapakazi na kwamba Tanzania itapeleka walimu kufundisha Kiswahili nchini humo.

"Ndiyo maana nimemkabidhi kamusi ya Kiswahili na vitabu vingi vya lugha ya Kiswahili vilivyoandikwa na Watanzania kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), " alisema Magufuli ambaye alikwenda nchini humo kushuhudia tukio la kuapishwa kwa Rais Ramaphosa, Jumamosi iliyopita.

Siku moja baada ya tukio hilo, marais hao walikutana Ikulu ya Pretoria kwa ajili ya mazungumzo.

"Tunafikiri njia hii itatusaidia kuitangaza vizuri lugha yetu ya Kiswahili, lakini nimemuomba katika SADC (Jumuiya ya Ushirikiano na Maendeleo Kusini mwa Afrika) angalau Kiswahili kiwe miongoni mwa lugha zitakazokuwa zinatumika," alisema Magufuli na kuongeza:

"Kama mwenzangu alivyozungumza tutashirikiana katika masuala mengi ya biashara, uvuvi, miundombinu na maji na amekubali atakuja kwenye ziara rasmi Tanzania na atakapokuja tutasaini makubaliano ya pamoja ya mambo hayo yote na baadaye kuendelea na mkutano wa SADC utakofanyika mwezi wa nane au wa tisa."

Rais Magufuli alimtakia mafanikio mema Rais huyo mpya wa Afrika Kusini ambaye awali Rais Magufuli alisema bado ana kazi kubwa ya kuchagua Baraza la Mawaziri.

"Urafiki kati ya Tanzania na Afrika Kusini umekuwapo tangu enzi za Baba wa Taifa Afrika Kusini, Nelson Mandela na marehemu baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere," alisema.

Septemba 2018, Afrika Kusini iliidhinisha lugha ya Kiswahili kufundishwa katika shule zake kuanzia mwaka 2020 na kufungua fursa kwa walimu kutoka ukanda wa Afrika Mashariki ambao ndiko chimbuko la lugha hiyo.

Taarifa rasmi ya Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, inasema kuwa: "Rais Ramaphosa amesema kufuatia uamuzi wa Afrika Kusini kuanza kufundisha lugha ya Kiswahili, nchi yake itachukua walimu wa Kiswahili kutoka Tanzania ili watumike kufundisha somo hilo katika shule za msingi na sekondari."

# HABARI KITAIFA

## Msichana aongoza shindano la Hisabati na Sayansi

Na Enock Charles

MWANAFUNZI wa Shule ya Msingi Hazina ya Magomeni jijini Dar es Salaam, Salma Sadiki, ameongoza shindano la masomo ya Hisabati na Sayansi yaliyoshirikisha zaidi ya wanafunzi 340.

Mashindano hayo yaliandaliwa mwishoni mwa wiki na shule za Feza na kushirikisha shule mbalimbali za msingi za umma na za binafsi jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa taaluma wa shule hiyo, Dennis Nyakerandi, alisema mwanafunzi huyo alipewa zawadi ya cheti na Sh. 300,000.

Aliwataja wanafunzi wengine wa Hazina walioingia 10 bora kwenye mashindano hayo kuwa ni Ibrahim Sharif aliyeshika nafasi ya pili na nafasi ya nne ilichukuliwa na Patricia Benatus wa shule hiyo.

Aliwataja wengine kuwa ni Sahill Imam, aliyeshika nafasi ya tano, Maliki Yassin, nafasi ya sita na nafasi ya nane ilichukuliwa na Khaulat Majid wa shule hiyo ya Hazina.

Denis alisema matokeo hayo yamewapa motisha kwamba wanaendelea kufanya vizuri kwenye taaluma na wanatarajia kufanya vizuri zaidi kwenye mitihani inayokuja.

"Ushindi huu haukuja tu umetokana na jitihada za walimu kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya mitihani, hivyo sisi imetupa moyo kwamba kazi tunayofanya inazaa matunda," alisema.

Alisema kwenye mashindano hayo wanafunzi walifanya mtihani wa Hisabati na Sayansi na walipaswa kumaliza ndani ya saa mbili.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akionyesha silaha mbili bastola aina ya browning na risasi tatu kwa waandishi wa habari jijini humo jana, zilizokamatwa, wakati akitoa taarifa ya kuuawa kwa majambazi watatu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mafuriko yaua mwanafunzi

Na Restuta Damian, BUKOBA

MVUA kubwa iliyosababisha mafuriko katika Manispaa ya Bukoba juzi, imesababisha kifo cha mwanafunzi wa darasa la tano.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, amethibitisha kutokea kwa kifo cha mwanafunzi huyo wa Shule ya Msingi Zamzam, Seif Mohamed (12), mkazi wa Kashenye Kata ya Kashai Manispaa ya Bukoba.

Kamanda Malimi alisema jana kuwa mwanafunzi huyo aliteleza na kusombwa na maji ya maporomoko ya Golani.

Kamanda alisema mwili wa marehemu uliokotwa majira ya mchana katika maeneo ya Mtaa wa Katotorwansi Kata Kashai, na kuwa haukutambulika haraka hadi ndugu zake walipokwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera.

Aliongeza kuwa mwili uliopolewa katikati ya maji yaliyokuwa yamefurika kwa muda mrefu kwenye Mto Golani unaoingi kwenye Mto Kanoni uliopo katikati ya mji wa Bukoba.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema kuwa wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhali kwa kuangalia mazingira rafiki ya kuendelea kuishi ili kujiepusha na athari zinazowapata nyakati za mafuriko yanasababishwa na mvua kubwa.

Akizungumzia mvua ya juzi, Gaguti alisema kwa saa tano hadi sita mvua ilisababisha uharibifu wa makazi ya watu 32 na kuathiri baadhi ya mitaa ya Manispaa.


Pia alisema miundombinu ya madaraja ilibomoka na kufungwa kwa barabara zilizokuwa zikisafirisha magari yatokayo mjini Bukoba.

Alisema chanzo kikubwa ni uharibifu wa mapitio ya maji kugeuzwa kufanyiwa shughuli za kibinadamu, hivyo kusababisha maji kushindwa kupata sehemu ya kwenda maeneo ambayo yamezoeleka nyakati za mvua.

Aliongeza kuwa hali ya wasiwasi imepungua, na kwamba wananchi wapatao 21 wamerejea katika makazi yao baada ya maji yaliyokuwa yamezingira nyumba zao kujaa na kuleta na mafuriko kupungua.

"Kwa sasa hali siyo kama ya jana (juzi) na taharuki kwa wananchi inapungua na wananchi 21 walikuwa wameondolewa kwa mitumbwi wamerejea kwenye makazi yao baada ya nyumba zao kujaa maji," alisema Gaguti.

Gaguti alisema wananchi waliorejea kwenye makazi waliondolewa kwa usafiri wa mitumbwi baada ya hali ya mazingira walikuwa wakiishi kutokuwa na eneo kavu na kuingiwa na taharuki kubwa," alisema.




## Waziri aagiza uchunguzi malipo vifuta jasho

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuunda timu ya kuchunguza uhalali wa malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa waathirika wa wanyamapori wakali na waharibifu.

Kanyasu ameagiza kuundwa kwa timu hiyo kutokana na malalamiko kutoka kwa wananchi walioharibiwa mazao yao na wamekuwa hawalipwi fidia hizo, huku waliolipwa wakidaiwa kuwa hawakustahili.

Akizungumza kwa nyakati tofauti juzi katika vijiji vya Sarakwa, Mariwanda, Unyalina Kihomboi vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, Kanyasu alisema baada ya uchunguzi huo kukamilika, watakaobainika kupokea fidia hizo ilhali walikuwa hawastahili, watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kuzirudisha fedha.

Alisema licha ya kuwa fidia hizo kulalamikiwa kuwa ni ndogo kulingana na hali ya maisha kwa sasa, wananchi walioharibiwa mazao yao wanatakiwa kulipwa kwa mujibu wa sheria na si vinginevyo.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Kanyasu amewataka wananchi mara tu wanapoharibiwa mazao yao na tembo watoe taarifa ndani ya muda wa siku tatu katika ofisi za vijiji ili hatua za malipo ziweze kufanyika kwa muda.

Pia Kanyasu aliwaeleza wananchi hao kuwa serikali imeanza kupitia upya utaratibu wa vifuta jasho na vifuta machozi ili kuendana na gharama za maisha ya sasa.

Naye Abel Hadawi, ambaye mazao yake zaidi ya ekari 20 yaliharibiwa mwaka jana, alimweleza Naibu Waziri kuwa huu ni mwaka wa tatu amekuwa akijaza fomu kwa ajili ya kulipwa fidia, lakini kila malipo yanapokuja jina lake limekuwa halimo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kikosi dhidi ya Ujangili (KDU) Kanda ya Ziwa, Emmanuel Nkya, aliwaeleza wananchi hao kuwa wanachotakiwa ni kujaza fomu nne ili kuwe na nakala kuanzia ofisi ya kijiji hadi makao makuu ya Wizara..

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# *Tahadhari ichukuliwe kuepuka kipindupindu*

ATHARI zitokanazo na mvua zimeanza kujitokeza, baada ya kuripotiwa kuwa kuna mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa kawaida mvua zinaponyesha hususan za masika ambazo huchukua kipindi kirefu, hutokea magonjwa ya mlipuko kama kuharisha, homa ya matumbo na kipindupindu.

Chanzo cha magonjwa haya huwa ni uchafu wa maji pamoja na mazingira kwa ujumla, kwa mujibu wa wataalamu wa afya.

Katika toleo letu la jana tuliripoti kwamba ugonjwa wa kipindupindu umeibuka katika Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam na mgonjwa mmoja kulazwa katika Zahanati ya Vingunguti.

Kwamba kutokana na hali hiyo, hatua kadhaa zimeanza kuchukuliwa na mamlaka husika, ikiwamo kutengwa eneo maalum kwa ajili ya kupokea na kuhudumia wagonjwa hao kama wataendelea kuongezeka.

Kaimu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omari Kumbilamoto, alisema kutokana na kugundulika kwa mgonjwa huyo Manispaa yake imetenga eneo maalum la kuhudumia wagonjwa ikiwa wataongezeka.

Kumbilamoto alisema hadi sasa wamebaini kuwa chanzo cha ugonjwa huo ni baadhi ya wananchi kutiririsha majitaka ambayo yanakwenda kwenye maji yanayotumiwa na wananchi.

Kwa mujibu wa Kumbilamoto ambaye pia ni diwani wa Vingunguti, hatua za awali zilizochukuliwa ni kunyunyiza dawa kwenye maeneo ya maji machafu yaliyotuama ikiwamo kuchukua hatua dhidi ya wanaotiririsha maji hayo kutoka kwenye vyoo.

Aidha, alisema wanawaelimisha wananchi kunyunyiza dawa, kuchemsha maji, kunawa kwa maji ya moto kabla ya kula na kuhakikisha usafi wa mazingira kila wakati.

Kwa mujibu wa Meya huyo, kwenye maeneo ya masoko wamewaelekeza wahusika kuhakikisha takataka hazikai kwa muda mrefu na usafi wa wafanyabiashara na watumiaji wengine. Mlipuko wa kipindipindu katika Manispaa ya Ilala ni jambo ambalo linapaswa kuwaamsha wakazi wa maeneo mengine kuchukua hatua za tahadhari.

Tunasema hivyo kwa kuwa tabia na mienendo ya maisha ya wakazi wa manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam zinafanana, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa maeneo mengine zaidi ya Ilala kutokea mlipuko wa ugonjwa huo.

Kwa mfano, tabia ya kutiririsha majitaka kutoka vyooni umekuwa utamaduni wa wakazi wengi wa Jiji hilo hususan ambao makazi yao yana changamoto ya miundombinu. Kutokana na hali hiyo, mvua zinaponyesha kuzitumia kutiririsha maji hayo yenye uchafu kikiwamo kinyesi.

Pia katika maeneo mengi uchafu unapozolewa kwenye masoko kurundikwa kwa muda mrefu kando ya barabara bila kuzolewa, hivyo kuwa chanzo cha kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Kadhalika, kumekuwapo na tabia ya wananchi hususan jijini Dar es Salaam kupika na kuuza vyakula kwenye maeneo machafu barabarani na karibu na mitaro ya maji, huku mamlaka husika zikiwaacha bila kuwachukulia hatua za kisheria.

Kwa Dar es Salaam pamoja na sababu nyingine, mamlaka hususan halmashauri kutosimamia sheria za usafi na afya ndiko kunakosababisha mlipuko wa kipindupindu kila uchao.

Miongozo ya afya imekuwa ikitolewa na mamlaka hizo kwa wananchi, zikiwamo hatua za tahadhari za kuchukua dhidi ya mlipuko wa kipindupindu.

Tunazishauri mamlaka za afya kuanzia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, halmashauri pamoja na ngazi za kata, vijiji, mitaa na vitongoji kuzitumia sheria zilizopo kusimamia usafi, ikiwamo kuwachukulia hatua kali wanaokaidi kuzifuata.

Bila kufanya hivyo, tutaendelea kutwanga maji kwenye kitu, na kipindupindu kitaendelea kusababisha madhara kwa wananchi, ikiwamo vifo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Serikali za mitaa zihusishwe kikamilifu kupambana na magonjwa ya mlipuko

Na Raphael Kibiriti

'MTU ni Afya' ni moja ya kampeni kubwa iliyoendeshwa na serikali ya awamu ya kwanza kwenye miaka ya 1970, ambayo kama zilivyo kampeni zingine za kiafya ililenga kuboresha ustawi wa wananchi.

Ni katika dhamira ileile ya kupambana na maradhi, moja ya maadui wakubwa watatu waliotangazwa na serikali chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere, wengine wakiwa umaskini na ujinga.

Kampeni hii ya 'Mtu ni Afya' ilikuwa na malengo matatu mahsusi lakini mawili kwa minajili ya Muungwana leo ilikuwa ni pamoja na kuongeza ufahamu kwa watu.

Ufahamu wa namna ya kuwa na maisha yenye afya kwa kuhamasisha vikundi na watu binafsi kuchukua hatua stahiki zinazotakiwa ili kulifikia lengo hilo.

Hatua za kutunza mazingira katika makazi wanayoishi kwa kuyaweka katika hali ya usafi, kuwa na vyoo bora, kunawa mikono kwa kutumia sabuni kabla na baada ya kula, mtu anapotoka msalani, mambo yaliyo ya msingi katika suala zima la kuzuia magonjwa.

Lengo lingine lilikuwa kutoa taarifa wazi na rahisi kuhusiana na dalili za magonjwa maalumu yakiwamo ya mlipuko na namna ya kuyazuia.

Kampeni hiyo iliyoendeshwa kwa njia mbalimbali kama vile kupitia kwenye vyombo vya habari, mikutano na vipindi vya darasani shuleni na kwenye mafunzo ya elimu ya watu wazima ilikuwa na mafanikio makubwa.

Pamoja na kwamba bado adui maradhi anaendelea kuwapo miongo kadhaa sasa ikiwa imepita, lakini Muungwana anadiriki kusema ushirikiano wa Watanzania wa wakati huo uliwezesha kampeni hiyo kufanikiwa.

Na ndiyo maana Tanzania ikawa mfano kwa mataifa mengine kupitia kampeni hii kama ilivyo kwa kampeni zingine ilizozizindua nyakati hizo, ikiwamo ya 'Elimu kwa Wote-UPE.'

Hata hivyo, Muungwana anashangaa kwa nini ushirikiano kama huo wa kampeni ya 'Mtu ni Afya' haupo zama hizi akiangalia namna baadhi ya wananchi wanavyozembea kuchukua hatua zinazoelekezwa na mamlaka kwa faida ya afya zao. Kuna mlipuko wa homa ya dengue katika baadhi ya mikoa nchini kwa hivi sasa, Dar es Salaam ikiongoza na elimu ya kujikinga na ugonjwa huo tayari inaendelea kutolewa na serikali kupitia wizara ya Afya nchini.

**Kwa mujibu wa Naibu Meya wa manispaa hiyo Omari Kumbilamoto, sababu ya mlipuko huo ni baadhi ya wakazi kutiririsha majitaka kutoka katika vyoo vyao kwenye maji yanayotumiwa na wananchi.**

Na katika hili serikali imeelekeza mikoa na halmashauri zote kuchukua hatua za kudhibiti ugonjwa huo, ikiwa ni pamoja na kunyunyizia dawa ya kuua viluwiluwi, kufukia madimbwi ya maji, kufyeka vichaka na kufunika mashimo ya maji taka.

Muungwana alitarajia wananchi kutoa ushirikiano kwa kufuata maelekezo ya mamlaka kwa ustawi wa afya zao kama ilivyokuwa nyakati za kampeni ya 'Mtu ni Afya.'

Katikati ya janga hili la homa ya dengue na ikionyesha namna baadhi ya wananchi wasivyofuata maelekezo ya serikali, kumeripotiwa kuibuka tena ugonjwa wa kipindupindu katika Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Naibu Meya wa manispaa hiyo Omari Kumbilamoto, sababu ya mlipuko huo ni baadhi ya wakazi kutiririsha majitaka kutoka katika vyoo vyao kwenye maji yanayotumiwa na wananchi.

Sasa kama hali ndiyo hii katika zama hizi ambapo kampeni ya 'Mtu ni Afya' ina miongo kadhaa, adui maradhi atafutika lini?

Ni rai ya Muungwana kwa serikali kupitia kwa maofisa afya katika halmashauri kutoa mamlaka ya kutosha kwa wenyeviti wa serikali za mitaa kusimamia ipasavyo suala la usafi wa mazingira.

Na hiyo si kwa kuwatoza faini tu wale wanaofungulia maji taka ya vyooni kwenda kwenye maji yanayotumiwa na wananchi, bali kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Zama hizi za Watanzania takribani milioni 55 waliopiga hatua kubwa kielimu huku karibu kila kata ikiwa na shule ya sekondari, si za mlipuko tena wa kipindupindu kila mwaka na magonjwa mengine kama homa ya dengue.

## BARUA/MJADALA

# *Watanzania tuzingatie tahadhari tunazopewa, tuhame mabondeni*

***Ndugu Mhariri habari za majukumu***

*NIMEJITOKEZA kama raia mwema wa taifa hili kutoa mchango wangu katika eneo ambalo ni la msingi katika ustawi wa Watanzania, kwa sababu linagusa shughuli zao za kila siku kwa njia moja au nyingine.*

*Ninasikitika kwamba ni eneo ambalo miaka nenda miaka rudi, limekuwa likipigiwa kelele na watu wengi wenye mapenzi mema na hasa nyakati za masika ama za vipindi vya mvua nyingi kama vinavyoendelea katika Jiji la Dar es Salaam.*

*Lakini si kwa Jiji tu la Dar es Salaam, pia kwa maeneo karibu yote ya ukanda wa Pwani kwa maana ya Tanga, Mkoa wa Pwani wenyewe, Lindi na Mtwara na kwa mujibu wa vyombo vya habari, ni karibu nchi nzima.*

*Nimejitokeza kuzungumzia tatizo moja ambalo linagusa mambo mawili kwa maana ya usalama wa watu lakini pia afya zao.*

*Tatizo hili linawahusu watu wanaoendelea kuishi maeneo ya mabondeni ambao ndio waathirika wakuu.*

*Ni waathirika wakuu wa madhara yatokanayo na wingi wa mvua za masika ama zinazoletwa na mabadiliko ya tabianchi kama ilivyojitokeza sasa kufuatia mvua ambayo imenyesha kwa takribani siku ya nane sasa.*

*Mhariri kwa miaka mingi kwa mfano katika Jiji la Dar es Salaam, watu wanaoishi katika Bonde la Mto Msimbazi, yale ya Magomeni, Jangwani, Mkwajuni, na Kigogo wameaswa kuyahama maeneo hayo.*

*Wameaswa kuhama maeneo hayo kutokana na ukweli kuwa mafuriko ambayo yamekuwa yakijitokeza si kwamba yameleta athari za vifo kwa waong'ang'ania kuishi katika maeneo hayo, bali pia athari za kiafya na mali zao.*

*Mbali na vifo, baadhi ya watu wamepoteza vifaa vya ndani, lakini mwishowe wamekumbwa na magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu, pamoja na malaria.*

*Magonjwa ya kupindupindu kwa sehemu kubwa huyakumba maeneo haya kutokana na tatizo lingine la wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, ambao baadhi yao hutumia kipindi hiki kufungulia maji ya vyooni wakiyaelekeza kwenye bonde hilo.*

*Wakati umefika sasa Mhariri kwa Watanzania na hasa wanaoishi maeneo ya mabondeni kurejesha fahamu zao katika mstari na hivyo kuhama kwenye maeneo hayo kama ambavyo serikali imekuwa ikielekeza kwa muda mrefu na wapenda maendeleo wengine.*

*Hiyo ni kwa ustawi si wa waathirika peke yao, bali pia kuokoa rasilimali za nchi zinazotumika kuwahudumia wanapokumbwa na majanga hayo.*

***Raia Mwema, Dar***




# Waliokosa elimu rasmi wasibweteke, wachangamkie fursa hizi za serikali

**Na Sabato Kasika**

ELIMU ni haki ya msingi ya kila mtoto, ingawa kuna baadhi ya watoto ambao hawakubahatika kuipata kutokana na changamoto mbalimbali.

Hata hivyo, pamoja na changamoto zinazochangia baadhi yao kutopata elimu, bado kuna njia wanayoweza kuitumia kupata.

Njia hiyo ni ile iliyoanzishwa na serikali kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA).

Mpango huu unalenga kuhakikisha kila mtoto anapata elimu ingawa ni nje ya mfumo rasmi.

Serikali ilichukua hatua za kuanzisha mpango huo kwa kutambua kwamba elimu ndio urithi pekee unaoweza kumkomboa mtoto kifikra, hasa kwa kuzingatia kwamba elimu ni kati ya haki za msingi za kibinadamu.

MEMKWA inahusisha makundi mawili, la kwanza likiwa ni rika la watoto walio na umri kati ya miaka 10-13, wanaosoma kwa muda wa miaka miwili hadi minne na kufanya mtihani wa darasa la nne.

Kundi la pili ni la rika la vijana wa miaka kati ya 14 hadi 18.

Mwaka 1999 MEMKWA ilianzishwa kwa majaribio kwenye baadhi ya wilaya zikiwamo za Ngara mkoani Kagera, Masasi mkoani Mtwara, Songea Vijijini mkoani Ruvuma na Kisarawe mkoani Pwani.

Baada ya programu hiyo kuonyesha mafanikio, mwaka 2003 serikali ilianzisha madarasa ya MEMKWA katika shule za msingi kote nchini lengo likiwa ni kuhakikisha wale wote waliokosa elimu rasmi wanaipata.

Pamoja na juhudi hizo za serikali za kutaka kuhakikisha Watanzania wote wanapata elimu, bado kuna changamoto kufuatia baadhi yao kutojua kusoma na kuandika.

Hii inatokana na kile kilichosemwa bungeni na Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Stella Manyanya, kwamba asilimia 20 ya Watanzania hawajui kusoma na kuandika.

Waziri Manyanya alisema hayo Septemba mwaka jana, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum Tasca-Restuta Mbogo (CCM) kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mbunge huyo alihoji kama kuna mpango wa serikali kurudisha elimu ya watu wazima iliyokuwapo miaka ya nyuma. Kwa hali kama hiyo ni wajibu wa kila Mtanzania kupambana na adui ujinga kutokana na ukweli kwamba tayari serikali imeshatoa fursa ya kumwezesha kila aliyekosa elimu rasmi kuipata kwa njia ya MEMKWA.

Hata wale ambao ni watu wazima, bado wana fursa kwenye mfumo wa elimu ya watu wazima, wakajua kusoma na kuandika badala ya kubweteka.

Ikumbukwe kuwa kusoma na kuandika ni mwanga wa kumwezesha mtu kuendesha maisha yake na hata kupambana na adui maradhi na umaskini.

Kwa hiyo MEMKWA ni fursa nzuri kwa vijana, ambao hawajui kusoma na kuandika ili waitumie kuondokana na adui ujinga anayeweza kuwa kikwazo cha wao kuendelea.

Mbali na MEMKWA, kwa sasa serikali inatoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne, hivyo mazingira ya kujipatia elimu yamerahisishwa.

Vilevile si vibaya kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) kuandaa mkakati wa kusaidia kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika kwa kutambua kwa maana ujinga ni adui wa maendeleo.

Jamii itambue kuwa iwapo kama watu wengi watakuwa hawajui kusoma na kuandika, itakuwa vigumu kwa nchi hii kufikia lengo lake la Tanzania ya viwanda ambayo inahimizwa kwa ajili ya maendeleo.

Kwa kukumbusha ni kwamba Mwalimu Julius Nyerere alitangaza vita kwa maadui watatu baada ya nchi kupata uhuru mwaka 1961, ambao ni ujinga, maradhi na umaskini.

Lakini maadui maradhi na umaskini hawawezi kuondoka kabla ya kumwondoa adui ujinga, hivyo Mjadala unaona ni muhimu kuunga mkono juhudi za serikali zinazotaka kila mtoto wa Kitanzania apate elimu.

Hivyo ni muhimu kurudi darasani kwa wale ambao wamesoma lakini wakatoka bila kujua kusoma na kuandika na pia ambao hawakubahatika kupata elimu, wajiunge na MEMKWA au kisomo cha watu wazima. Inawezekana wapo baadhi ya watu ambao wanaona aibu kuhudhuria madarasa ya MEMKWA au kisomo cha watu wazima, lakini watambue kuwa elimu haina mwisho na ina mchango mkubwa katika maendeleo.

Sensa ya mwaka 2012 ilionyesha kuwa asilimia 22 ya Watanzania walikuwa hawajui kusoma na kuandika, na huenda takwimu hizo zikawa zimeongezeka au kupungua iwapo jamii itakuwa imetambua umuhimu wa elimu.



# Sakata la makinikia lafufuliwa bungeni

INATOKA UK 2

cha Dola za Marekani bilioni 190 (Sh. trilioni 424) ambayo ni kodi iliyokuwa ikikwepwa pamoja na riba," alisema.

Heche aliongeza: "Kiasi hiki cha fedha kiliwafanya Watanzania kuwa na matumaini makubwa, wengi wao wakiamini kila Mtanzania ataweza kumiliki gari aina ya Noah na wengine wakiamini huduma za kijamii zitapatikana bure.

"Hata hivyo, Acacia waliikataa taarifa iliyotolewa na serikali kuwa haijawahi kukwepa kodi na huilipa serikali asilimia nne ya mirabaha ya dhahabu, shaba na fedha kwenye makinikia kama ilivyo katika makubaliano baina yake na serikali.

"Tutakumbuka mwaka 2007, kampuni hii ilituhumiwa kukwepa kodi na kuzua mtafaruku mkubwa na serikali ya wakati huo.

"Katika makubalino, Barrick iliahidi kulipa Dola milioni 700 wakati mazungumzo zaidi yakiendelea ili kuona namna gani nchi itanufaika, lakini hadi sasa, fedha hizo hazijatolewa, huku Acacia wakiendelea kuchimba dhahabu katika migodi wanayoimiliki nchini. "Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kufahamu kwanini fedha hizo hazijalipwa hadi sasa? Ikiwa kweli Acacia walipaswa kulipa malimbikizo ya kodi na tozo na hadi sasa hawajalipa, kwanini wanaendelea na shughuli za uchimbaji madini nchini wakati tuliambiwa ni wezi wa rasilimali za nchi yetu?"

Katika hotuba yake hiyo, Heche pia alisema kambi hiyo inataka kujua sababu za serikali kutoa fedha ambazo hazifiki hata asilimia moja ya fedha za maendeleo.

Alibainisha kuwa wizara hiyo katika mwaka huu wa fedha, iliidhinishiwa na Bunge Sh. bilioni 19.62 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hata hivyo, hadi kufikia Februari mwaka huu, wizara hiyo ilikuwa imepokea Sh. milioni 100, sawa na asilimia 0.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

BILIONI 100/-

Heche pia alisema kambi yao inaitaka serikali kuacha mazoea ya kuvunja sheria za nchi ambazo viongozi wamekula viapo kuzilinda.

Alisema kambi imebaini taarifa za wizara hiyo katika mwaka huu wa fedha zinaonyesha imepokea Sh. bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya wizara eneo la Ihumwa, jijini Dodoma.

"Pamoja na malengo mazuri ya ujenzi wa ofisi, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaona siyo sawa Wizara ya Fedha na serikali kutoa fedha ambazo hazikuwa kwenye bajeti.

"Ikiwa serikali ilikusudia kujenga ofisi hiyo, kwanini haikuomba bajeti yake ndani ya Bunge hili ili kuidhinishiwa na Bunge hili?

"Na ikiwa serikali ilipata wazo hili baadaye, kwanini haikufuata utaratibu wa kisheria ya bajeti ya nyongeza kwa matakwa ya sheria za nchi?" Heche alihoji.

Waziri kivuli huyo pia alisema kambi yao inataka kujua lini urasimu unakwamisha mradi wa chuma wa Mchuchuma na Liganga zitakwisha ikiwa ni pamoja na kuangalia masharti mapya ya uwekezaji chini ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017.

Heche pia alisema kambi inaishauri serikali kuhakikisha sheria zinazohusu rasilimali za nchi kama sekta ya madini, mafuta na gesi asilia zipitiwe upya ili kumpa mamlaka ya moja kwa moja Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kupata taarifa zitakazosaidia ukaguzi wake kwa maslahi mapana ya nchi.

Mbunge huyo wa Tarime Vijijini (Chadema) pia aliitaka serikali kulieleza Bunge kiasi ambacho wananchi wanaozunguka Mgodi wa Nyamongo, North Mara, watalipwa kama fidia kutokana na madhara waliyopata kufuatia mgodi huo kutitirisha maji machafu yenye sumu kwenye makazi ya watu.

Alisema tayari serikali imeipiga faini ya Sh. bilioni 5.6 Kampuni ya Acacia kama adhabu kwa kushindwa kudhibiti bwawa la maji yenye sumu na kuhatarisha afya za wakazi wanaozunguka mgodi huo.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Masha Mshomba (waliokaa kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kutoka Zambia (WCFCB), Dk. Elizabeth Lungu Nkumbula, wakitia saini makubaliano ya ushirikiano baina ya mifuko hiyo, katika hafla iliyofanyika ofisi za WCF Dodoma.

# Jela maisha kwa kubaka mtoto wa miaka 5

INATOKA UK 2

mkubwa wa kueleza na kufanya mahakama hiyo kuamini kuwa mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo kwa makusudi kabisa. Pia aliyemfanyia uchunguzi alithibitisha mahakamani kuwa mtoto huyo alikuwa amebakwa.

Hakimu Mutembei alisema mahakama haina wasiwasi na ushahidi uliotolewa na daktari pamoja na mtoto huyo ambaye alimbaini mshtakiwa kuwa ni jirani yake ndiye aliyembaka kwa sababu walikuwa na mazoea ya kuitana anko.

Aidha, Mutembei alisema upande wa mashtaka umethibitisha kosa bila kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama inamtia mshtakiwa hatiani kwa kosa aliloshtakiwa.

Upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Benedict Kivuma na upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na wakili wa kujitegemea Ignatus Kagashe, ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa.

Hakimu Mtembei alisema kutokana na vitendo vya ubakaji kukithiri na kuwa vingi katika Mkoa wa Kigoma hasa kwa watoto chini ya miaka mitano, mshtakiwa atakwenda jela maisha ili vijana wengine wajue kuwa kubaka adhabu yake ni maisha.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Benedict Kivuma, alidai kuwa Januari 5, 2018 majira ya mchana eneo la Burega, mkoani Kigoma, mshtakiwa alimbaka mtoto huyo na kumsababishia maumivu makali.

# MOI yakumbwa na uhaba wa madaktari

INATOKA UK 2

kila siku na kupata ulemavu wa kudumu.

Aidha, alisema wameshafanya utafiti mbalimbali za kutibu mifupa ya kiuno na mifupa mirefu na kwamba matokeo yake yatakapotolewa yataisaidia Moi kufanya kazi kwa weledi zaidi.

Naye Daktari Bingwa wa Mifupa, Dk. Joseph Mwanga, alisema mafunzo hayo yatawawezesha kubobea kufanya upasuaji wa mifupa ya nyonga na mifupa mirefu.

Alisema watakutana madaktari bingwa kutoka mataifa mengine kujifunza namna ya kuboresha utendaji kazi wao na kutoa tiba stahiki kwa wagonjwa.

Alisema pia watajifunza teknolojia mpya ya matibabu na maadili ya utendaji kazi wao na watafanya mafunzo kwa vitendo.

Daktari Bingwa wa Mifupa kutoka California, Prof. Michael Terry, alisema wamekuja nchini kushirikiana kujifunza kuhusu tiba ya mifupa mirefu na mifupa ya kiuno kwa lengo la kusaidia nchi za Afrika kutoa tiba na kufanya upasuaji wa kisasa.

# Mbunge ahoji utitiri leseni wachimbaji wa tanzanite

INATOKA UK 3

za kukwama kwa mradi wa Liganga na Mchuchuma, akieleza kuwa mradi huo ukikamilika, utatoa ajira kwa watu 5,000 na utachangia pato la taifa kwa asilimia tatu hadi nne.

"Huu ni mradi wa kielelezo lakini miaka minne imepita kilio chetu Njombe tunataka kujua ukoje?" Mgaya alihoji.

Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Magige (CCM), alisema wachimbaji wadogo bado wanateseka kutokana na tozo zinazotozwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kuwa juu licha ya Rais Dk. John Magufuli kuagiza tozo hizo ziondolewe.

"Wachimbaji wanateseka sana, tozo bado zipo juu, TRA bado wanatoza tozo kubwa, tulipitisha hapa bungeni. Waziri wa Fedha unanisikia na leo ninashika shilingi, wafanyabiashara wana mitaji midogo, lakini tozo bado zipo tu," alisema.

Mbunge wa Nyang'wale, Hussein Amar (CCM), aliitaka serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata leseni, akieleza kuwa bado kuna changamoto ya upatikanaji wa leseni hizo.

HABARI KITAIFA

# Shamim Mwasha, mumewe wafikishwa mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MMILIKI wa blogu ya 8020 Fashion, Shamim Mwasha (41) na mume wake, Abdul Nsembo (45), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin Hydrochloride zenye uzito wa gramu 232.70.

Wanafamilia hao walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kelvin Mhina.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali, Costastine Kakula.

Kakula alidai kuwa washtakiwa hao, wakazi wa Mbezi Beach, wanatuhumiwa kwa shtaka moja la kusafirisha dawa za kulevya.

Alidai kuwa Mei mosi, mwaka huu, eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wanatuhumiwa kusafirisha dawa hizo kinyume cha sheria ya uhujumu uchumi.

Kakula alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili wa utetezi, Hajra Mungula, aliomba upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi haraka ili hatua nyingine iweze kuendelea licha ya kwamba jana ndiyo siku ya kwanza kwa kesi hiyo kusomwa mahakamani hapo.

Hakimu Mhina alisema shtaka lao ni la uhujumu uchumi, mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, hadi upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu, kitengo cha uhujumu uchumi yenye mamlaka ya kuisikiliza.

Alisema kesi hiyo itatajwa Mei 27, mwaka huuu, na kuangalia kama upelelezi umekamilika au la. Washtakiwa wanaendelea kukaa mahabusu mpaka siku ya kwenda tena mahakamani



Muuza mkaa akisubiri wateja eneo la Mavuji mkoani Lindi juzi. Hata hivyo, wadau wa mazingira wamekuwa wakihimiza kuwapo kwa nishati mbadala kwa kuwa uchomaji wa mkaa unachangia kuharibu mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wachangisha mil. 450/- za kuboresha kituo cha afya

**Na Mwandishi Wetu**

KANISA la Anglikana, Dayosisi ya Mpwapwa mkoani Dodoma lina mpango wa kuchangisha zaidi ya Sh. milioni 450 kwa lengo la kutanua na kuboresha kituo chake cha afya cha St. Lukes.

Askofu wa Dayosisi hiyo, Jacob Chimeledya na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Tom Mazanda, walisema uamuzi wa kuanzisha mradi huo wa upanuzi ikiwamo kujenga wodi ya wanawake na watoto, upanuzi wa maabara, kununua vifaa vya afya na kuongeza watendaji umetokana na mahitaji yaliyopo katika kituo hicho ambacho kinahudumia watu wengi.

"Wana Mpwapwa wanatambua umuhimu wa kituo hiki cha St Lukes na ndio maana tumeamua kuungana na kuangalia namna ya kuchangisha fedha za kuwezesha mradi huo," walisema kuitia taarifa kwa vyombo vya habari.

Mganga Mkuu wa kituo hicho, Dk. Edwin Kiula, alisema kituo kilisajiliwa rasmi mwaka 1993 kama zahanati kutoka kwa Wamishionari wa CMS walioanzisha huduma za afya katika eneo hilo toka mwaka 1876.

Kituo cha Afya cha St. Lukes kwa sasa kinahudumia wastani wa wagonjwa kati ya 50 na 60 kwa siku, wanawake wanaojifungua kwa mwaka ni kati ya 550 na 600.

Kwa mujibu wa Dk. Kiula, wanawake wanaotibiwa magonjwa mengine ya kinamama ni zaidi ya 400 na watoto wanaolazwa ni wastani wa 300 kwa mwaka, wakati wagonjwa wa nje (OPD) kwa ujumla ni 11,000 hadi 13,000 kwa mwaka kliniki ya wajawazito na watoto ina wastani wa mahudhurio 18,000 hadi 20,000 kwa mwaka.

Magonjwa yanayotibiwa sana katika kituo hicho ni maradhi ya via vya uzazi (PID), nimonia kwa watoto, kuhara na malaria, aliongeza Dk. Kiula.

Viongozi hao walisema ingawa kituo hicho kinamilikiwa na Dayosisi ya Mpwapwa, lakini kinahudumia watu wote bila kubagua na wamekuwa wakipokea wagonjwa kutoka sehemu zote za nchi kutokana na wataalamu waliopo katika kituo hicho.

"Hata hivyo mahitaji yanaendelea kuongezeka siku hadi siku ndio maana tumeamua kufanya chagizo hili tuweze kujenga wodi ya wanawake, kununua vifaa vipya na pia kuongeza wataalamu," walisema.

Waliongeza kuwa, ukilinganisha mahitaji ya wakati wa kuanzisha kituo hicho mwaka 1993 na mahitaji ya sasa ni wazi kuna upungufu mkubwa mno ambao wanalenga kuuboresha ili kukidhi viwango vya sasa kama ilivyoelekezwa kwenye muongozo wa " quality of care" wa kimataifa na "Big Result Now" wa kitaifa.

Kwa bahati nzuri na kwa jitihada za uongozi wa kituo na Dayosisi kwa ujumla, kituo cha Afya cha St Lukes kwa miaka miwili mfululizo, 2016 na 2017 kilichaguliwa kuwa kituo bora cha afya cha kwanza kiwilaya kwa ubora kupitia tafiti ya Matokeo Makubwa Sasa yaani " Big Results Now" chini ya Ofisi ya Rais.

Walisema mgeni rasmi katika harambee hiyo itakayofanyika jijini Dar es Salaam Julai 26, 2019 ni Rais mstaafu, Jakaya Kikwete ambaye ataongozana na viongozi wengine kutoka nje na ndani ya Mpwapwa.

Kwa mujibu wa viongozi hao, tayari michango mbalimbali imeanza kuwasilishwa ili sehemu kubwa ya fedha ziwe zimeshakusanywa kufikia Julai." Tunatoa rai kwa Watanzania wote wachangie katika suala hili la kijamii ili tuweze kuokoa maisha ya wanawake na watoto na kuboresha afya zao kwa ujumla," taarifa yao ilieleza.

"Tuna imani kuwa mwitikio utakuwa mkubwa ili tuweze kutimiza malengo haya kwa muda tuliojiwekea. Ni matumaini yetu kuwa kila Mwanampwapwa atashiriki kwa namna moja au nyingine maana lazima tuanzie nyumbani kwanza kabla hatujabisha hodi kwa jirani," walisema.

Walisema, kampuni ya Ernegia Limited ya Dar es Salaam imeteuliwa kusimamia shughuli yote ya usimamizi na uendeshaji wa kukusanya michango hadi hitimisho la siku ya harambee tarehe 26.07.2019 ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Kikwete.

Wametoa wito kwa taasisi mbalimbali, mashirika, kampuni, viongozi, wafanya biashara na wanaMpwapwa wote kutoa ushirikiano na kuunga mkono katika juhudi za upatikanaji wa fedha zilizokusudiwa.

# Sababu Rorya kutunga sheria hifadhi milima

**Na Anthony Gervas, RORYA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara, inakusudia kutunga sheria ya kuhifadhi mazingira katika milima yake ili kurudisha uoto wa asili uliopotea.

Hayo yamesemwa juzi na Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, Albert Machiwa, katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika mjini Rorya.

"Halmashauri yetu tunatakiwa kutunga sheria ya kulinda na kuhifadhi mazingira ya milima ili kurudisha uoto wa asili uliopotea na kuwatoza faini wananchi watakaokuwa wakikamatwa kwa kosa la ukataji miti ovyo," alisema Machiwa.

Machiwa alisema kuwa Wilaya ya Rorya, inahitaji juhudi kubwa za upandaji miti ili kuepuka kuwapo kwa jangwa na kurudisha sura yake, kutokana na wilaya hiyo kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba inayoweza kutumika kwa kilimo cha mazao ya aina yoyote.

Alisema kuwa wilaya hiyo pia inatarajia kuanzisha kilimo cha kahawa na pamba kwa wingi ili kuongeza kipato cha wakulima na kuinua uchumi wao.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Simon Chacha, aliwakumbusha wajasiriamali wilayani humo kuhakikisha kila mmoja anakuwa na kitambulisho cha biashara ndogo, vinginevyo hataruhusiwa kufanya biashara yake.

"Mimi nawakumbusha tu wajasiriamali wadogo kuwa kila mmoja anatakiwa kuwa na kitambulisho, vinginevyo hataruhusiwa kufanya biashara, serikali bado inaendelea na zoezi la kugawa vitambulisho ambalo kwa sasa limefikia asilimia 53," alisema Chacha.

**"Mimi nawakumbusha tu wajasiriamali wadogo kuwa kila mmoja anatakiwa kuwa na kitambulisho, vinginevyo hataruhusiwa kufanya biashara, serikali bado inaendelea na zoezi la kugawa vitambulisho ambalo kwa sasa limefikia asilimia 53," alisema Chacha.**

# Majengo Shule ya Ashira kukarabatiwa wiki 3

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa tayari serikali imeshapeleka wahandisi katika Shule ya Wasichana Ashira iliyopo mkoani Arusha, ili ndani ya wiki tatu ukarabati wa majengo yake yaliyoungua kwa moto hivi karibuni ufanyike.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akijibu swali la nyongeza Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Suzan Lyimo.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema pamoja na juhudi za serikali kuhakikisha kwamba wanajenga mabweni, lakini baadhi ya mabweni hayo yamekuwa yakiungua mara kwa mara.

"Hivi karibuni Shule ya Ashira mabweni yake mawili yameungua, je, serikali mna mpango gani kuhakikisha kwamba kunakuwa na ulinzi katika shule hizo ili rasilimali kubwa ya fedha iliyowekwa ilindwe?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo alisema juzi alikuwa Shule ya Ashira na kwamba taarifa ya awali inaonyesha ni hujuma.

"Mabweni haya hayajaungana na sio kwamba kulikuwa na hitilafu ya umeme," alisema.

Alieleza kuwa juzi serikali imeshatuma timu ya wahandisi tangu jana inafanya kazi lengo kubwa ndani ya wiki tatu waanze ukarabati wa majengo hayo.

"Ukarabati uanze kwa kuwa muda si mrefu vijana wa kidato cha tano wataingizwa kwenye majengo hayo na tutafanya ukarabati wa shule hiyo yote kwa ujumla wake ili kurudi katika hali yake ya kawaida," alisema.

Kuhusu kuweka ulinzi, alisema "Kipaumbele chetu suala la ulinzi tutahakikisha kunakuwa na ulinzi tunatumia fedha nyingi sana, haiwezekani watu wakahujumu jitihada hizo za serikali."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Azza Hamad, alihoji mkakati wa serikali wa kujenga mabweni katika shule za sekondari zilizoanzishwa ili kuwasaidia watoto wa kike waweze kupata elimu iliyo bora mkoani Shinyanga.

Waziri Jafo akijibu swali hilo, alisema serikali inatambua umuhimu wa shule za sekondari kuwa na mabweni ili kuboresha elimu na kwa sasa mpango wa serikali ni kuziboresha shule za sekondari zilizopo.

Alisema ukarabati wa shule hizo unahusisha miundombinu ya mabweni hasa kwa watoto wa kike ili waweze kupata elimu iliyo bora.

"Hadi sasa shule za sekondari 1,241 zimejengwa mabweni kati ya 3,634 zilizopo kwa kutumia ruzuku ya serikali kuu, mapato ya ndani ya halmashauri na mchango wa jamii na serikali itaendelea kujenga mabweni kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo kwa kadiri itakavyoruhusu," alisema.

## Tozo kwenye mbegu zafutwa kupunguza gharama

WIZARA ya Kilimo imesema katika kipindi cha mwaka 2017/18 ada na tozo 12 katika tasnia ya mbegu zimefutwa kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji na bei ya mbegu.

Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, aliyasema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Hanang (CCM), Dk. Mary Nagu, ambaye alitaka kujua ni lini serikali itasimamia upunguzwaji wa bei kubwa ya mbegu za mahindi na pembejeo.

"Serikali iliondoa kodi ya mbegu ya mahindi mwaka 2017/2018, je, ni lini sasa serikali itasimamia upunguzwaji wa bei kubwa ya mbegu za mahindi na pembejeo?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Bashungwa, alisema serikali imeendelea kuchukua hatua ambazo zinasaidia kupunguza bei za pembejeo za kilimo.

"Mnamo mwezi Februari 2019, serikali imekutana na wadau wa pembejeo za kilimo kwa lengo la kujadili maendeleo ya pembejeo za kilimo ikiwamo kujadili suala la bei ya mbegu," alisema.

Hata hivyo, alisema katika kikao hicho wadau walikubaliana kufanya utafiti kwa kuhusisha Taasisi za Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI) na chama cha wafanyabiashara wa mbegu (TASTA) ili kutathmini gharama za uzalishaji na usambazaji.

"Jitihada zinazoendelea ni kutafuta vyanzo vya fedha ili kuwezesha mshauri elekezi kufanya tathmini hiyo na matokeo ya tathmini hiyo yatawezesha upangaji wa bei ya mbegu ambayo itamnufaisha mkulima na mzalishaji," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya watoto yatima, kwenye futari ya pamoja kutoka kwenye vituo sita vya kulea watoto hao, jijini Dar es Salaam, iliyofanyika katika viwanja vya Karimjee Mei 26. **PICHA: PMO**

## TAFICO kujenga viwanda kusindika mazao ya uvuvi

SHIRIKA la Uvuvi Tanzania (TAFICO), linatarajia kujenga viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi nchini ikiwa ni moja ya mikakati yake.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akijibu swali la Mbunge wa Ubungo (Chadema), Saed Kubenea.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua ni lini na ni wapi kiwanda cha samaki kwa ukanda wa Pwani kitajengwa na uvuvi ni shughuli inayohusu wakazi wengi sana na ni wa pili kutoka kwenye kilimo kwa kutoa ajira kwa Watanzania.

"Je, mpango wa ujenzi wa Bandari ya Samaki umefikia wapi?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema wizara inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi kwa kuweka mazingira mazuri ikiwamo uwapo wa malighafi kwa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi.

Alisema hadi sasa kuna viwanda vitano vya kusindika mazao na uvuvi katika ukanda wa Pwani.


Aliongeza kuwa serikali imeingia mkataba na mshauri elekezi wa Kampuni ya Sering Ingegneria, kutoka Italia kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi katika mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

Alisema kampuni hiyo ilianza kazi Agosti 2, 2018 na tayari imekabidhi taarifa ya awali na kazi inaendelea, hatua ya pili ya ukusanyaji wa taarifa muhimu inaendelea.

"Upembuzi huu utakapokamilika utawezesha kutambua maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa bandari na gharama za ujenzi wa bandari ya uvuvi," alisema.




Habari na Augusta Njoji



## Watumiaji maji ya mito washauriwa

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

JUMUIYA za watumiaji wa maji kwenye mito mikubwa mkoani Arusha, wameshauriwa kuanza kutumia mabomba ya maji, ili kuwapo kwa matumizi mazuri ya maji na kulinda mifereji pamoja na vyanzo vingine vya maji visikauke na kuharibiwa.

Ushauri huo ulitolwa jana na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Bonde la Mto Pangani, Patrice Otieno, alipokuwa akifungua warsha ya siku mbili ya watumiaji wa maji ya mito Themi, Kikuletwa na Nduruma, iliyofanyika ukumbi wa Kituo cha Afya Ngarenaro jijini Arusha. Alisema ili jumuiya hizo ziendelee kutumia maji ya mito hiyo bila usumbufu, lazima kuhimiza uwekaji wa mabomba ambayo ndiyo njia sahihi na bora ya kila mmoja kupata maji kwa shughuli zake.

Alisema wakiendelea kutumia njia za kiasili maji wanayotumia yatazidi kupungua kwa kuwa mengi yanapotea kabla ya kumfikia mlengwa.

Otieno aliwataka pia waimarishe mapato yanayotokana na vyanzo vya maji ya mito hiyo, kwa kuwa kwa sasa kila mto una jumuiya yake inayosimamia matumizi ya maji na hivyo matumizi hayo, yatumike kuboresha miundombinu pamoja na kuimarisha usafi na utunzaji wa mifereji kila wakati.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo ya Jamii, Jane Kabogo, alizishauri jumuiya hizo za watumiaji wa maji kutafuta wafadhili ili kuendelea kuimarisha miundombinu, hivyo kuendelea kupata maji ya kutosha.

Aliwashauri jumuiya hizo kuwasiliana na halmashauri za wilaya ili kupata mikopo ya fedha za kuendeleza maji kwa sababu halmashauri za wilaya zimetenga asilimia 10 kwenye bajeti ya kusaidia makundi mbalimbali ya kijamii.

Alizihimiza jumuiya hizo kufanya kazi kwa pamoja na serikali za vijiji na kata, kuwezesha usimamizi mzuri na uendelezaji wa utunzaji wa vyanzo vya maji ya mito hiyo mikubwa ili kuendelea kuhudumia na kuwakamata wakorofi wachache wenye nia ya kuiharibu miundombinu hiyo.

Wakichangia mada, baadhi ya washiriki, John Kalemani na Janeth Mosha, walisema umefika wakati wakachimba mabwawa kwa ajili ya kukinga maji ya mvua ili kuwezesha kuendeleza shughuli mbalimbali kikiwamo kilimo cha umwagiliaji, badala ya kuyaacha maji hayo yakipotea kama ilivyo sasa.

# Ujenzi wa barabara wageuka kero

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MRADI wa ujenzi wa kuboresha miundombinu ya barabara katika Jiji la Arusha, umegeuka kero kwa baadhi wakazi kutokana na mkandarasi kutelekeza baadhi ya barabara baada ya kuzichimba na kusababisha kusimama kwa shughuli za kibiashara na kijamii.

Ujenzi wa barabara hizo unatekelezwa na kampuni ya Ravji Construction ya Moshi, ulianza Januari 14, mwaka huu, na ulitarajiwa kukamilika Julai 31.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, mmoja wa wakazi wa Mtaa wa Leyaro, John Minja, alisema mkandarasi anayetekeleza mradi huo alichimba kina kirefu katika barabara kwa ajili ya kuanza ujenzi na kuitekeleza kwa zaidi ya miezi miwili sasa.

Alisema hali hiyo imesababisha wakazi wa mtaa huo kushindwa kuzifikia biashara na pia makazi yao.

"Kama unavyoona barabara imechimbwa kwa kina kirefu, lakini imetelekezwa na mtaa huu una shughuli za biashara kama maduka na hoteli kubwa na makazi ya watu. Tumekuwa tunapata usumbufu kufikia biashara zetu na pia wateja wanashindwa kutufikia," alisema Minja.

"Mkandarasi amekuwa akisuasua kutekeleza mradi na hali hii imetusababishia hasara kubwa sana. Wateja wetu wanalalamika kuwa barabara hii haingiliki," aliongeza.

Mkazi mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Rashid Hamis, alisema anaamini kuwa mkandarasi huyo, alikuwa hana sifa zinazotakiwa kupewa kazi hiyo na kwamba mamlaka zinazohusika zinapaswa kuingilia kati ili kuwaondolea kero wakazi wa mtaa huo.

"Tunamshangaa mkandarasi huyu, kwa jinsi anavyotekeleza mradi huu, amechimba barabara na kuhamia eneo lingine, ambapo pia amechimba kama ilivyo hapa na kutelekeza na kuwasababishia wananchi usumbufu na kero isyo ya lazima," aliongeza.

Akizungumza na Nipashe kuhusu malalamiko hayo, Mratibu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Arusha, Edward Amboka, alithibitisha kuyapokea.

Alisema hali hiyo inatokana na changamoto ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na kwamba kwa kawaida mkandarasi ni lazima achimbe barabara kwa wastani wa sentimita 80 ili kuweka matabaka ya udongo kabla ya hatua ya mwisho ya kuweka lami.

"Ni kweli kuna changamoto kubwa ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katikati ya mji, kutokana na kwamba mkandarasi hawezi kuweka njia mbadala au mchepuko kwani barabara inapochimbwa kunakuwa hakuna nafasi nyingine," alisema.

Mhandisi huyo alisema ameshatoa maelekezo kwa mkandarasi huyo kufanyia marekebisho dosari hiyo kwa kuharakisha uwekaji wa matabaka ya udongo ili amalize kwa muda aliopangiwa.

"Wananchi kwa sasa wavumilie tu ila naamini watafurahia baada ya kazi ya uwekaji wa lami kukamilika. Kama ilivyo kwa maeneo mengine na pamoja na upungufu huo, mkandarasi hajaomba muda wa nyongeza na kwa mujibu mkataba lazima ikamilike ifikapo Julai 31, mwaka huu, " alisema Amboka.

Mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya barabara za Jiji la Arusha kwa kiwango cha lami, unatekelezwa kwa fedha za mfuko wa barabara na utagharimu zaidi ya Sh. milioni 700.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Tamim Kambona (kulia,) akimkabidhi cheti cha ushiriki wa mashindano ya Quraan, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Hassan Benzi, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Katazo mifuko plastiki laibua fursa

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WAJASIRIAMALI jijini Arusha wamepata mafunzo ya muda mfupi ya utengenezaji mifuko mbadala ya karatasi kwa ajili ya vifungashio ili kukabiliana na upungufu wa mifuko utakaojitokeza, baada ya serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki.

Wakizungumza jana katika hafla ya kuhitimu mafunzo ya wiki mbili ya kutengeneza vifungashio kwa kutumia karatasi, katika Chuo cha Ufundi cha Tanganyika Polytechnic, baadhi ya wahitimu hao waliishukuru serikali kwa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kwa kuwa imewawezesha kupata fursa ya kujifunza kuzalisha mifuko mbadala itakayowawezesha kujiajiri na kuongeza kipato.

Wakizungumza kwa niaba ya wenzao, Martha Mwakidebe, Rose Chisala na Neema Mgendi, waliipongeza serikali kwa hatua ya kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki, kwa kuwa imewapa fursa ya kujifunza na kuanzisha viwanda vidogo, kwa ajili ya kuzalisha mifuko mbadala ambayo imeanza kuwanufaisha.

"Hii fursa itatusaidia sisi wajasiriamali kujiajiri kwa kutumia ujuzi tulioupata kutengeneza mifuko mbadala, ili kupiga vita matumizi ya mifuko ya plastiki," alisema Chitala.

Naye Meneja wa Shirika la Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kufunga mafunzo hayo, aliwataka wahitimu kutumia fursa hiyo kuanzisha viwanda vidogo, kwa ajili ya kuzalisha vifungashio. Alisema kwa kufanya hivyo watakuwa wanaunga mkono sera ya serikali kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda.

Alikipongeza chuo cha Tanganyika Polytechnic kwa ubunifu na kuanzisha mafunzo ya ufundi stadi yatakayowasaidia kujengea uwezo wa kufanyakazi za kuzalisha kupitia ujuzi walioupata.

Awali, Mkuu wa Chuo hicho, Abdul Semvua, alisema mafunzo hayo ni ya tatu kuhitimu tangu waanzishe programu hiyo ambayo imelenga kuunga mkono katazo la serikali kuhusu uzalishaji wa mifuko ya plastiki kwa kutoa elimu ya ujuzi kwa wajasiriamali kuweza kutengeneza mifuko ya karatasi.

"Tumekuwa na mafanikio makubwa tangu tuanzishe programu ya kutoa ujuzi kwa wajasiriamali kutengeneza mifuko ya karatasi na wengi waliohitimu kwa sasa wanatengeneza vifungashio na wameanza kuonja mafanikio," alisema Semvua.

Awali mbunifu wa mitaala katika chuo hicho, Dk. Richard Masika, alisema nia ya chuo ni kujenga uwezo wa ujuzi kwa wajasiriamali ili wawe na uthubutu wa kuanzisha viwanda vidogo na kuondoa dhana iliyojengeka kwamba wenye uwezo wa kuanzisha viwanda ni wageni kutoka nje ya nchi.

Alisema mbali na chuo hicho kutoa mafunzo ya ujasiriamali kinatoa mafunzo ya ufundi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama), umeme wa jua na umeme wa nyumbani.

# Ujenzi wa barabara Getifonga- Kahe waiva

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

AHADI ya Rais John Magufuli ya kujenga barabara ya Getifonga/Mabogini/Kahe, eneo la Moshi Vijijini kwa kiwango cha lami, imetengewa 'fungu nono' katika bajeti ya mpya ya mwaka wa fedha unaoanza Julai Mosi, mwaka huu.

Mhandisi wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Loisheyi Mollel, alisema jana kuwa barabara hiyo itajengwa kuanzia mwaka ujao wa fedha. Barabara hiyo ya Getifonga/Mabogini/Kahe, itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia eneo la Getifonga/Mabogini hadi Chekereni kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 22.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20, Tarura itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1 katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 674.52 ikiwamo ile aliyoahidi Rais Magufuli yenye urefu kilomita 20.

Mollel alieleza kuhusu utekelezaji wa mpango huo, baada ya taarifa ya utekelezaji wa robo tatu ya mwaka inayoanzia Januari 2019 hadi Machi kusomwa katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Kabla ya kutolewa taarifa hiyo inayoleta faraja zaidi kwa wananchi wa maeneo hayo, Diwani wa Kata ya Mabogini, Emanuel Mnzava, ilisema katika sekta ya ujenzi ndani ya kata yake, ahadi ya Rais (Magufuli) ya kuijenga barabara hiyo bado haijatekelezwa.

Katika taarifa yake, Mnzava alitoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, zaidi akiiomba ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na Tarura kusaidia kufuatilia ahadi hiyo.

Kata hiyo ya Mabogini ina jumla ya vijiji vinane, vitongoji 45 na ina kaya 8,360 zenye jumla ya wakazi 28,992.



Mwenyekiti wa Bodi wa Benki ya TPB Plc, Dk. Edmund Mndolwa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa mkutano mkuu wa wanahisa wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi na Mwakilishi wa Msajili wa Hazina, Lightness Mauki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taarifa ya awali moto Ashira yatolewa

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

TAARIFA za awali kuhusu uchunguzi wa tukio la kuteketea kwa moto kwenye mabweni mawili ya ghorofa ya Shule kongwe ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira, inaonyesha kuwa kuna mtu aliyewasha moto huo.

Dokezo kuhusu hujuma hiyo limo katika taarifa ya awali iliyotolewa jana na Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Daniel Kileo, mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Waziri Jafo ameagiza ndani ya siku 30 kufanyika kwa uchunguzi wa kina ili kubaini kiini cha moto huo, kufanyika tathmini ya uharibifu na gharama za ukarabati wa majengo hayo.

Kutokana na ajali hiyo ya moto iliyotokea Mei 23, mwaka huu, saa 2:00 asubuhi, Waziri Jafo amesema serikali iko mbioni kuifanyia ukarabati mkubwa shule hiyo kutokana na miundombinu yake kukabiliwa pia na chakavu.

Alisema haileti maana mabweni mawili kuungua kwa wakati mmoja, ilhali kuna miundombinu tofauti ya umeme.

Moto huo ambao chanzo chake bado hakijajulikana lakini hadi sasa chimbuko la moto huo linaacha maswali mengi yasiyojibika. Waziri Jafo alipokea taarifa ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira, Elizabeth Abdalah, ambaye alisema wanafunzi 73 wamepoteza vifaa vyao vyote, huku wanafunzi wengine 224 wakipoteza baadhi ya vifaa.

Sekondari ya Wasichana ya Ashira, imo katika kundi la shule kongwe za kitaifa za wasichana zilizowika miaka ya nyuma kwa kutoa wanafunzi wenye vipaji maalum, zikiwamo pia Sekondari ya Wasichana ya Weruweru, Kilakala, Iringa, Loleza, Msalato, Machame, Tabora na Nganza.

# Walimu wanolewa kuongeza kiwango

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

CHUO Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mwenge (Mwecau), kwa ushirikiano na Halmashauri ya Wilaya ya Siha kimeanza kuwanoa bongo, walimu 60 wa shule za sekondari za wilaya hiyo ambao watatumika kama injini ya kubadili taswira ya ufaulu katika mitihani ya kitaifa.

Katika kuhakikisha kiwango cha elimu kinapanda, serikali na wadau wa elimu wamekuwa wakiendesha mafunzo mbalimbali ili kuondoa tatizo linalosababisha kiwango cha elimu kushuka.

Ofisa Habari wa chuo hicho, Athanas Sing'ambi, aliieleza Nipashe jana kuwa walimu hao wanapatiwa mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji shuleni.

"Nia yetu ni kuwawezesha walimu kuwa na uwezo mkubwa wa ufundishaji ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi, dhana ni kwamba bila kuwanoa walimu katika baadhi ya masomo yanayoonekana kutofanywa vyema na wanafunzi inaweza kuwa ngumu kufikia malengo yanayotarajiwa," alisema.

"Gari linapotembea umbali mrefu kuna vitu vinalegea na kuchoka, hivyo huhitaji matengenezo au marekebisho ili liendelee na safari vizuri zaidi. Kuna umuhimu kwa walimu kupatiwa mafunzo kazini ili awe na kasi ya ufundishaji na matokeo ya anachofundisha kiwe na tija," aliongeza.

Kwa nini kuna umuhimu wa walimu kunolewa, Sing'ambi ameeleza zaidi kuwa walimu wanahitaji mafunzo ya mara kwa mara kutokana na jinsi ulimwengu unavyobadilika. Kwa mfano, wanasayansi wametupa taarifa kwamba sayari ya Pluto haina sifa ya kuwa sayari, kwa sababu haina magimba yanayoizunguka, vile vile sayari nyingine imegunduliwa.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalifunguliwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Valerian Juwal.

Mafunzo yanafanyika katika Shule ya Sekondari Magnificant yakishirikisha walimu 60 wa Shule za Sekondari za Siha.

**"Gari linapotembea umbali mrefu kuna vitu vinalegea na kuchoka, hivyo huhitaji matengenezo au marekebisho ili liendelee na safari vizuri zaidi. Kuna umuhimu kwa walimu kupatiwa mafunzo kazini ili awe na kasi ya ufundishaji na matokeo ya anachofundisha kiwe na tija," aliongeza.**

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 28, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 15



**Jinsi majina ya vimbunga vikubwa yanavyoundwa, kuchanganya watu**

Ukurasa 17





HRW: Wasichana waathirika unyanyasaji kingono Kasai



Ukurasa 18

## Facebook yafunga akaunti bilioni 3 za watumiaji wake



# Dawa za asili kuua wadudu waharibifu shambani zanufaisha wakulima Singida

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# FAHAMU UMUHIMU WA HATI YA TABIA NJEMA (POLICE CLEARANCE CERTIFICATE)



Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini (DCI) Robert Boaz. **PICHA: MTANDAO**

Ni cheti/hati ya uthibitisho ambayo hutolewa na Jeshi la Polisi ikithibitisha kuwa mtu aliyepewa hati hiyo hajawahi kutiwa hatiani na Mahakama kwa makosa ya jinai.

**MATUMIZI YA HATI YA TABIA NJEMA**

Hati ya Tabia Njema hutumika kwa shughuli mbalimbali za uthibitisho kama ifuatavyo:-

Kuomba VISA katika Balozi mbalimbali za nchi za nje zilizopo hapa nchini, kwa ajili ya mtu kusafiri kwenda katika nchi hizo kikazi, kimasomo, kibiashara au vinginevyo.

Kuomba ajira ndani ya nchi au nje ya nchi.

Lakini kusajili kampuni, kumiliki bunduki na kuomba uraia wa Tanzania.

Aidha, taasisi au mwajiri kumchunguza mtumishi wake. Pia kuomba kibali cha ukazi katika nchi ya kigeni (Residence permit). Pia kuomba kibali cha kufanya kazi nchi ya kigeni (work permit). Vilevile kuomba kibali cha kusoma nchi ya kigeni (study permit).

**KIGEZO MUHIMU CHA MTU KUPEWA HATI YA TABIA NJEMA**

Ili mtu aweze kupewa Hati ya Tabia Njema inampasa kufika Forensic Bureau Makao Makuu Dar es Salaam, kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole ambazo zitachunguzwa kitaalamu ili kutambua kama alishawahi kutiwa hatiani au hapana.

Pia mbali na Makao Makuu kwa watu walioko mikoani wanaweza kufika katika ofisi za wakuu wa Upelelezi wa Mikoa au Ofisi za Polisi za Wilaya waliko kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole.

Wakishachukuliwa alama hizo zitatumwa Forensic Bureau Makao Makuu kwa ajili ya uchunguzi na utolewaji wa Hati ya Tabia Njema ambayo itatumwa kwa mhusika aliyeomba hati hiyo.

**UMUHIMU WA HATI YA TABIA NJEMA**

Katika dunia ya leo yenye shughuli nyingi na mwingiliano mpana na uliowazi kwa kiasi kikubwa kati ya watu wa mataifa mbalimbali, hakuna nchi ambayo ingependa kupokea mtu ambaye haeleweki au mtu mwenye historia mbaya ya uhalifu.

Halikadhalika, hakuna kampuni au taasisi yeyote ambayo ingependa kumwajiri au kumpa jukumu lolote mtu ambaye ana historia chafu ya kiuhalifu.

Nchi na kampuni au taasisi mbalimbali zinahitaji watu wenye tabia na mwenendo mwema katika maisha ambao hawawezi kuwa chanzo cha matatizo katika nchi au taasisi zao.

Hivyo, ni jukumu la kila mtu kujitunza na kutojihusisha na uhalifu wa aina yoyote ili asije akakosa huduma hii muhimu kwa sasa.

Huduma ambayo ukiikosa ni dhahiri unaweza kushindwa kufikia malengo yako ambayo yaweza kuwa ni ya kielimu, ajira, biashara, safari za kikazi, kibiashara, kiutalii, kusajili kampuni n.k.

**MAMLAKA YA KUTOA HATI YA TABIA NJEMA**

Hati ya Tabia Njema hutolewa na Jeshi la Polisi kupitia kurugenzi ya Forensic Bureau ambayo ni Taasisi ya Uchunguzi wa kisayansi ndani ya Jeshi la Polisi.

Mojawapo ya huduma muhimu zinazotolewa na taasisi hii ni Hati ya Tabia Njema (Police Clearance Certificate) ambayo kwa kiasi kikubwa ni kwa matumizi ya kiraia.

**VIAMBATANISHO MUHIMU KATIKA MAOMBI YA HATI YA TABIA NJEMA**

Pamoja na alama za vidole viambatanisho muhimu katika maombi ya Hati ya Tabia Njema baadhi vinatofautiana kulingana na sababu ambayo mtu au taasisi inaombea Hati ya Tabia Njema kama ifuatavyo:-

**VISA YA MASOMO NJE YA NCHI**

Hapa panahitajika nakala ya hati ya kusafiria. Pia nakala ya barua ya kukubaliwa chuo (ADMISION LETTER). Vilevile picha picha ndogo moja na barua ya maombi.

**VISA YA MAKAZI/KUFANYA KAZI NJE**

Hapa panahitajika nakala ya hati ya kusafiria, picha ndogo moja, barua ya maombi na nakala ya mkataba wa kazi.

**URAIA WA TANZANIA**

Hapa panahitajika barua kutoka ofisi ya uhamiaji, nakala ya hati ya kusafiria na picha ndogo moja.

**MAOMBI YA KAZI/AJIRA NDANI YA NCHI**

Panahitajika barua ya ofisi anayotarajia kuajiriwa kama benki, kampuni za ulinzi n.k.

Vilevile nakala ya kitambulisho cha mhusika.

Lakini pia picha ndogo moja na barua ya maombi kama mhusika hatoki kwenye taasisi.

**MAOMBI YA HATI YA TABIA NJEMA KWA WAGENI WALIO NJE YA NCHI**

Panahitajika nakala ya hati ya kusafiria na picha ndogo moja, lakini pia alama za vidole zilizochukuliwa kutoka kituo chochote cha polisi katika nchi ambapo mhusika anaishi na barua ya maombi.

***Imetolewa na:***
***Ofisi ya Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi***
***Dar es Salaam.***
***habariphq@gmail.com***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Kiswahili hakiendelezwi, chapotoshwa!

'LUGHA' ni mpangilio wa maneno yanayotumiwa na watu wa jamii fulani katika mawasiliano; ni mtindo anaotumia mtu katika kujieleza.

'Lughawiya' ni taaluma inayoshughulikia uchambuzi wa lugha katika nyanja mbalimbali kama vile sarufi, maana, matamshi na matumizi.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja mbalimbali. Kati ya hizo, lahaja ya Kiunguja ndiyo iliyoteuliwa kuwa Kiswahili sanifu. Lahaja za Kiswahili ni Kingwana, Kimgao, Kitumbatu, Kimashomvi, Kimrima, Kiunguja, Kihadimu, Kipemba na Kijomvu. Pia Kimtang'ata, Kimvita, Chichifundi, Kivumba, Kingozi, Kipate, Kitikuu, Kishela, Kiamu, Chimiini, Chimbalani, Kingazija na Kinzwani.

Kwa mujibu wa kitabu cha 'Utamaduni wa Mzanzibari' kilichoandikwa na Amour Abdalla Khamis na kupata ithibati ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), kuna maswali matatu yanayoulizwa mara kwa mara; 1) Mswahili ni nani? 2) Utamaduni wake ni upi? na 3) Asili yake ni wapi?

Maswali haya, kwa mujibu wa mwandishi, hupata jawabu za kejeli na kumdharau Mswahili kuwa ni mtu aliyetawaliwa na tamaduni za nje na kutokuwa na nasabu (uhusiano wa kizazi baina ya watoto na wazazi au wazee wao) wala watwani mahususi. Kejeli na dharau kama hizi zinafanywa sana na hata baadhi ya Waswahili wenyewe kwa kutoithamini lugha yao ya Kiswahili yenye msingi wa utamaduni wa Mswahili, pale baadhi ya watu wanapohoji kuwa Kiswahili:

Hakijitegemei kwani kimepokea maneno, matamshi na maandishi yenye asili na miundo ya Kiingereza na Kiarabu na kupoteza uasili wake.

Hakina mwenyewe wala pahali mahususi bali kila msemaji na mjuzi ndiye mwenyewe na sasa ni miliki ya Afrika au dunia nzima. Hakitumiwi kwa usahihi na ufasaha miongoni mwa Waswahili wenyewe na badala yake huona fahari ya kutumia Kiingereza au kuchanganya Kiswahili na Kiingereza.

Waandishi wa sarufi yake hawaafikiani katika uchambuzi wa baadhi ya vipengele kama vile aina za maneno, vitenzi, ngeli za majina na aina za sentensi.

Dhana hizi zinahitaji kutafitiwa kwa kina ili kujua ukweli wake. Inawezekana baadhi ya dhana hizo zikawa na ukweli kutokana na kuathiriwa kwa Waswahili, Kiswahili na Uswahili jambo ambalo ni la kawaida kwa watu wote, lugha zote na tamaduni zote za dunia hii. Lakini upo uhakika kuwa baadhi ya dhana hizo si sahihi kwa Mswahili, Kiswahili na Uswahili wake. (Ukurasa wa 1-2).

Fasili ya Mswahili: Kilugha neno Mswahili lina asili ya Kiarabu kwa maana ya mtu wa pwani. Kiistilahi, kwa mujibu wa Bakhresa, S.K. (1992:256) "Mswahili ni mtu ambaye lugha yake ni ya Kiswahili. Mtu mwenye maneno mengi, mpayukaji, laghai, mdanganyifu."

TUKI (2004:279) wanasema kuwa Mswahili ni "Mtu asiyekuwa na lugha nyingine yoyote ya jadi yake isipokuwa Kiswahili. Mtu anayeishi mjini ambaye lugha yake ya mwanzo ni Kiswahili au mwenyeji wa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki na visiwa vilivyo karibu yake. Mtu mwenye maneno mengi, mjanja."

Fasili hizi zote zinamweka Mswahili kuwa ni mtu matata sana katika eneo la Mwambao wa Afrika Mashariki na kuwahofisha wengine wasio Waswahili ili wam-beze. Awali tulisema kuwa Mswahili anakejeliwa na kudharauliwa katika jamii za Afrika Mashariki.

Naona ukweli ndio huo kwa mwenye macho na masikio ya kuziona au kuzisikia fasili hizo zilizomo katika makamusi yanayotegemewa. Mtu mwenye maneno mengi, laghai, mjanja, mnyang'anyaji katika Afrika Mashariki ndiye Mswahili! Ama kweli asiyekujua hakuthamini na akutukanae hakuchagulii tusi. Sifa hizi si za Mswahili tu ni sifa za watu wengi zilizoenea kwa baadhi ya jamii tofauti za watu wa Afrika Mashariki na dunia nzima. Leo iweje sifa hizi atwikwe na kubambikizwa Mswahili peke yake? (rejea Fasili na Sifa za Mswahili Uk. 4).

Lugha: Kwa mujibu wa Chiraghdin, S. & Mnyampala, M. (1977-52 na Nurse, D. & Spear, T. (1985-62), lugha ya Waswahili ni Kiswahili chenye kujumuisha viswahili na lahaja zake 16 zikiwamo:

1.Kiunguja Mjini (Unguja mjini, Magharibi na Kati). 2. Kipate (Kaskazini ya Pate). 3. Kisiu (Mji wa Siu Kenya). 4. Kibajuni au Kitikuu (Kaskazini ya Lamu na Kusini ya Kismayuu-Shungwaya). 5. Kimgao au Kimwani (Kilwa na Kaskazini ya Msumbiji). 6. Kimtang'ata (Tanga mjini na Pangani). 7. Kipemba (Kisiwa cha Pemba).

**Methali: Eleza haja upate haja.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Jinsi majina ya vimbunga vikubwa yanavyoundwa, kuchanganya watu

MOJA ya maeneo yenye utata na mshangao mkubwa ni kutolewa kwa majina ya vimbunga vikubwa vinavyoanzia bahari kuu na kujimwaga mabara tofauti kwa nyakati mbalimbali.

Ni hali ambayo ni ya kawaida kwa baadhi ya nchi na ni ya kushangaza kwa mfano hapa kwetu.

Hivi karibuni Tanzania iliponea chupuchupu kushuhudia madhila ya kimbunga kikubwa kutoka Bahari ya Hindi kilichopewa jina la Kenneth, ambacho 'dakika za mwisho' kilipungua nguvu na kuishia Kusini, kikajimwaga Msumbiji na kusambaratisha vijiji kadhaa, kuharibu nyumba, mashamba na kuua watu. Ni kimbunga cha pili kikubwa kuipiga Msumbiji kwa msimu mmoja.

Hapakuwa na maelezo ya wazi ya kitaaluma kwanini kimbunga Kenneth kiliacha njia yake ambayo ilikuwa inaonekana bayana kikiwa katika kasi ya kilomita 600 kwa saa baharini, halafu kikapoteza nguvu na kufikia kasi ya kilometa 250 kabla ya kuacha njia ya kujimwaga mikoa ya Mtwara na Lindi.

Kuna maelezo ya jumla ya uhusiano kati ya mkondo wa vimbunga na muundo wa dunia kuwa nguvu za uvutano zinakuwa na nguvu zaidi katika eneo la Ikweta ambako kila upande huvutia kwake. Kimbuga kikiwa Kusini kinapata shida kuvuka Ikweta na kuingia eneo la Kaskazini, na hapa kwetu Ikweta iko ncha ya Kaskazini (karibu na Kisumu, Kenya). Halafu kuna mbinyo wa pwani ya Tanzania kupinda kushoto ukitoka Kusini.

Kwa njia moja au nyingine, yaani kwa vile Msumbiji iko Kusini zaidi kuliko Tanzania, halafu ardhi yake ni kama 'imeingia' baharini kwa kina zaidi, inaendana na njia za vimbunga wakati ardhi ya Tanzania ina 'mbinyo' na iko Kaskazini zaidi, kuna mazingira ya Tanzania kukwepa vimbunga na athari zake lukuki.

Tatizo kubwa zaidi ni kuwa vimbunga vimekuwa vikiongezeka kwa idadi yake na ukali wake, hali inayoelezewa kwa jumla kuwa inatokana na mabadiliko ya tabianchi, hasa kuongezeka kwa wingi wa maji baharini baada ya ncha za barafu Kaskazini na Kusini ya dunia kuanza kuyeyuka kwa kasi.

Ni kutokana na ongezeko la joto katika anga, bahari.

Ukiangalia kinachoelezwa na baadhi ya wataalamu kuhusu kutolewa majina ya vimbunga hivi unaweza kugundua kuwa kuna siri bado zimefichwa, kwani haielezwi kinagaubaga uhusiano wa kimbunga na jina linalotolewa, na hata suala la kwanini kuwe na majina kama hayo.

Mmoja wa watalaamu anaeleza kuwa kuna haja ya uelewa wa jinsi kutolewa kwa 'lebo' (majina) kwa



Sehemu ambayo ilitokea uharibifu wa Kimbunga Kenneth hivi karibuni nchini Msumbiji. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa jadi ya makabila tofauti nchini, kikianza kimbunga (hivi vya ardhini ni vidogo) mtu anaweza kuweka ungo uliofunikwa katika nia yake, na kikishapita ukafunua ungo, unaona nyoka pale.

majanga ya kimazingira kunavyoweza kuathiri jitihada za kukabiliana na hali hiyo.

Ni kama vile kimbunga kikipewa jina la ua fulani basi kitakuwa kama hakina madhara kwani ua linapendeza, na hivyo pia kwa majina ya wanawake, tofauti na wanaume.

Hata hivyo, takwimu zinatoa picha nyingine, kuwa vimbunga vyenye majina ya kike vimekuwa na nguvu ya uharibifu hata zaidi.

Mtaalamu huyo ambaye haielekei anaelewa kwa kina sababu za msingi za kitamaduni za kutoa majina ya vimbunga anatoa rai kuwa kuna haja ya kuangalia upya hulka ya kutoa majina ya kujiamulia tu kwa majanga ya kimaumbile kama sehemu ya jitihada ya kufanikisha mawasiliano.

Hoja hiyo inatetewa na mchangiaji wa mada hiyo katika mtandaomaktaba wa Wikipedia kuwa vimbunga vinapewa majina na vituo tofauti vya tahadhari ili kurahisisha mawawiliano kati ya watabiri wa hali ya hewa na jamii, ni muhimu ili kuainisha kinachozungumziwa na hivyo kuchukua hatua.

Kuanza kuelewa chanzo cha kutoa majina ya vimbunga, inafurahisha kusoma katika mtandao huo kuwa majina hayo yalianzia India, na kwa jumla ndiyo nchi yenye vimbunga vikubwa na vingi zaidi kuliko maeneo mengine duniani.

Isitoshe, kwa jumla kuna kanuni ya India kuwa na majanga ya kibinadamu ya kushangaza, kuanzia magonjwa ya mlipuko (kwa mfano jiji la Calcutta siku hizi linaandikwa Kihindi, Kolkata zamani lilikuwa linaitwa 'the cholera capital of the world,' yaani mji mkuu wa kipindupindu duniani.

Ajali za India za treni, mabasi, mvua na maporomoko (labda kuacha matetemeko ya nchi) kwa jumla ni takwimu za kushangaza duniani. Kwa mfano katika kipindi cha nusu mwaka 2018, kimbunga Gaja kilikuwa cha pili baada ya eneo la pwani ya Odisha na Andhra Pradesh kuteswa na kimbunga Titli, kilichoua zaidi ya watu 70.

Gaja, ambacho kiliangukia pwani ya Tamil Nadu na Andhra Pradesh inamaana ya 'tembo' katika lugha ya Kihindi, Sanskrit. Uchambuzi wa Wikipedia unasema kuwa vimbunga vinapewa majina vinapokuwa na kasi ya zaidi ya kilomita 61 kwa saa, na majina yanatokana na orodha zilizopo tayari zinazoendana na eneo vimbunga vinakotokea.

Sasa kwa vile vimbunga huwa vinaanzia bahari kuu, tuseme majina hayo ni ya kina nani wanaohusika na ukanda wa bahari, au muda huo?

Mchambuzi anaeleza kuwa wakati wa Vita Vikuu vya Pili, vimbunga vya maeneo ya joto (tropic) vilikuwa vinapewa majina yasiyo rasmi ya wanawake na Jeshi la Anga la Marekani kutokana na majina ya wapenzi wao au wake zao.

Ni wanaanga waliokuwa wakichunguza kuanza na kushika kasi kwa vimbunga, wakaona ni vyema watoe jina kwa kila kimbunga kama njia ya kurahisisha mawasiliano.

Mara nyingi Jeshi la Anga la Marekani linatoa majina hata kwa mabomu makubwa au ndege inayobeba bomu hilo, kwa mfano bomu la atomiki lililoangushwa Hiroshima hapo Agosti 6, 1945, kumaliza vita vikuu lilibebwa na ndege ya kivita iliyoitwa Enola Gay. Ni jina la Enola Gay Tibbets, mama mzazi wa Kanali Paul Tibbets, rubani wa ndege hiyo.

Ni kanuni hiyo hiyo ya kutoa majina kwa operesheni za kijeshi, ambayo baadhi yanavuma sana, kwa mfano Operesheni Desert Storm (kimbunga jangwani) kuing'oa Iraq chini ya Rais Saddam Hussein aliyeivamia Kuwait mwezi Septemba 1990. Jina lingine lililovuma ni mashambulizi ya kina ya Israel nchini Lebanon ni 'Peace for Galilee' (Amani kwa Galilaya) mwaka1982 ambako jeshi la Israel liliingia Lebanon kuwaangamiza wapiganaji wa Kipalestina.

Jingine ni 'Black September' lililotumiwa na Wapalestina kuelezea vita ya Mfalme Hussein wa Jordan dhidi ya PLO, chama cha ukombozi wa Palestina kilichokuwa kinataka kuupindua utawala wake, mwaka 1970. Ina maana kuwa majina haya ya vimbunga yanayosikika kimsingi ni marudio ya matukio ya zamani ambako askari wa Marekani walikuwa wanadhibiti Bahari ya Hindi na Pacific pia, hivyo kuwa na wakati wa kutosha kuangalia vimbunga bahari kuu zote tatu - Hindi, Pacific na Atlantiki.

Marekani kwa upande wa Mashariki ni Atlantiki (yenye vimbunga vingi) na Magharibi ni Pacific ambayo kimsingi haina vimbunga, kana kwamba vimbunga vinafuata maeneo yenye watu wengi kama ukanda wa Caribbean na Kusini ya Marekani kwa upande mmoja, Kusini ya India kwa upande mwingine na sasa inaelekea eneo la Kusini Mashariki ya Afrika linaongezwa.

Hata hivyo, kwa jadi fulani unaweza kusema askari wa Marekani walikuwa 'wanajiinua kufika mbinguni' kwani vimbunga vinaendana na nguvu za giza zinazofurahia mazingira hayo.

Kwa jadi ya makabila tofauti nchini, kikianza kimbunga (hivi vya ardhini ni vidogo) mtu anaweza kuweka ungo uliofunikwa katika nia yake, na kikishapita ukafunua ungo, unaona nyoka pale.

Inabidi utoe sadaka kama chembe za mahindi, karanga au chochote, la sivyo kimaadili utakuwa umemsumbua. Ataonekana kupotea usimwone, lakini kihalisia atamvaa mtu huyo, na mara nyingi unakuta ni mtoto anacheza tu, na kwa wakati hiyo mtoto huyo anakuwa ndiyo sadaka aliyoacha kuileta.

Kule India wakitoa majina watakuwa wanajua wanafanya nini kwa kiwango kikubwa, na askari wa Marekani wana utamaduni wa kuchangia baadhi ya vitu.

UGUNDUZI

**NA BEATRICE PHILEMON**

# Dawa za asili kuua wadudu waharibifu shambani zanufaisha wakulima Singida

- Zinatumia malighafi zinazopatikana vijijini
- Ni matokeo ya mradi wa kuwajengea uwezo wakulima

LENGO Namba mbili kati ya malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) linataka dunia imalize janga la njaa, kuwe na usalama wa chakula, lishe bora na kilimo endelevu miongoni mwa mataifa, Tanzania ikiwamo.

Hata hivyo, moja ya changamoto kubwa inayoikabili Tanzania kama ilivyo kwa maeneo mengine ya dunia, ni tatizo la mara kwa mara la upungufu wa chakula kwa watu wake.

Sababu zinazochangia tatizo hili ukiacha uduni wa kilimo kwa wananchi, wengi wakiwa ni wakulima wadogowadogo ni changamoto ya ukosefu wa pembejeo zikiwamo dawa za kilimo.

Dawa za kilimo zimekuwa na mambo mengi, ughali wake lakini pia athari zake kwa mazao kutokana na kemikali zinazotumika na kwa afya za wakulima na hivyo kuzorotesha tija tarajiwa ya kilimo.

Ndiyo maana wadau mbalimbali wamejitokeza kuendesha utafiti, lakini kutoa mafunzo kwa lengo la kupata dawa za kilimo zitakazoongeza tija, pia kuondoa madhara yatokanayo na baadhi ya dawa za kilimo za viwandani.

Hivyo katika dhamira ya kuwezesha Lengo Namba mbili la SDGs kufikiwa, Mradi wa kutengeneza dawa za asili za kilimo umewezeshwa nchini.

Ni mradi wa miaka mitatu ulioanza mwaka 2016, ukitarajiwa kumalizika Juni mwaka huu mkoani Singida, na ambao umeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo, hususani katika Wilaya ya Singida unakotekelezwa.

Unaojulikana kama 'Singida Nutrition and Agro-ecology Project (SNAP)' ambao ulianza na vijiji 10 katika halmashauri ya wilaya hiyo na vingine 10 vikafuata baadaye.

Miongoni mwa kazi kubwa zilizofanywa na mradi huo ukiacha matumizi ya dawa za asili katika kilimo ni pamoja na kuwajengea uwezo wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo mseto na lishe.

Mradi pia unalenga kuboresha uhakika wa chakula katika kaya na jamii na kuboresha nafasi ya kila mmoja kuwa na afya na lishe bora.

Aidha, kuboresha udongo kwa kulima kilimo mseto kwa kutumia mazao ya jamii ya mikunde, kupinga unyanyasaji wa kijinsia na kutoa elimu kuhusu usawa wa kijinsia.



Wakulima walionufaika na mradi wa kilimo mseto na lishe Singida (SNAP) wakiwa kwenye warsha ya siku moja ya hitimisho la mradi wa SNAP.

### MBINU

Ili kufikia tija iliyokusudiwa, mradi ulianza kwa kufundisha wakulima washauri 40 kutoka katika vijiji 20 vya kwenye mradi.

Kwamba kila kijiji kilipeleka katika mafunzo wakulima washauri wawili, mwanaume na mwanamke ambao ndio wanaotumika kueneza elimu hii kwa wakulima wengine katika vijiji hivyo.

Hadi sasa zaidi ya kaya 1200 zimenufaika kwa kuwa na ujuzi wa kutengeneza na kutumia dawa za asili kwa ajili ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao yao.

> Tunatoa elimu kwenye jamii na shuleni kuelimisha wazazi na watoto wenyewe kukataa kufanyiwa ukeketaji.

Aidha, wananchi wamepata elimu ya kuhifadhi mazao kitaalamu, lishe na kilimo mseto.

Mradi huo unaendeshwa na ActionAid Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ilonga, Chuo Kikuu cha Cornell (Marekani), Chuo Kikuu cha Nelson Mandela (Arusha) kwa ufadhili wa Shirika la Marekani la McKnight Foundation.

### WASHAURI

Pili Shabani, ni mkulima mshauri kutoka kijiji cha Ntondo, Kata ya Msisi, Wilaya ya Singida.

Ni miongoni mwa wakulima washauri 40 walionufaika na mradi huo, ikiwa ni pamoja na kupata mafunzo nchini Malawi.

Akizungumza na Nipashe, Pili anashukuru kufaidika na mafunzo ya kutengeneza dawa za asili kwa ajili ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao shambani na wakati wa kuvuna (Traditional pesticides).

"Tumefundishwa jinsi ya kutengeneza dawa za asili kwa kutumia bangi pori, mwarobaini, ndulele, alovera pamoja na majivu ya miti," anasema.



Mkulima mshauri kutoka Kijiji cha Ntunduu, Claud Mnyawi (aliyechuchumaa), akiwafundisha wakulima wenzake jinsi ya kutengeneza dawa za asili kwa kutumia unga wa mwarobaini kilo moja kwenye maji ya lita 10.

### DAWA YA MWAROBAINI

Akizungumzia jinsi ya kutengeneza dawa ya asili ya mwarobaini kwa ajili ya kuua wadudu waharibifu wa mazao shambani, Pili anasema:

"Mtu anatakiwa kuchukua majani ya mwarobaini, kuyaanika katika sehemu isiyo na jua...baada ya hapo anayatwanga na kisha achanganye na kijiko kimoja cha sabuni ya unga," anasema na kuongeza:

"Baada ya hapo achukue kilo moja ya unga wa mwarobaini, aweke kwenye lita 10 ya maji, akoroge ili kuleta mchanganyiko mzuri wa dawa, halafu aifunike kwa muda wa saa 24."

Pili anasema kinachotakiwa baada ya hapo, ni kuichuja mara mbili kwa kutumia mfuko wa 'Sandalusi', na kisha mara ya tatu kwa kutumia kitambaa laini, ndipo inakuwa tayari kwenda kunyunyiziwa shambani.

"Cha kuzingatia katika utengenezaji wa dawa hii ni kuhakikisha majani hayo unayaanika kwenye ubaridi tu mpaka yakauke na jinsi ya kuweka unga na maji, vipimo vya maji na dawa," anasema.

### MATUMIZI YAKE

Pili anasema dawa hii ya asili inapaswa kunyunyiziwa shambani muda wa kuanzia saa 12 mpaka saa mbili asubuhi au jioni saa 1:30 au saa mbili ambapo wadudu huwa wamejikusanya kwenye mmea.

### DAWA YA ASILI KUTUMIA NDULELE

Pili anataja pia namna ya kutengeneza dawa ya asili kwa kutumia tunda pori lijukanalo kana ndulele.

Anasema dawa hiyo inatengenezwa kwa kutumia ndulele (Solanum sp) ambalo ni tunda pori.

"Unakatakata vipande vidogo vidogo, halafu unakausha kwenye ubaridi si katika jua kali...ikishakauka unatwanga, halafu unachukua unga wa ndulele unachanganya na kijiko kimoja cha sabuni ya unga," anasema na kuongeza:

"Halafu unakoroga kwenye maji, unafunika kwenye chombo chenye mfuniko kwa muda wa saa 24, kisha unachuja mara mbili kwa kutumia mfuko wa sandalus, mara tatu kwa kitambaa laini, hapo inakuwa tayari kwa kwenda kunyunyizia shambani.

### KUHIFADHIA MAZAO

Pili anataja faida nyingine akisema kwamba teknolojia hii inaweza kutumika kutengeneza dawa zingine za asili kwa ajili ya kuhifadhia mazao.

Anasema ili kupata dawa ya asili ya kuhifadhia mazao, mtu anatakiwa kuchukua unga wa mwarobaini, ndulele na bangi ya mbwa na kuchanganya.

"Hapo inakuwa tayari ni dawa kwa ajili ya kuhifadhia mazao kama vile mahindi, kunde, mbaazi, mtama, ngwala na mazao mengine," anasema.

### MAYUDE

Naye mkulima kutoka Kijiji cha Ntunduu, Kata ya Kinyeto, Kassim Mayude anasema wanaishukuru ActionAid Tanzania, na wadau wengine kwa kuleta elimu hiyo ya kutengeneza dawa za asili kwa ajili ya kilimo.

Mayude anasema elimu hiyo imeleta mabadiliko makubwa katika shughuli zake za kilimo, lakini imewaongezea pia ujuzi zaidi wa kutengeneza dawa zingine ya asili.

Anasema mradi wa SNAP umewafundisha kutengeneza dawa za asili kwa kutumia bangi pori, mwarobaini, ndulele pamoja na majivu ya mti kwa muda wa wiki mbili.

"Baada ya mafunzo tulinyunyizia dawa tulizotengeneza kwenye mikunde na mbaazi kwa sababu ndiyo mazao yanayoshambuliwa sana na wadudu, akiwamo mdudu Kantangaze kwenye zao la nyanya.

"Mdudu aina ya Kantangaze anaanza kushambulia kunde wakati zikiota na mbaazi wakati wa maua," anasema.

Mayude anasema dawa za asili zimesaidia kupunguza wadudu kwenye zao la kunde, kwani mara nyingi huwa haziwauwi wadudu wanaoshambulia kunde, ila huwafukuza wadudu kwa sababu ya harufu yake kali.

"Mpaka sasa mimi ni mkulima wa mazao ya uwele, kunde, mahindi, maharage, mbaazi, alizeti, nyanya, vitunguu, 'Chainizi' na bamia," anasema.

Mayude anabainisha kuwa kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019, ametenga ekari tatu kwa ajili ya kilimo cha ulezi, kunde na vitunguu.

> Kabla ya kuanza kutumia dawa za asili, mdudu huyu alikuwa anatusumbua sana…

"Baada ya kuona dawa za viwandani zina madhara kwa binadamu, tuliamua kuingia kwenye utengenezaji wa dawa za asili kwa kutumia pilipili, sabuni ya kipande na mafuta ya kupikia," anasema na kuongeza.

"Vitu hivi vinatakiwa kuwa vimesagwa kwa ajili ya kuchanganyika haraka na ndiyo maana sabuni kwa ajili ya povu, pilipili kwa ajili ya uchungu/ukali na mafuta kwa ajili ya kuteleza, hivyo mdudu hushindwa kula mmea kutokana na utelezi."

Mayude anasema wameanza kutumia dawa hizi za asili mwaka jana kwenye mazao ya nyanya, bamia na mbogamboga na zimefaa kwenye mazao ya kunde, mtama na mahindi.

Anabainisha kwamba sisimizi weusi wanaoshambulia mikunde, hufukuzwa na dawa hii shambani.

"Lakini katika kumdhibiti mdudu aina ya Kantangaze, unatakiwa kuchanganya mwarobaini, bangi ya mbwa, mwalovera na ndulele... na unatakiwa kupulizia asubuhi sana saa 12 wakati bado yupo kwenye mmea na jioni saa 12 jioni au saa moja, akirudi kwenye mmea ili afe hapo hapo."

### NI MSUMBUFU

Mayude anasema mpaka sasa mdudu anayewasumbua hata wakitumia dawa za viwandani ni Kantangaze.

"Kabla ya kuanza kutumia dawa za asili, mdudu huyu alikuwa anatusumbua sana...tulipokwenda katika maduka ya pembejeo za kilimo, walitushauri tutumie dawa aina ya BELT," anasema na kuongeza:

"Hii dawa ni kali sana na sisi kama wakulima tunahofia kupata maradhi kwa sababu ni dawa ya kiwandani."

### UGHALI WA DAWA

Mkulima huyu anasema kuwa hata kwa upande wa gharama, dawa hii ni ghali.

"Ipo kwenye ujazo wa milimita 50, bei ni shilingi 35,000 na wananchi wengi hawawezi kumudu kwa sababu ni ghali sana," anasema.

### ATHARI ZA KIAFYA

Mayude anasema, hata kwa upande wa kiafya, mkulima anashauriwa kwamba akiitumia kwenye zao la nyanya asiingie shambani kwa muda wa siku tatu, na mazao yake yasitumike kwa muda wa siku saba.

"Ina maana baada ya hizo siku saba ndiyo unaruhusiwa kula hayo mazao...yaani zao lolote ambalo litapuliziwa kwa kutumia dawa hii linatakiwa kuliwa baada ya siku saba kupita," anasema na kuongeza:

"Na sisi kama wakulima wa nyanya, mikunde, mahindi na mazao mengine, baada ya kuona kuwa dawa hii ina masharti na ni kali, tuliamua kujikita katika utengenezaji wa dawa za asili."

### FAIDA

Mayude anasema dawa za asili zimeleta mafanikio makubwa kutokana na faida zake mbalimbali.

INAENDELEA UK.18

---

JIELIMISHE

## HRW: Waathirika unyanyasaji kingono

RIPOTI ya Shirika la Muungano wa Ulinzi wa Elimu dhidi ya mashambulizi kwa kushirikiana na Human Rights Watch (HRW), inasema wasichana walikumbwa na unyanyasaji wa kingono wakati wanamgambo walipozishambulia shule huko Kasai.

Vurugu hizo ziliathiri watoto wote, lakini wasichana ndio walikuwa waathirika wakubwa wa unyanyasaji ikiwamo kubakwa na kuolewa na wanamgambo.

Ripoti hiyo yenye kurasa 76 imezingatia mahojiano 55 yaliyofanywa na wanafunzi wa kike, walimu na wakuu wa shule ambazo zilishambuliwa katika mkoa huo.

Wanafunzi na walimu wa kike walibakwa na kulazimishwa kuolewa na wanamgambo.

Baadhi yao walilazimishwa pia kujiunga na makundi ya wapiganaji wakitumika kama ngao katika uwanja wa mapambano bila ya kujihami, kwa sababu iliaminika kuwa wasichana hao walikuwa na ulinzi wa nguvu za kimazingara kuvilinda vikosi hivyo vya wanamgambo.

Watoto wengi wanaaminika kuuawa na vikosi vya usalama vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), pamoja na wasichana ambao walitumiwa kama ngao.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Jeshi la Congo FARDC pia lilishambulia shule takribani 38 katikati mwa mkoa wa Kasai na kufanya uhalifu wakati walipolilenga kundi la wanamgambo la Kamuina Nsapu.

Uhalifu huo ni pamoja na kuwalenga raia, utekaji, ubakaji na unyanyasaji mwingine.



Ripoti inaonyesha kinamama ndio walikuwa waathirika wakubwa wa vitendo hivyo. **PICHA: MTANDAO**

Maofisa kadhaa wa jeshi hilo wanashukiwa kufanya uhalifu ikiwemo mauaji na unyanyasaji wa kingono Mashariki mwa DRC, kati ya mwaka 1998 na 2013.

Ripoti inaeleza kuwa pande zote, yaani Jeshi la DRC na lile la Kamuina Nsapu, walitumia shule kwa ajili ya shughuli za kijeshi.

Mkurugenzi wa Muungano wa Ulinzi wa Kimataifa wa Elimu, Diya Nijihowne aliieleza DW kuwa.

"Mamia ya shule zilivamiwa kwasababu ziliwakilisha majengo ya kiraia, kwa hiyo ilikuwa rahisi kulengwa na wanamgambo…wasichana walibakwa, kutekwa na kusajiliwa na makundi ya wanamgambo ambao waliamini kuwa wasichana wana nguvu za kichawi," anasema.

Walimu na wanafunzi hawakuwa na taarifa za kutosha kuhusu mashambulizi na mara nyingi mashambulizi yalikuwa ya kushutukiza.

Wakuu wa shule na walimu wanasema hawakupokea taarifa yoyote juu ya tishio la mashambulizi kutoka kwa mamlaka za mkoa na serikali au hata vikosi vya usalama katika mkoa huo.

Kwa maana hiyo hawakujua jinsi ya kukabiliana na kujilinda dhidi ya mashambulizi, wala mafunzo ya kiusalama au taarifa juu ya hatari ambazo zingejitokeza.

Ingawa wavulana na wasichana wote elimu yao ilitatizwa, wasichana waliathirika zaidi kwasababu ya kushindwa kurejea shuleni.

Mzozo huo ulisababisha hali ya kiuchumi katika mkoa huo kuwa mbaya sana. Wazazi waliposhindwa kuwalipia karo watoto wote, ilibidi wachague kuwalipia ada watoto wa kiume kuendelea na masomo.

Mei 2016, serikali ya DRC ilichukua hatua muhimu za ulinzi wa elimu kwa kuidhinisha mkataba wa kimataifa wa usalama wa shule, ambao una wajibu wa kuwalinda wanafunzi, walimu na vyuo dhidi ya mashambulizi ya vikosi vilivyo na silaha sambamba na makundi ya wanamgambo.

Nijihowne anasema licha ya kuridhia mkataba huo ni lazima uchunguzi ufanyike na wahusika wawajibishwe.

Tangu Mei 2017, nchi 87 duniani kote zimetia saini mkataba huo wa kimataifa wa Usalama wa shule. **DW**

UTAFITI

# Facebook yafunga akaunti bilioni 3 za watumiaji wake

MTANDAO wa Facebook umechapisha orodha ya mabilioni ya akaunti feki ilizozichukulia hatua, kati ya Oktoba 2018 na Machi mwaka huu.

Katika kipindi hicho cha miezi sita, Facebook ilifunga zaidi ya akaunti bilioni tatu feki, idadi ambayo inasema ni kubwa zaidi kuwahi kufungwa.

Zaidi ya jumbe milioni saba za "chuki" pia zilitolewa katika mtandao huo wa kijamii.

Kwa mara ya kwanza, Facebook inaripoti kuwa baadhi ya watumiaji wa mtandao huo ambao ujumbe wao ulifutwa wamekata rufani na kuongeza kuwa zingine zilirudishwa baada ya uchunguzi wa kina.

Akizungumza na vyombo vya habari, mwanzilishi wa mtandao huo Mark Zuckerberg, aliwakosoa vikali wale wanaotoa wito kampuni hiyo ifutwe, akiongeza kuwa wanafanya kila wawezalo kukabiliana na changamoto zinazoibuka.

"Sidhani suluhisho ni kuvunjilia mbali kampuni kwa sababu tunashughulikia tatizo hilo," anasema na kuongeza:

"Ufanisi wa kampuni hii umetuwezesha kufadhili mpango huu kwa kiwango kikubwa...kiwango cha fedha tunazotumia kuimarisha usalama wa mtandao wetu ni kikubwa kuliko 'mapato ya mwaka mzima' ya mtandao wa Twitter."

**AKAUNTI BANDIA**

Facebook inasema kumekuwa na ongezeko la akaunti bandia kwa sababu 'wahalifu' wamekuwa wakitumia mfumo maalum kuzifungua.



Mwanzilishi wa mtandao wa Facebook, Mark Zuckerberg. **PICHA: MTANDAO**

Lakini ikaongeza kuwa ilifanikiwa kuzigundua na kuzifuta zote katika kipindi cha dakika moja, kabla hawajapata nafasi ya kuzitumia kufanya uhalifu.

Mtandao huo wa kijamii pia utaripoti posti zilizotolewa kwa kuuza "bidhaa ambazo zimedhibitiwa" kama vile bunduki na dawa.

Aidha, imebainisha kuwa iliwachukulia hatua watumiaji milioni moja wa mtandao huo kwa kuuza bunduki katika miezi hiyo sita, kipindi ambacho ilichukua kuandaa ripoti hiyo.

Ripoti hiyo pia ilikadiria idadi ya jumbe, kama zile zinazoangazia unyanyasaji watoto, ghasia na propaganda kuhusu ugaidi, zinazowafikia wateja wake.

Uchunguzi huo ulibaini ni mara ngapi posti 10,000 zilizo na ujumbe huo zilionekana kwenye Facebook:

Kwamba watu wachache, kati 14 waliona picha za utupu.

Kwamba karibu watu 25 waliona taarifa zilizo na ujumbe wa kuchochea ghasia.

Kwamba wachache kati ya watu watatu waliona taarifa zilizo na ujumbe wa unyanyasaji wa watoto na propaganda kuhusu masuala ya ugaidi.

Kwa ujumla, karibu asilimia tano ya watumiaji wa mtandao huo wanafanya hivyo kupitia akaunti feki.

# Dawa za asili kuua wadudu waharibifu

INATOKA UK.17

"Dawa hizi hazitumii gharama kubwa wakati wa kutengeneza...unaweza kuzitumia kuhifadhi mazao kudhibiti wadudu wanaopekecha mazao, ukitumia dawa hizi hawaingii tena," anasema na kuongeza:

"Lakini pia dawa hizo hazina madhara kwa binadamu na muda wa kutumia kwa sababu ukiweka leo unaweza kutumia mazao hayo."

**PILI AUNGA MKONO**

Faida hizi za matumizi ya dawa za asili kwenye kilimo zinabainishwa pia na Pili kama walivyofundishwa wakati wa mafunzo.

"Kwanza dawa hizi haziuzwi, wadudu rafiki wa mazao na zinafukuza wadudu waharibifu...lakini pia zinarutubisha udongo na makapi yanayopatikana wakati wa kuzitengeneza, yanaweza kutumika kama mbolea," anasema na kuongeza:

"Wakulima wengi katika wilaya yetu wameacha kutumia dawa za viwandani, wanatumia za asili na hivi sasa tunataka kuanzisha soko la dawa hizi kwa sababu zinarutubisha udongo na hazina madhara kwa binadamu kama zile za viwandani."

Anabainisha dawa za viwandani zina sumu ambazo ni chanzo cha kuzaa watoto wenye mtindio wa ubongo au kuzaa watoto kabla ya muda.

"Ni wachache wanaoendelea kutumia dawa za viwandani katika wilaya yetu, kwa sababu inachukua muda kwa watu wengine kuelewa unavyokuwa unamfundisha... ila kadri tunavyoendelea kutoa elimu, naamini wataacha kabisa kutumia dawa za viwandani," anasema.

**CHANGAMOTO**

Pili anasema ingawa wamepata mafunzo ya utengenezaji wa dawa za asili, changamoto kubwa ni ile ya wadudu sugu kwa baadhi ya mazao kama vile mbaazi.

"Yaani imekuwa vigumu kwa dawa za asili kuua hao wadudu au kuwafukuza kwenye zao la mbaazi... ukinyunyizia dawa wanachukua muda mrefu kuhama au kufa kwa sababu dawa zetu za asili zinafukuza tu na kuua kwa kiasi kidogo," anasema na kuongeza:

"Mdudu wa mbaazi anashindwa kutoka kwenye mbaazi kwa sababu mmea ukianza kutoa maua na mbaazi zikiwa bado ndogo tu, ndiyo mdudu anaanza kushambulia mbaazi."

Changamoto nyingine anayoitaja ni ile ya wakulima kutumia vifaa duni katika kutayarisha dawa hizo na kusababisha kuchelewesha kutoa matokeo ya haraka katika kuua au kuwafukuza wadudu waharibifu wa mazao.

"Vilevile mabadiliko ya tabianchi bado yanaendelea kuathiri shughuli za kilimo na hali hii inasababisha kutoleta matokeo mazuri katika mavuno," anasema na kuongeza:

"Kupitia elimu hii nimeweza kudhibiti wadudu waharibifu katika zao la mahindi, kunde, karanga na ngwala."

## JE, WAJUA?

# Homoni ya progesterone 'inaweza kupunguza, kupoteza ujauzito'



Samantha Allen na mwanawe Noah. **PICHA: MTANDAO.**

WANAWAKE ambao wamewahi kupoteza ujauzito au waliovuja damu katika miezi ya awali ya ujauzito, wanaweza kuimarisha nafasi yao ya kujifungua salama iwapo watapewa homoni ya progesterone, utafiti unaonyesha.

Watafiti nchini Uingereza wamefanya majaribio kwa wanawake 4,000 wenye mimba.

Samantha Allen, mwenye umri wa miaka 31, alianza kuvuja damu alipompoteza mwanawe wa kwanza na alifanya hivyo tena alipokuwa mjamzito kwa mara ya pili. Baada ya kupewa homoni hiyo kwa wiki nane, alimzaa mwanawe wa kiume Noah.

Progesterone ni homoni muhimu wakati wa ujauzito, inayotumika kuimarisha uzio wa kizazi ambako ni sehemu kuna kijusi kinachojiambatanisha na kusaidia mfumo wa kinga mwilini.

Samantha alipewa tembe za homoni ya progesterone kwa majaribio, ambazo alizitumia mara mbili kwa siku mpaka alipotimiza wiki 16 za ujauzito.

Alisema aliacha kuvuja damu wiki moja tangu aanze kutumia tembe hizo na aliendelea vizuri na ujauzito wake. Sasa anatumaini kwamba wanawake zaidi waliopoteza ujauzito watanufaika.

"Natumaini hawatoteseka tena, kwani inakuathiri sana, anasema.

Mwanamke mmoja kati ya watano hupoteza mimba, na mara nyingi uvujaji damu unahusishwa na kuongezeka kwa hatari ya mwanamke kupoteza ujauzito. Wakati homoni hiyo tayari imetumika katika mfumo wa kupachika mimba (IVF), Samantha anasema hakuwa na shida yoyote kushiriki katika utafiti huo.

"Ninafurahi, sikuhisi hatari yoyote kwa sababu hayakuwa majaribio ya kiwango cha awali," anasema.

Utafiti huo wa Chuo Kikuu cha Birmingham uliochapishwa katika jarida la afya la New England, umewahusisha kundi la wanawake 200 wajawazito waliopewa homoni ya progesterone, huku kundi jingine la wanawake kama hao wakipewa tembe bandia.

Wote walikuwa wanavuja damu katika miezi ya kwanza ya ujauzito.

Licha ya kwamba utafiti huo umeonyesha si wanawake wote wanaovuja damu katika siku za kwanza wanaweza kusaidiwa kwa kutumia homoni hiyo, manufaa hayo ni makubwa miongoni mwa wanawake walio na historia ya kupoteza ujauzito. (Watoto watatu au zaidi) Miongoni mwa wanawake hao, kulikuwa na ongezeko la asilimia 15 la wanawake waliojifungua, huku wanawake 98 kati ya 137 wakifanikiwa kujifungua ikilinganishwa na wanawake 85 kati ya 148 waliopewa tembe hizo bandia.

Arri Coomarasamy, daktari wa afya ya uzazi katika hospitali ya kinamama na watoto ya Birmingham, anasema matibabu hayo huenda yakasaidia kuokoa maisha ya maelfu ya watoto.

Anaendelea kueleza kwamba matibabu hayo hata hivyo hayatofanya kazi kwa wanawake wote wanaopoteza ujauzito, kwa sababu kuna sababu nyingi na ngumu kuhusu kwanini wanawake hupoteza ujauzito.

Ni wanawake walio na tatizo la upungufu wa homoni ndio wanaoweza kufaidika. **BBC**

SHERIA

NA FRANSISCO MPANGALA

# Mambo ya msingi ya kufahamu katika mchakato wa kukamatwa

KATIBA ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 15 (2) inasema: "Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo isipokuwa (a) Katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au (b) Katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na Mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai."

Tafsiri ya ibara hii ni kuwa hairuhusiwi kwa mtu yeyote au chombo chochote kunyang'anya uhuru wa mtu kuwa huru (kukamata) kinyume na njia zilizoainishwa na sheria zetu za nchi au wakati wa kutekeleza amri ya mahakama.

Busara ya ibara hii ni kutoa fursa kwa kila mtu ndani ya nchi kupata nafasi ya kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo yake binafsi na yale ya kijamii kwa uhuru wa kwenda mahali popote bila kuzuiwa au kupata kizuizi chochote.

Ni vigumu kwa mtu kushiriki katika shughuli za maendeleo kama hayuko huru au amezuiwa kwenda mahali popote anakoona kunafaa kujipatia riziki. Kwa maana hii, ni lazima ziwepo taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa wakati wa kuiondoa haki hii.

Tuna wajibu wa kuepuka kufanya makosa ambayo yatatufanya tukamatwe na kuondolewa haki hii ya kikatiba ya kuishi kama mtu huru.

Hata hivyo, pamoja na kwamba tunaweza kujitahidi kuepuka kufanya makosa, maisha nayo hayatabiriki.

Yumkini unaweza kukamatwa kimakosa au likatokea jambo lolote lisilotarajiwa litakalokufanya ukamatwe. Na hata usipokamatwa, yumkini mtu yoyote wa karibu kama rafiki, ndugu au jirani anaweza kukamatwa. Kimsingi, kukamatwa ni jambo linaloweza kumtokea mtu yoyote.

Kwa maana hii, ni muhimu kupata taarifa za kutosha zinazohusiana na kukamatwa. Taarifa hizi zitakupa mwongozo wa kujua haki na wajibu wako pale unapokamatwa au mtu wako wa karibu anapokamatwa.

Kwa maana hii, yafuatayo ni baadhi ya mambo ya msingi ya kufahamu pale mtu yoyote anapokamatwa.

**MAANA YA KUKAMATWA**

Kumkamata mtu kwa mujibu wa sheria ni kitendo cha kumuondolea mtu uhuru wake wa kufanya harakati zake za kila siku kwa kumpeleka kwenye kizuizi kinachotambulika kisheria.




Mtuhumiwa anawekwa kizuizini ili apelekwe mahakamani (mapema kwa kadri itakavyowezekana) kujibu mashtaka ya jinai yanayomkabili.

Anaweza pia kuwekwa kizuizini kwa lengo la kufanyiwa upelelezi juu ya mashtaka ya jinai yanayomkabili.

**KUMKAMATA MTUHUMIWA**

Sura ya 20 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, ndiyo sheria inayotoa mwongozo wa namna na jinsi ya kumkamata mtu.

Kwa kawaida kukamatwa kunahusisha kugusa au kumshika mtuhumiwa kwa namna itakayomfanya mtuhumiwa ashindwe kumtoroka au kumkimbia mtu aliyemkamata.

Kama mtu anayekamatwa atajaribu kukimbia au kufanya jaribio la kuzuia tendo la ukamatwaji halali kufanyika, mtu au ofisa anayemkamata anaruhusiwa kutumia nguvu kiasi.

Ukamatwaji haupaswi kuendeshwa kwa maslahi binafsi, ukamatwaji unatakiwa kufanywa kwa nia njema, ukizingatia utu, usiri na haki za binadamu. Mkamataji anapaswa kutanguliza maslahi ya kutenda haki wakati anamkamata mtuhumiwa.

**AINA ZA UKAMATAJI**

Kuna aina mbili za ukamataji ambazo ni kumkamata mtu kwa kutumia kibali na kumkamata mtu bila kutumia kibali.

**KIBALI**

Ukamatwaji unaotumia kibali kwa kawaida unatolewa na hakimu, katibu kata au katibu wa halmashauri ya kijiji baada ya kupokea taarifa iliyo chini ya kiapo ikimtuhumu mtuhumiwa kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kwamba mtu husika ametenda kosa.

**BILA KIBALI**

Ukamatwaji usio na kibali ni ule unaofanywa pale makosa kama uvunjifu wa amani mbele ya polisi au hakimu yanapotokea, kumzuia ofisa wa polisi kutekeleza majukumu yake au kitendo chochote kinachoazimia kutusi nembo ya taifa au bendera ya taifa.

**SABABU ZA MTU KUKAMATWA**

Polisi au ofisa anayemkamata mtuhumiwa ana wajibu wa kutaja kosa au kutoa sababu zinazomfanya amkamate mtuhumiwa.

Ieleweke kuwa si kila kosa linaweza kukufanya ukamatwe (na hasa makosa ya madai). Zifuatazo ni baadhi ya sababu zinazoweza kumfanya mtu akakamatwa.

**MAKOSA YA JINAI**

Kwanza, makosa ya jinai kutegemeana na aina au uzito wa kosa ambalo mtuhumiwa ametuhumiwa kulifanya. Endapo mtuhumiwa atadhaniwa kufanya kosa la ugaidi, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha na makosa mengineyo ya jinai, yatamfanya akamatwe mara moja.

**KUDHARAU KUTII AMRI HALALI YA MAHAKAMA**

Sababu ya pili inayoweza kumfanya mtu akamatwe ni kudharau kutii amri halali ya mahakama au kukwepa kwa makusudi kufikiwa na wito wa kufika mahakamani.

Yumkini mtuhumiwa ameitwa mara kadhaa mahakamani au amekataa kupokea wito, basi mtuhumiwa anaweza kukamatwa kwa kosa hili.

> "Ukamatwaji ulio kinyume na sheria ni unaofanywa kinyume na vipengele vya kisheria vilivyopo kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinavyoelekeza namna na jinsi ya kumkamata mtuhumiwa.

**UHAI NA USALAMA WA MTUHUMIWA**

Ulinzi wa uhai na usalama wa mtuhumiwa inaweza kuwa sababu ya tatu itakayomfanya mtu akamatwe.

Mtuhumiwa anaweza kufanya tukio linaloweza kuibua hasira kali kwenye jamii na hivyo wananchi wakataka kuchukua hatua mkononi.

Kama polisi amejiridhisha kuwa uhai wa mtuhumiwa uko hatarini, mtuhumiwa anaweza kukamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda ili kulinda uhai na usalama wa maisha yake.

**USALAMA WA JAMII**

Ni sababu nayo inayoweza kumfanya mtu kukamatwa. Kwamba pale usalama wa jamii na watu wengine unapokuwa hatarini.

Yaani mtu husika ana matatizo ya akili au ni mtu anayependa kufanya vurugu, kuharibu mali na kujeruhi watu.

Polisi na viongozi wa maeneo husika wakijiridhisha kuwa anavyoendelea kuwa uraiani atazidi kufanya uharibifu nayo inaweza kuwa ni sababu ya kumkamata mtu husika.

Lengo la ukamatwaji huu ni kumdhibiti mtu husika asiendelee kufanya uharibifu.

**UKAMATWAJI KINYUME NA SHERIA**

Ukamatwaji ulio kinyume na sheria ni unaofanywa kinyume na vipengele vya kisheria vilivyopo kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinavyoelekeza namna na jinsi ya kumkamata mtuhumiwa.

Ukamatwaji wa aina hiyo pamoja na mambo mengine unahusisha kumkamata mtu bila kuwa na mamlaka ya kisheria na kumkamata mtu bila kumtaarifu sababu za kumkamata.

Aidha, kutumia nguvu kubwa (zilizopitiliza) kumkamata mtu bila sababu za msingi na kumuweka mtuhumiwa kizuizini kwa muda mrefu tofauti na mahitaji ya kisheria yanavyotaka.

Mtuhumiwa anatakiwa apelekwe mahakamani ndani ya saa 24 au kuachiwa kwa dhamana. Vitendo vya kikatili au vitendo vilivyo kinyume na haki za binadamu wakati wa ukamatwaji navyo haviruhusiwi kwa mujibu wa sheria.

**MADHARA**

Yapo madhara kwa polisi au ofisa kumkamata mtuhumiwa kwa namna iliyo kinyume na sheria.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Wadau wanajadili

## MOJA ya matukio ambayo bado yanaisumbua jamii ni yale yanayohusiana na imani za kishirikina. Elimu inayotolewa nchini haijafanikiwa kuondoa imani hizo?



**NEMES TEMBE (MWENYEKITI WA CHAMA CHA ALBINO TANZANIA)**

BINAFSI mada hii imenigusa sana. Unaposema elimu, maana yake inajumuisha ufahamu na mengine ya msingi ambayo mwanafunzi anayapata shuleni kwa ajili ya kuyatumia katika jamii inayomzunguka.

Kimsingi elimu inatolewa lakini inategemea ni jinsi gani wanafunzi wanavyoipokea. Wapo ambao wameipokea vizuri ikawa na manufaa kwao na pia wapo wale walioiweka pembeni na kuamua kufanya mambo yanayokwenda kinyume na elimu waliyopata ingawa pia kuna kundi lingine ambalo halikubahatika kupata elimu kabisa.

Watu walioamua kutumia elimu yao vibaya na wale ambao hawakubahatika kuipata ndio wamekuwa wakijihusisha na vitendo visivyofaa ndani ya jamii na hasa vya kuamini mila potofu hadi kuua watu wenye ulemavu wa ngozi kwa lengo la kupata utajiri na wengine kuua watu wenye macho mekundu wakiamini kwamba ndio wanaowaloga.

Mimi ninadhani ni vyema sasa pamoja na elimu ya shuleni, jamii ipate elimu nyingine ya kuiwezesha kuachana na matendo yanayohusiana na imani za kishirikina.

Cha kushangaza ni kwamba hadi litokee tukio ndipo jamii inahamasishwa kuachana na imani za aina hiyo, lakini kwa mtazamo wangu ni kwamba jamii inatakiwa kuhamasishwa kila mara.

Kwa utaratibu huo nina uhakika kunaweza kuwapo na mabadiliko makubwa kutoka katika matendo hayo na kuwa watu wema.



**BAKARI CHIKOJO (MKAZI WA LIWALE MKOANI LINDI)**

MWALIMU (Julius) Nyerere ambaye ni mwasisi wa dhana ya elimu ya kujitegemea alichukua hatua moja mbele zaidi na kuainisha umuhimu wa kumwandaa mtoto anapokuwa shuleni ili aanze kujitegemea kwa kiasi fulani huko shuleni.

Mwalimu kama ilivyo kwa mambo mengi aliona mbali zaidi ya wengi wetu tunavyoona.

Alijua kwamba Watanzania sio tu wana rasilimali nguvukazi bali pia kuna msururu wa vitu wanavyoweza kuvifanya wao wenyewe kwa kutumia nguvu na akili zao za kuzaliwa. Haya yalikuwa ni mawazo ya kimaendeleo na kimapinduzi.

Laiti yangelifanyika kwa moyo safi kama Nyerere alivyotumaini, yangelichangia kutuweka katika daraja la juu zaidi kuliko tulivyo sasa. Bahati mbaya viongozi na walimu wakorofi wachache wakachakachua dhana ya elimu ya kujitegemea. Uongozi wa baadaye wa Tanzania ukaamua kuacha na kuturudisha nyuma zaidi kimaendeleo.

Matokeo yake ni kutafuta maisha hata kwa kuua watu wengine kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia. Wapo wanaoamini kwamba kuua ndio njia pekee ya kutajirika.

Mbaya zaidi ni matukio ya kuua watu wazima kwa kuamini kwamba mtu mzima akiwa na macho mekundu ni lazima atakuwa mchawi!

Binafsi huwa ninashangaa sana kusikia matukio ya aina hii ambayo hayakuwapo zamani, lakini wakati huu ambao serikali imejenga shule kila sehemu tofauti na zamani ndio yanaibuka.



**FATUMA MACHONGWE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

TANZANIA inakabiliwa na changamoto ya kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi bila kujengewa vyema stadi za kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Changamoto hiyo inasababisha kuwapo kwa ongezeko la wahitimu wa elimu ya msingi wanaohitimu ngazi hiyo ya elimu bila kuwa na stadi za KKK, hali inayochangia kuwapo kwa ongezeko la idadi ya wajinga nchini na hivyo nchi kukosa maarifa na kusababisha ongezeko la umaskini miongoni mwa jamii yetu.

Ikumbukwe kuwa sekta ya elimu ni miongoni mwa sekta zinazokabiliwa na changamoto nyingi ingawa kwa sasa serikali imeamua kutoa elimu bure kwa lengo la kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anasoma.

Lakini kuna haja ya kuboresha maslahi ya walimu ili waweze kufundisha kwa moyo. Iboreshe mazingira ya kazi, na pia mishahara inayokidhi hali halisi kwenye utumishi wa umma na kuongezwa posho ya kufundishia na mahitaji mengine muhimu ili ufundishaji uwe mzuri na hiyo inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza hizo changamoto za kuwa na watu wanaoendekeza mambo ya imani potofu, kwa kuwa watakuwa wamesoma na kuelimika vizuri.

Binafsi ninaamini kwamba chanzo cha imani potofu ni adui ujinga ambaye tulitangaza kumpiga vita mara baada ya nchi kupata uhuru mwaka 1961. Tunaweza kufanikiwa kuondoa mila potofu katika jamii kwa njia ya elimu.



**JUSTA MWAITUKA (MKURUGENZI WA KOWOHEDE TANZANIA)**

ELIMU ya Tanzania ni elimu inayonyumbulisha mambo mengi yanayotaka ufahamu wa mwanafunzi. Mitaala yake ni shirikishi, kwa maana ya kuwa inahusu masomo mengi ya kujenga ufahamu na kupata maarifa na elimu pana.

Ndiyo maana utaona pamoja na sisi Watanzania kujidharau, lakini utajua elimu yetu pia ni elimu ya uwakilishi wa kidiplomasia, kidemokrasia na kiutawala. Utaona kuwa tumefikia kutoa viongozi wa kidunia.

Suala la kuwa na imani potofu si suala la kuwa na elimu ama la, bali ni Watanzania kukengeuka kimaadili na kuwa na hisia za kichawi. Kumbuka kikombe cha babu, kumbuka binadamu kugeuka nyoka, kumbuka imani ya kuua albino kwa ajili ya utajiri.

Haya yote hayasababishwi na watu kukosa elimu bali watu kuwa na imani potofu. Kubadilisha haya panahitajika mjadala wa kitaifa. Kwa nini tuna imani potofu?

Kwa nini tunachukua sheria mkononi? Tunajenga taifa gani? Urithi gani tunawapa watoto wetu? Kwa nini hivi sasa jamii ina hasira na haithamini uhai wa mtu mwingine? Wapi tumekosea?

Mijadala hii iwe kwa nyanja zote, ngazi ya familia, mtaa, kijiji, kata, wilaya hadi taifa. Lazima tukatae ujinga na imani za kishirikina. Haya ni zaidi ya elimu ya darasani, ni matatizo ya kisaikolojia zaidi.



**AMANI NACKSON (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

UJINGA ni moja ya maadui ambao baada ya kupata uhuru mwaka 1961, serikali iliwatangazia vita ya kuwakomesha. Maadui wengine ni maradhi na umaskini, ambao ni lazima kupambana nao ili kuwatokomeza nchini kwa manufaa ya taifa hili.

Ninaweza kusema kuwa elimu imefanikiwa kuondoa imani potofu nchini, ingawa wapo watu wachache ambao kwa sababu zao wenyewe hawataki kubadilika. Hii inatokana na ukweli kwamba si rahisi watu wote kukubali jambo hata liwe zuri kiasi gani.

Ninasema hivyo kwa sababu katika jamii bado wapo baadhi ya watu hawaoni umuhimu wa elimu. Ndiyo maana hawapeleki watoto wao shule. Wapo pia wanaowakatisha masomo na kuwaozesha watoto wao ili wapate mahari.

Kundi hili linatakiwa kusaidiwa ili kutoka huko liliko na kuachana na maisha ya aina hiyo. Ikumbukwe kuwa watu wa aina hiyo ambao hawaoni umuhimu wa elimu ndio wepesi wa kurubuniwa na kujikuta wakijihusisha na matukio ya hatari, ambayo kama wangekuwa wameelimika wasingekubali kuyafanya hata kama wanaishi maisha duni.

Hebu fikiria eti mtu anakwenda kumuua mwenzake kwa kuamini kwamba ni mchawi baada ya kumuona ana macho mekundu! Kwa mtu aliyesoma akaelimika hawezi kufanya upuuzi huo.



## HABARI MBEYA

# Waomba kujengewa kituo afya

**Na Grace Mwakalinga, SONGWE**

WANANCHI wa Kata ya Mkulwe, Wilaya ya Momba mkoani Songwe, wameiomba serikali kuwajengea kituo cha afya ili kuwanusuru na adha ya kusafiri zaidi ya kilomita 40 hadi 120 kufuata huduma za afya kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe iliyopo mjini Vwawa wilayani Mbozi.

Wananchi hao walisema adha ya kukosekana kwa kituo cha afya, imesababisha wagonjwa wengi kupoteza maisha wakiwa njiani kwa sababu ya kutumia umbali mrefu pamoja na miundombinu mibovu ya barabara.

Nimeiomba serikali kusaidia ujenzi wa kituo hicho eneo lao ambacho kitakuwa msaada mkubwa na kuondokana na vifo vya wagonjwa hususani mama na mtoto.

Stella Kamizi, alisema kukosekana kwa kituo cha afya katika kata yao, kumesababisha wagonjwa kupoteza maisha wakiwa njiani kutokana na miundombinu mibovu ya barabara.

Alisema wako tayari kuchangia nguvu kazi zao kujenga kituo cha afya pia wanategemea msaada wa serikali na wadau wengine kujenga kituo hicho.

"Tuko tayari kuanza ujenzi wa kituo cha afya kwa nguvu zetu, tumepoteza ndugu zetu kwa sababu ya ukosefu wa huduma hiyo... naamini tukianza serikali nayo itatuunga mkono, ombi letu ni kituo hicho kiwe na huduma zote muhimu ikiwamo upasuaji pamoja na huduma za mama na mtoto," alisema Stella.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Juma Irando, alisema serikali imeridhia wananchi kujenga kituo cha afya kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), inayoelekeza kila kata kujengwa kituo cha afya.

Alisema serikali kupitia bajeti na vikao vyake itatoa kipaumbele katika kata hiyo ili kijengwe kituo cha afya ambacho kitawasaidia wananchi kupata matibabu kwa muda mwafaka na kuokoa gharama za kusafiri umbali mrefu kufuata huduma maeneo mengine.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Kheri Kagya, alisema serikali katika kuboresha huduma za afya, imetoa Sh. bilioni 6.7 ili kujenga vituo nane vya afya na hospitali mbili.

**"Tuko tayari kuanza ujenzi wa kituo cha afya kwa nguvu zetu, tumepoteza ndugu zetu kwa sababu ya ukosefu wa huduma hiyo... naamini tukianza serikali nayo itatuunga mkono, ombi letu ni kituo hicho kiwe na huduma zote muhimu ikiwamo upasuaji pamoja na huduma za mama na mtoto," alisema Stella.**

# Wanne matatani tuhuma za mauaji ya ndugu yao

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za mauaji ya ndugu yao yaliyohusishwa na imani za kishirikina.

Aliyeuawa ni Tenson Meta (54), na tukio hilo lilitokea katika Kijiji cha Isangala wilayani Mbeya.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, jana, Mei 17 saa 21.45 usiku katika Kijiji cha Isangala wilayani Mbeya, watuhumiwa kwa makusudi walimuua Meta kwa kumshambulia na vitu butu na vyenye ncha kali kisha kumuweka kwenye buti ya gari na kwenda kumzika wilayani Chunya.

Kamanda Matei aliwataja waliotekeleza mauaji hayo kuwa ni Devi Simbazye (44) ambaye ni mganga wa kienyeji na mkazi wa Isangala, Peter Ndege (43) mkazi wa Kibaoni Wilaya ya Chunya, Ally Mtukwa (51) mkazi wa Itewe Wilaya ya Chunya na Lameck Mwanyanje (39) mkazi wa Majengo wilayani Chunya.

Taarifa ya Kamanda Matei ilifafanua kuwa mganga wa Jadi, Devi Simbazye, alipelekewa Meta na ndugu wa marehemu ambao ni watuhumiwa wakishinikizwa auawe kwa madai ya kuwa mshirikina.

Alisema baada ya kufikishwa kwa mganga huyo alipiga ramli chonganishi zikieleza marehemu kuhusika na mauaji ya ndugu zake. Aidha, Matei alisema Jeshi la Polisi linaandaa utaratibu wa kwenda kuufukua mwili wa marehemu kwa ajili ya uchunguzi, na kwamba wanaendelea na upelelezi ukikamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Mganga wa jadi anayetuhumiwa kuhusikana na mauaji hayo, Devi Simbazye, alidai Meta alimtolea lugha za dharau kwa madai hawezi kumfanya chochote na kumtumia mvua kubwa na nyoka.

Alisema Meta alipozidiwa nguvu akaanza kuumwa, huku na yeye akijitahidi kujiweka sawa ili asidhuriwe.

Katika hatua nyingine Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, linamtafuta dereva wa gari la kusafirisha vipodozi na pombe haramu toka Zambia ambaye amesababisha ajali baada ya kumgonga dereva bodaboda, Emmanuel Kajange, Mei 25 mwaka huu majira ya usiku wilayani Mbeya.



Wachuuzi wa mashuka wakiyanadi kando ya Barabara ya Msimbazi, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanakijiji wagomea mradi wa maji

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANANCHI wa Kijiji cha Mshewe Kata ya Mshewe katika Wilaya ya Mbeya, wamegomea mradi wa maji uliojengwa katika kijiji chao kwa madai kuwa hawakuuhitaji.

Waliyasema hayo juzi kwenye kikao kilichoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP- Mtandao) cha kutathmini shughuli za maendeleo zilizofanyika pamoja na changamoto zake tangu kuanzishwa kwa vituo vya taarifa na maarifa mwaka 2013.

Walieleza miongoni mwa masuala ambayo ni changamoto kwao ni ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika kijiji chao, wakidai hawakuwahi kuomba kwa sababu hakuna changamoto ya maji katika kijiji chao.

Walisema viongozi wanashindwa kuzindua mradi huo kwa kuwa hakuna sehemu ya kupeleka maji hayo katika kijiji na kuongeza kuwa mradi huo ungepelekwa kwenye vijiji ambavyo vina changamoto kubwa ya maji ikiwamo Ilota na Mapogoro.

Sabina Mwalyego alieleza kuwa kijiji hakina changamoto ya maji na kwamba serikali imeingia hasara kuujenga mradi huo, hivyo ingefaa kupelekwa maeneo mengine.

Alisema inawezekana viongozi wa vijiji au kata walikuwa na maslahi binafsi ya kuanzisha mradi huo kijijini hapo ili kujipatia fedha, na kwamba kitendo hicho sio cha kiungwana.

"Sisi wananchi wa Mshewe hatukushirikishwa wakati mradi huo unaanzishwa, laiti tungetushirikishwa tungekataa, wangetuletea mradi mwingine ikiwamo hitaji la kituo cha afya... wametumia gharama kubwa lakini mradi huo hautumiki," alisema Sabina.

Mtafiti kutoka TGNP- Mtandao, Heavensia Nyange, aliwashauri wananchi hao kukaa na viongozi wao kujua namna mradi huo utaweza kutumika kuliko ilivyo kwa kuwa miundombinu ya mradi huo yakiwamo mabomba yanaweza kuharibika.

Alisema miradi mikubwa kama hiyo inapoanzishwa lazima washirikishwe wananchi ili kufahamu kama ni hitaji lao au la ili waweze kunufaika nayo.

Diwani wa Mshewe, Esther Mbega, alisema mradi huo uligharimu Sh. milioni 336, na kabla ya kuingia madarakani mwaka 2015, aliukuta.

Alikiri haukuwa hitaji la wananchi kwa sababu wanayo maji ya kutosha, na kwamba inawezekana miaka ya nyuma kuna baadhi ya viongozi walikaa na kuwasainisha baadhi ya wananchi kuukubali mradi huo ili wajinufaishe.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko ya wananchi kuhusiana na mradi huo na mara kadhaa amekuwa akikutana na wataalamu wa halmashauri kuhusu mradi huo.





## Gharama za kuunganisha umeme zashushwa

**Na Renataha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imepunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi wake, ambayo awali ilikuwa Sh. 177,000 na sasa ni Sh. 27,000.

Akizungumza wakati wa ziara ya kuwasha umeme katika Kijiji cha Chibwegere kilichopo wilayani Mpwapwa jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema serikali imeamua kufanya hivyo ili kutoa fursa kwa kila mwananchi iwe mjini au kijijini kuunganisha umeme.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni mwananchi kuwa na gharama ya kutandaza umeme ndani ya nyumba (wiring), ambayo inafanywa na makandarasi kabla ya Tanesco kufanya kazi ya kuunganisha umeme na kuwasha.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni mwananchi kuwekeza fedha kwa ajili ya kutandaza umeme wakati akiendelea na ujenzi ili anapomaliza ujenzi anakamilisha uwekaji umeme.

Alisema serikali ya awamu ya tano iko pamoja na wananchi wake kuhakikisha wanakuwa na umeme katika maeneo wanayoishi.

Alifafanua kuwa wapo wananchi wanaoishi karibu na miundombinu ya njia ya umeme na sio kwamba wanashindwa kulipa Sh. 27,000 bali wanashindwa gharama ya kutandaza umeme ndani ya nyumba inayofanywa na makandarasi.

"Gharama hizo za wiring zimeonekana kuwa ndio changamoto kwa wananchi na serikali imepokea changamoto hizo na zitafanyiwa kazi," alisema Mgalu.

Aliutaka uongozi wa Tanesco jijini Dodoma na wilayani Mpwapwa kuhakikisha wanakamilisha usambazaji wa umeme kwa wanakijiji ili waweze kunufaika na huduma hiyo.

Naibu Waziri huyo alifafanua kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wanafikisha huduma ya umeme kwa wananchi na hadi kufikia Desemba mwaka huu, watakuwa wamekamilisha kazi hiyo ya kusambaza umeme katika vijiji vya nchi nzima na kubakiza kazi ya kuwaunganishia wananchi.

Naye Mbunge wa Jimbo wa Kibakwe, George Simbachawene, alisema mpaka sasa vijiji 42, tayari vimeshapata umeme huku vikibaki vijiji vinane ambavyo bado havijapata umeme.

Alisema anaishukuru serikali kutokana na kuwawekea umeme wananchi wa jimbo lake na kuongeza kuwa kutokana na jitihada za wizara, vijiji vilivyobaki vitaunganishiwa umeme

# Kanisa launga mkono juhudi za serikali

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KANISA la Mennonite Tanzania limesema kuwa linaunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, katika kupambana na mafisadi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Joseph Mtorela, jijini hapa wakati wa ibada ya maadhimisho ya miaka 85 ya kanisa hilo nchini pamoja na kuweka jiwe la msingi wa ujenzi wa kanisa.

Alisema kanisa hilo linaunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano katika kupambana na mafisadi, rushwa pamoja na udhibiti wa mapato katika maeneo mbalimbali ya nchi.

"Pia tunampongeza Rais Magufuli, kwa miradi mikubwa ya kitaifa ambayo serikali yake hivi sasa inaitekeleza kama vile ununuzi wa ndege, mradi wa kuzalisha umeme wa Stiegler's, treni ya umeme pamoja na mingine mingi," alisema.

Aidha, Askofu huyo alisema kuwa kanisa hilo linapinga mila potofu katika jamii na kuiomba serikali kushirikana nalo katika miradi mbalimbai ya maendeleo. Pia alisema kuwa katika kujenga makao makuu ya nchi mkoani hapa, kanisa hilo linaiomba serikali kuipatia eneo ambao na wao watashiriki katika kujenga ofisi yao pamoja na kuwekeza katika sekta ya elimu na afya.

Vilevile aliwataka viongozi wote wa umma kutenda haki katika maeneo yao kwa kuacha vitendo vya rushwa pamoja na ufisadi.

"Kama viongozi wetu hawa watafanya kazi kwa kumuogopa Mungu kila mmoja wao atatenda haki haijalishi kuwa yeye ni mbunge, waziri, mkuu wa mkoa wote kwa pamoja watatenda haki," alisema.

Akizungumzia kanisa hilo alisema toka lianzishwe limeenea sehemu mbalimbali za nchi na mipaka sasa lina waumini wapatao 65,500.



Wakazi wa Kondoa Mjini, mkoani Dodoma, wakikokota mkokoteni uliobeba nishati ya kuni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, mjini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waeleza changamoto upatikanaji vifungashio

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAJASIRIAMALI mkoani Dodoma ameiomba serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kuweka katika fursa ya viwanda vya utengenezaji wa vifungashio vya kuhifadhi bidhaa zao, ili kuepuka gharama kubwa wanayonunua kutoka kwa wafanyabiashara wanaoagiza nje ya nchi.

Ombi hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa kampuni ya utengenezaji wa bidhaa za asili inayojishughulisha na ujasiriamali (Kemmy Group Produsts Makole), Penina Kaminyonge, alipokuwa akisoma risala fupi kwa niaba ya wajasiriamali wenzake kwenye ufunguzi ya maonyesho ya Dodoma Fair yanayofanyika jijini Dodoma, yaliyoandaliwa na Edodoma Empowerment.

Alisema kuwa wajasiriamali hao wanashindwa kufikia malengo yao kutokana na upatikanaji wa vifungashio hivyo kuwa mgumu na kuiomba serikali kupitia wizara husika kuliangalia suala hilo la kupatiwa viwanda ili waweze kufikia malengo yao ya kujikomboa kiuchumi.

Hata hivyo, wameitaka serikali kuwa makini na vitendea kazi vinavyoingizwa nchini kwa kuwa vimekuwa vikiwakosesha masoko na ubora wa bidhaa zao, hali ambayo imekuwa ikiwasababishia walio wengi kushindwa kufikia malengo.

Mkurugenzi wa Utawala wa Edodoma Empowerment, Rehema Gawile, alisema moja ya mpango mkakati wake ni kuhakikisha kuwafikia vijana wengi kwa ajili ya mafunzo ya Tehama, pamoja na changamoto waliyonayo ya vitendea kazi vikiwamo vya kompyuta.

Aidha, mkakati mwingine wa taasisi hiyo ni pamoja na mpango wa kuwapeleka watoto yatima shuleni na walio mitaani na kuwapatia makazi ya kudumu.

Alisema pamoja na majukumu hayo Edodoma Empowerment, imebeba dhima ya kuhamasisha wananchi wa kipato cha chini na kuwapa mafunzo ya kibiashara na usimamizi wa fedha teknolojia rahisi ya uzalishaji mali, kukuza mitaji, kutoa elimu ya magonjwa ya zinaa na kupima Ukimwi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Kitambi, akifungua maonyesho hayo alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na wajasiriamali katika kuleta uchumi, hivyo itahakikisha fursa mbalimbali zinawafikia ili kuleta maendeleo.



# Waziri aipa tano wakala wa chakula

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, amesema Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi uko makini na inatambua majukumu yake ikiwamo kusimamia ubora na usalama wa bidhaa kwa lengo la kulinda afya za wananchi.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chakechake, Suleiman Sarahan Said, aliyetaka kujua kama serikali inatambua kwamba kuna wafanyabiashara wanaoendelea kupewa vibali na kuingiza bidhaa ambazo zimepitwa na wakati.

Waziri Hamad alisema mfanyabiashara yeyote aliyepewa kibali akibainika kuingiza bidhaa zisiyokidhi viwango vya ubora na usalama atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alizitaja hatua hizo ni pamoja na kuziteketeza au kuzirudisha zilikotoka bidhaa hizo ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Katika swali lingine aliloulizwa na mwakilishi huyo aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kupitia na kupima ubora wa vyakula vilivyoko madukani, alisema wizara yake inaendelea na utaratibu wake wa kawaida wa kila siku wa kufanya ukaguzi na uchunguzi wa bidhaa mara kwa mara.

"Tumekuwa tukifanya ukaguzi huo katika maeneo mbalimbali ikiwamo bandarini, katika maghala, maduka makubwa na madogo," alisema Hamad.

Aidha, aliwapongeza wananchi kwa kutoa ushirikiano kupitia wakala wa chakula na kuelezea kuwa ushirikiano huo unawapa moyo mwepesi wa kuwatambua wanaofanya ubadhirifu na kutekeleza majukumu yao kwa manufaa ya wananchi.

Hamad alisema serikali imekuwa ikichukua hatua kuhakikisha wananchi wanakula vyakula sahihi na salama ili kulinda afya zao.

Alisema leseni 39 za wafanyabiashara zimefungiwa kutokana na kuingiza na kuuza bidhaa zisizosalama na leseni hizo zimezuiwa hadi pale watakaporekebisha makosa yao.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma (katikati), akibadilishana mawazo na Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais, Yahya Ahmada Abdulwakil (kushoto), nje ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Apigia debe kilimo cha michikichi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MWAKILISHI wa Mgogoni Kisiwani Pemba, Shehe Hamad Mattar, amehoji lini utekelezaji wa Zanzibar kuzalisha mafuta ya mawese kwa wingi utafanyika ili kuhifadhi mazingira na pia kuongeza kupatikana chakula cha nyuki.

Mattar alihoji jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiuliza swali la msingi.

Katika swali hilo, alisema serikali ya Muungano ilishatenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kilimo cha michikichi na kutaka kujua utekelezaji wake utaanza lini Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alisema serikali ya Tanzania imetenga kiasi hicho kwa ajili ya kilimo cha michikichi ili kuzalisha mafuta ya mawese na kuhifadhi mazingira lilipokewa vizuri na serikali ya Zanzibar kwa vile jambo hilo ni la maendeleo.

Alieleza kuwa kwa upande wa Zanzibar katika kuendeleza mazao ya mafuta, imeanzisha mpango wa kuendeleza zao la asili la minazi kwa kutoa miche bila malipo na kuandaa sera na kwamba iko katika hatua za mwisho kutayarisha sheria ya zao la nazi.

"Pia zao la alizeti limeanzishwa kwa upatikanaji wa mafuta ya kupikia," alisema Naibu Waziri huyo katika kikao hicho cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea huko Chukwani nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Aidha, alisema suala la kuanzisha rasmi zao la michikichi Zanzibar linahitaji tathmini ya kina kuona ukubwa wa eneo la ardhi na kuangalia vipaumbele vya mazao yatakayozalishwa.

Dk. Makame alisema hivi sasa kilimo cha michikichi Zanzibar hakipo katika vipaumbele vya mazao ya biashara na badala yake kipaumbele kiko kwa minazi.

Hata hivyo akijibu suali la nyongeza la mwakilishi huyo, aliyetaka kujua wizara inachukua hatu gani kwa wakulima wanaochukua miche ya minazi, Dk. Makame alisema wizara yake inafuatilia kwa karibu watu wanaopewa miche ya minazi na sehemu wanazokwenda kuotesha ili kuhakikisha miche hiyo inapandwa na kutunzwa.

"Wizara yangu inafuatilia kwa makini wakulima wanaochukua miche ya minazi ambayo hutolewa na serikali kupitia wizara yangu, ili kuhakikisha miche hiyo inakua na kuongeza idadi ya minazi," alisema.

# Wadau washirikishwa mabadiliko ya sheria

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Katiba na Sheria imesema Tume ya Kurekebisha Sheria katika kutekeleza jukumu lake la msingi, hufanya mikutano na makundi mbalimbali katika wilaya zote za Zanzibar ili kukusanya maoni juu ya mapendekezo ya wananchi juu ya sheria husika.

Waziri wa wizara hiyo, Khamis Juma Mwalimu, alisema jana kuwa tume hiyo pia imeshakutana na vyama vya wafanyakazi, Jumuiya ya Waajiri Zanzibar na Kamisheni ya Kazi kujadili sheria hizo na maoni na mapendekezo yao yameshazingatiwa katika rasimu za sheria hizo.

Aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Konde, Omar Seif Abeid, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi aliyetaka kujua tume hiyo ina mpango gani wa kukutana na taasisi mbalimbali.

Waziri huyo alieleza tayari tume ilikutana na vyama vya wafanya kazi, jumuiya ya waajiri Zanzibar na kamisheni ya kazi katika vikao sita, vitatu vilifanyika Unguja na vitatu Pemba.

Alisema mwaka wa fedha 2018/2019 tume ilijiwekea lengo la kuzifanyia mapitio sheria tano na hadi Aprili, mwaka huu, sheria nne kati ya hizo zimefanyiwa mapitio na hatua iliyobaki ni kuziwasilisha katika mamlaka husika kwa hatua ya kufuata utaratibu wa kuziwasilisha serikalini.

Mwalimu alizitaja sheria hizo kuwa ni pamoja na sheria ya ajira namba 11 ya mwaka 2005, sheria ya uhusiano kazini ya mwaka 2005, sheria ya kamisheni ya wakfu na mali amana namba mbili ya mwaka 2007 na sheria ya watu wenye ulemavu haki na fursa sawa namba tisa ya mwaka 2006.

Aidha, alisema tume inaendelea kuzishauri taasisi za serikali pale inapobainika kwamba sheria zinazosimamiwa na taasisi hizo zinakinzana na sheria ili tume ichukue hatua za kuzirekebisha kwa kushirikiana na taasisi husika.

"Hatua hii ni muhimu sana kwani huwapa fursa wananchi ya kushiriki katika kutoa mapendekezo na maoni yao juu ya maombi ya kuzingatiwa katika sheria husika," alisema.

**Waziri huyo alieleza tayari tume ilikutana na vyama vya wafanya kazi, jumuiya ya waajiri Zanzibar na kamisheni ya kazi katika vikao sita, vitatu vilifanyika Unguja na vitatu Pemba.**

# Washereheshaji wasaidia hospitali

Na Elizabeth Zaya

CHAMA cha Washereheshaji Tanzania (SAA), kimetoa msaada wa vifaa mbalimbali katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi ikiwamo vifaa tiba, vyakula na fedha taslimu.

Msaada huo ulitolewa katika wodi ya watoto ikiwa ni miongoni mwa shughuli walizozifanya katika kusherehekea miaka 15 tangu kuanzishwa kwa chama hicho.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo juzi, Mwenyekiti wa Chama hicho, Emmanuel Urembo, alisema wamefanya hivyo ukiwa utaratibu ambao wamejiwekea kila mwaka kusaidia makundi yenye uhitaji.

"Chama chetu kina utaratibu kwamba kila mwaka huwa tunatembelea eneo lenye uhitaji na kutoa misaada mbalimbali. Leo katika Hospitali ya Rufani Tumbi, tuliona tuje tutoe na sisi msaada wa vifaa tiba, vyakula na kiasi chochote cha pesa tunachojaliwa kama sadaka kwa Mwenyezi Mungu, tumesaidia padogo, lakini tunaomba na makundi mengine tujenge utaratibu huu," alisema Urembo.

Mbali na Tumbi, pia walitoa msaada wa vyakula na mavazi katika kituo cha kulelea yatima cha Buloma kilichopo Picha ya Ndege katika mkoa huo.

Akizungumza kwa niaba ya hospitali hiyo, Mary Mpongwe, nesi, alisema miongoni mwa changamoto zilizopo katika hospitali hiyo ni kupata wagonjwa ambao wanashindwa kuchangia huduma za matibabu.

"Kama hospitali, huwa tunajitahidi sana kutoa misamaha ya kibinadamu kwa wagonjwa wasio na uwezo, lakini huwa inafika kipindi inazidi uwezo, tuna wagonjwa hapa ambao hawana hata uwezo wa kununua 'pampers' kwa hiyo tukipata misaada kama hii inatusaidia sana,"alisema Mpongwe.

Ofisa Sanaa wa Baraza la Sanaa la Taifa (Basata), Makame Augustino, alitoa wito kwa makundi mengine kujifunza kupitia kikundi hicho ili mbali na kuendesha shughuli zao, lakini pia yajiwekee mipango ya kusaidia jamii.

**"Kama hospitali, huwa tunajitahidi sana kutoa misamaha ya kibinadamu kwa wagonjwa wasio na uwezo, lakini huwa inafika kipindi inazidi uwezo, tuna wagonjwa hapa ambao hawana hata uwezo wa kununua 'pampers' kwa hiyo tukipata misaada kama hii inatusaidia sana,"alisema Mpongwe.**

# Madereva malori walilia kipimo sahihi cha mafuta

Na Romana Mallya

MADEREVA wa malori wameiomba serikali kushughulikia changamoto zinazohusiana na kipimo sahihi cha mafuta wakati wa kuyashusha nje ya nchi badala ya kutumika 'flow mita' fimbo 'stick' iliyotolewa na wakala wa vipimo.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Malori Tanzania (CHAWAMATA), Greyson Wimile, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kuhusu changamoto zinazowakabili madereva wanaosafirisha mafuta nje ya nchi.

Wimile alisema changamoto ya kipimo sahihi cha mafuta walishawasilisha serikalini na kuomba iifanyie kazi kwa wakati ili waondokane na kadhia wanazozipata kwenye nchi nyingine.

"Tunaomba serikali itoe ufafanuzi kuhusu kipimio, hii stick tumepewa na Wakala wa Vipimo, ni aina fulani ya fimbo ambayo gari linaponunuliwa haliruhusiwi kubeba mafuta mpaka liende kwa Wakala wa Vipimo ambayo ni Idara ya Serikali," alisema.

Aliongeza: "Fimbo hii haiwezi kuchakachuliwa, dereva ninapokwenda kupakia mafuta natumia kipimo hiki ambacho serikali imenipatia, nikifika sehemu ya kupakia mafuta nitamwambia mpakiaji aniwekee labda lita 6,000 akishaweka nachukua kipimio changu kuhakikisha," alisema. Alisema kwa upande wa Tanzania fimbo hizo hazina tatizo, ila wanapovuka mipaka wakati wa kushusha mafuta dereva anaonekana ameiba kutokana na kutumika flow mita badala ya fimbo hiyo.

Wakili wa chama hicho, Alloyce Komba, alisema kipimo sahihi kinachotakiwa na serikali ni stick, lakini wamiliki wa malori wanatumia kipimo cha 'flow mita' wakati wa kushusha mzigo ambacho huonyesha upungufu wa mafuta.

"Tulishawasilisha changamoto hii serikalini na imeanza kuifanyia kazi na tunaomba ufumbuzi wa tatizo hili upatikane mapema ili kuondoka mkanganyiko huu," alisema.

Alisema matumizi ya flow mita yamechangia madereva kuonekana magari waliyokabidhiwa kusafirisha mafuta, yanakuwa na upungufu wa ujazo wa mafuta tofauti kikitumika kile cha stick.




Maji ya mvua za masika zinazoendelea kunyesha yamemega udongo wa kibao cha Shule ya Msingi Mbezi, jijini Dar es Salaam, hivyo kutishia kubomoka. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Dk. Bashiru asifu ubunifu wa kuhifadhi Qur'an kwa watoto

Na Mwandishi Wetu

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka Watanzania kutumia uwezo wa kuhifadhi vitabu vitakatifu kuongeza ubunifu katika nyanja ya sayansi na teknolojia ili kuendeleza jamii kwa kuipatia maendeleo stahiki.

Dk. Bashiru alitoa wito huo katika Kata ya Pahi, wilayani Kondoa mkoani Dodoma, wakati wa mashindano ya kuhifadhi Qur'an yaliyowashirikisha wadau kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kuwa kuna umuhimu mkubwa katika kuwekeza kwenye elimu kwa watoto, kwa kuwa wakisoma si tu wanajengewa maarifa, lakini pia wanaunganishwa na hivyo kuwa chachu ya kuweza kusaidia jamii inayowazunguka.

Mratibu na mwandaaji wa mashindano hayo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kondoa, Dk. Ashatu Kijaji, alisema kuwa lengo la mashindano hayo ya kuibua vipaji vya watoto vya kusoma Kitabu Kitukufu cha Qur'an ni kuwajengea vijana uwezo wa kuwa na ujasiri katika kueleza wanayo yaamini yakiwamo mambo mazuri ambayo yanafanywa na serikali.

Kwa upande wake, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alisema kuwa kazi zinazofanywa na Dk. Kijaji, ni zakupigiwa mfano hasa kwa wanawake na kuwataka wazazi katika Wilaya ya Kondoa kumuunga mkono kwa kushiriki kikamilifu katika mikakati ya kuinua elimu katika eneo hilo, kwa kuhakikisha wanawapeleka watoto katika makambi yaliyo na lengo la kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mustapher Shabaan, aliwapongeza vijana walioshiriki mashindano hayo na kuonyesha umahiri mkubwa wa kuhifadhi Qur'an na kuwataka waumini wa Kiislamu kusoma na kukielewa kitabu hicho kitukufu kwa kuwa kimejaa elimu na maarifa mengi yatakayowasaidia kwenda vyema katika jamii na kupata thawabu kutoka kwa Mungu.

## UN kusimamia vita dhidi ya ebola DRC

**GENEVA,** Uswizi

UMOJA wa Mataifa (UN) kuanzia sasa ndiyo utasimamia harakati za kupambana na ugonjwa wa ebola Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ripoti kuhusu idadi ya vifo vinavyotokana na ebola, huko DRC inaeleza kwamba tangu Agosti mwaka 2018 zaidi ya watu 1,200 wameshakufa na wengine kadhaa wameambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

Hatua hiyo ya UN kuombwa kusimamia harakati za kupambana na ugonjwa huo DRC imechukuliwa Geneva, Uswisi kutokana na ongezeko la vifo vya kila mara vya ebola.

Vifo hivyo vimeripotiwa kutokea kila mara eneo la Kivu Kaskazini pamoja na Ituri Mashariki mwa DRC kwenye mji wa Butembo mahali ambako kumeshuhudiwa vifo na maambukizi mengi kwa wakazi wa huko.

UN ndiyo itasimamia harakati za kupambana na ugonjwa huo DRC ili kuhakikisha unatokomezwa kabisa kutokana na hadi sasa umeshawaua watu wengi, huku kukiwa na hatari ya kusambaa katika nchi jirani.

Akizungumza na VOA, mbunge wa Beni, Kizerbo Kasereka alieleza kwamba alipokea kwa furaha taarifa za UN kuingilia kati kusimamia utokomezaji wa ugonjwa wa ebola katika eneo lao. **VOA**

## Trump, Abe watofautiana

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, ameonyesha wazi kutofautiana na Rais wa Marekani, Donald Trump, kuhusu njia mwafaka ya kushughulikia suala la mpango wa nyuklia la Korea Kaskazini.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wao wa pamoja, Rais Trump ameendelea kusisitiza msimamo wake wa kuheshimu urafiki alioanza kuujenga na kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un.

Rais Trump amesema licha ya mazungumzo ya hivi karibuni kugonga mwamba, bado anaamini kuwa Kim Jong Un anayo nafasi ya kufanya jambo sahihi kwa kuachana na mpango wake wa nyuklia.

Kwa upande wake, Abe amesema namna Rais Trump anavyoshughulikia suala la Korea Kaskazini ni hatari kwa usalama wa kikanda.

"Ni lazima kiongozi huyu aonyeshe kuwa yuko makini katika kuhakikisha nchi hiyo haimiliki silaha za maangamizi," Abe amesema.

Waziri mkuu huyo ametolea mfano jaribio la hivi karibuni la Korea Kaskazini na kusema kitendo kilichofanywa na taifa hilo kinakiuka sheria za kimataifa na imani ambayo tayari mataifa yao yalikuwa yameonyesha kwa nchi hiyo.

Haya yanajiri wakati huu Serikali ya Pyongyang ikimkashifu mshauri wa masuala ya usalama wa taifa wa Marekani John Bolton, ambaye imemuita kama "mpenda vita." **RFI**

# Upinzani wagawanyika maandamano Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

CHAMA kikuu cha upinzani nchini Sudan pamoja na baadhi ya viongozi wa waandamanaji wamekataa wito wa kushiriki maandamano ya siku mbili yanayotarajiwa kufanyika kuanzia leo.

Maandamano hayo yana lengo la kushinikiza jeshi kukabidhi madaraka kwa utawala wa kiraia.

Msimamo huu wa upinzani ni ishara za kugawanyika ndani ya vuguvugu la mabadiliko linaloshiriki mazungumzo na baraza la kijeshi.

Mazungumzo kati ya viongozi walioko chini ya mwavuli wa maandamano, The Alliance for Freedom and Change pamoja na majenerali wa jeshi ambao wanaongoza nchi hiyo baada ya kumwondoa madarakani Omar al-Bashir mwezi uliopita, yamekuwa yakisuasua, huku pande zote zikivutana kuhusu nani aongoze serikali ya mpito.

**Tunakataa maandamano yaliyotangazwa na baadhi ya makundi ya upinzani, mgomo wa kitaifa ni silaha ambayo inapaswa kutumika baada ya kukubaliwa na kila upande.**

Katika jitihada zao za kuweka shinikizo kwa baraza la kijeshi, viongozi wa waandamanaji walitisha maandamano ya nchi nzima kuanzia leo, lakini chama cha Umma, ambacho ndio muhimili wa upinzani kimekataa wito wa kuandamana.

Chama cha Umma kilisema: "Tunakataa maandamano yaliyotangazwa na baadhi ya makundi ya upinzani, mgomo wa kitaifa ni silaha ambayo inapaswa kutumika baada ya kukubaliwa na kila upande."

Taarifa hiyo iliongeza: "Tunapaswa kuepuka njia za namna hii ambazo zinaweza kuharibu mambo."

Chama cha Umma ambacho kinaongozwa na Waziri Mkuu wa zamani, Sadiq al-Mahdi, kimesema uamuzi wa kuitisha mgomo wa nchi nzima unapaswa kuchukuliwa na baraza la viongozi wa maandamano.

Baraza la namna hii bado halijaundwa "na litaundwa katika kikao cha wiki hii." imeongeza taarifa ya chama hicho.

Katika mahojiano ya hivi karibuni na shirika la habari la AFP, Mahdi aliwaonya waandamanaji wasiwachokoze wanajeshi wanaotawala, ambao kwa sehemu kubwa alisema walikuwa sehemu ya kumwondoa madarakani Bashir. **RFI**



Kofia zinazovaliwa utosini au kippa huvaliwa na wanaume wa Kiyahudi. Kofia hizo zimepigwa marufuku Ujerumani na kamishna wa kupambana na ubaguzi wa chuki za kijamii nchini humo, amewataka Wayahudi kuepuka kuvaa kofia hizo katika maeneo ya umma. **PICHA: BBC**

## Sababu Wayahudi kukatazwa kofia zao

**BERLIN,** Ujerumani

KAMISHNA wa kupambana na ubaguzi wa chuki za kijamii nchini Ujerumani, Felix Klein, amewataka Wayahudi kuepuka kuvaa kofia za Kiyahudi katika maeneo ya umma.

Klein amewaonya Wayahudi waache kuvaa kofia zao zinazofahamika kama 'kippa' katika baadhi ya maeneo kutokana na kuongezeka kwa chuki dhidi yao nchini Ujerumani.

Kamishna huyo amesema maoni yake juu ya suala la chuki kwa Wayahudi "Yamebadilika ikilinganishwa na yalivyokuwa awali."

Rais wa Israeli Reuven Rivlin amesema wito huo unamaanisha "Kukiri kwamba, kwa mara nyingine tena, Wayahudi hawako salama katika ardhi ya Ujerumani."

Ongezeko kubwa la idadi ya makosa ya chuki dhidi ya Wayahudi liliripotiwa mwaka jana.

Huku takwimu rasmi zikionyesha matukio ya uhalifu wa chuki dhidi ya Wayahudi yakifikia hadi 1,646 katika mwaka 2018, idadi hiyo ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na mwaka 2017.

Mashambulio ya moja kwa moja dhidi ya Wayahudi nchini Ujerumani pia yaliongezeka katika kipindi hicho, huku yale ya kuwapiga Wayahudi yaliyorekodiwa ni 62, ikilinganishwa na mwaka jana ambapo watu 37 ndio waliopigwa mwaka 2017.

Akizungumza na gazeti la Handelsblatt, Waziri wa Sheria wa Ujerumani, Katarina Barley, alisema kuwa kuongezeka kwa uhalifu wa chuki dhidi ya Wayahudi ni "aibu kwa nchi".

"Siwezi kuwashauri Wayahudi kwamba wavae kofia zao zinazofunika utosini kwa wakati wowote na kila mahali nchini Ujerumani," aliliambia gazeti la Funke.

Aidha, aliwatolea wito maofisa wa polisi, walimu na mawakili kupata mafunzo ya kuweka bayana "kile kinachokubalika na ambacho hakikubaliki "Wakati wanapokabiliana na uhalifu dhidi ya Wayahudi".

Kauli zake zimekuja wiki kadhaa baada ya mmoja wa wataalamu wa ngazi ya juu wa masuala ya sheria za ubaguzi dhidi ya Wayahudi kusema kuwa ubaguzi bado upo sana miongoni mwa jamii za Ujerumani.

"Ubaguzi dhidi ya Wayahudi umekuwapo. Lakini ninadhani hivi karibuni, umetajwa sana kuongezeka na wa kiwango kibaya zaidi," Claudia Vanoni aliliambia shirika la habari la AFP. **BBC**

# Samia: Hatutaongeza muda mifuko ya plastiki

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais, Samia Hassan Suluhu, amesisitiza kwamba serikali haitaongeza muda wa matumizi ya mifuko ya plastiki huku akipiga marufuku matumizi ya maji maarufu ya 'Kandoro' yanayohifadhiwa katika mifuko midogo laini kwa sababu haijathibitishwa usalama wake na pia inachafua mazingira.

Makamu wa Rais alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza katika kikao cha viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuhusu utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki.

Alisema zipo picha ambazo zinasambazwa katika mitandao ya kijamii, watu wakilinganisha mifuko ya plastiki na ya karatasi lengo likiwa ni kuishawishi serikali kuongeza muda wa matumizi ya mifuko hiyo.

"Watu wanaoainisha picha za mifuko ya plastiki na ya karatasi, kuna mtu mkono mmoja ameshika mifuko ya plastiki ikiwa mingi na mkono mwingine ameshika mifuko ya karatasi ikiwa michache, picha nyingine zinaonyesha shefu za mifuko mbadala zikiwa tupu na mingine ni mingi, haya yote ni kuishawishi serikali iongeze muda wa matumizi ya mifuko hiyo," alisema Samia Suluhu na kuongeza:

"Nataka kuwaambia ndugu zangu kwamba hatutaongeza muda, ifikapo Juni Mosi hakuna mfuko wa plastiki kuonekana na katika hili hakuna kubembelezana, tumeshasema sana tangu mwaka 1991, naomba sasa tutekeleze na Dar es Salaam ndiyo kigezo, tukifanya vizuri hapa mikoa yote itafanya vizuri kwa sababu huu mkoa ndiyo msambazaji mkubwa wa mifuko hii ya plastiki, na Dar es Salaam ndiyo Tanzania yenyewe."

"Kwa bahati nzuri mimi hili ni zoezi la pili, Zanzibar inayosifiwa leo kuwa haina mifuko, ilipigwa marufuku nikiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Uwekezaji na Utalii pale, lakini waliofanikisha ni serikali za mitaa, wakuu wa wilaya na viongozi wengine, walisimamia kuzuia mifuko hiyo, sasa tukifanya hivyo nchio nzima tutafanikiwa na linaweza kuchukua muda mfupi tu na hili suala ni la kila mtu."

Pia Makamu wa Rais aliliagiza Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuharakisha utoaji wa vibali kwa viwanda vya uzalishaji wa mifuko hiyo mbadala ili waanze uwekezaji haraka.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, January Makamba, alisema Tanzania ikifanikiwa kutekeleza katazo la matumizi ya mifuko hiyo itakuwa imeingia katika orodha ya nchi 60 ambazo zimepiga marufuku ya matumizi ya mifuko hiyo ya plastiki kati ya nchi 127 zilizopo katika makubaliano ya kimataifa ya kuondosha matumizi ya mifuko hiyo. Alisema mpaka sasa tayari kuna kampuni 70 ambazo ziko tayari kwa ajili ya utengenezaji wa mifuko hiyo mbadala.

Pia makamba alisema katazo hilo haligusi mifuko ambayo inatumika kufungia bidhaa.

"Kinachokatazwa ni mifuko ya plastiki tu, vifungashio vingine vya mikate, maziwa, sukari, mifuko inayotumika katika ujenzi, huduma za afya. Tumeanza na hii ya kubebea, lakini tutaendelea hatua kwa hatua," alisema Makamba.



Rais wa GSM Group, Ghalib Mohamed (kushoto), pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko wa kampuni hizo, Allan Chonjo (katikati), wakimsikiliza Wema Sina mmoja wa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ambaye alijishindia seti ya meza baada ya kutembelea duka la Danube, wakati wa uzinduzi wa duka jipya la MAX lililopo Mlimani City, jijini humo jana. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Askofu wa Tanzanite azikwa

INATOKA UK 4

ma.

Naye Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya Meru, Shaban Mdoe, alisema kwa muda aliyokuwa kiongozi katika kata yake alihakikisha anapigania maslahi ya wananchi wake.

"Mollel alihakikisha anawapigania maslahi ya wananchi wake wapate huduma za kijamii kama vile maji, ujenzi wa barabara, ujenzi wa shule na vituo vya afya katika kata yake," alisema Mdoe.

Akizungumza kwa niaba ya wachimbaji wa madini ya Tanzanite, Hamis Ramadhani, alisema, Mollel alikuwa kiongozi na mzee wakuigwa katika jamii yake.

"Kata yetu imepata pigo kubwa kwa kumpoteza mtu muhimu, kwani alikuwa akimsikiliza kila mtu bila ya kumbagua mtu kwa rangi yake, dini na kabila lake," alisema Ramadhani. Alisema daima watamkumbuka kwa matendo mema aliyofanya katika familia na jamii inayomzunguka.

Akitoa salamu za rambirambi, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji wadogo wa madini Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Justine Nyari, alisema sekta ya madini imempoteza mtu muhimu ambaye alitoa mchango wake kuyatangaza madini ya Tanzanite nje ya nchu hususani katika soko la madini la dunia.

"Marehemu alikuwa na moyo wa unyenyekevu na wakujitolea, pia alitoa mchango mkubwa katika kuyatangaza madini yetu nje ya nchi," alisema Nyari.

Wawakilishi wa waandishi wa habari, Novatua Makunga, alisema Mollel alikuwa mpambanaji mzuri na alishawahi kufanya naye kazi.

Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, aliwaomba wananchi waungane kuleta maendeleo katika jimbo hilo na waache itikadi za vyama.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema Mkoa wa Arusha umepata pigo, kupoteza Askofu aliyefanya masuala mbalimbali ya kusaidia na kugusa jamii.

***Imeandikwa na Allan Isack na Cynthia Mwilolezi (Arusha)***

# Mabilioni yalivyonaswa utoroshwaji wa madini

INATOKA UK 4

11.7.

"Madini yaliyokamatwa katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Mwanza na Dar es Salaam yalitaifishwa na serikali. Madini yaliyokamatwa mikoa ya Arusha, Morogoro na Geita yapo katika hatua mbalimbali ya uchunguzi," alisema.

"Mpaka Machi mwaka huu, madini yaliyotaifishwa yalikuwa na thamani ya Dola milioni 13.5 na Sh. milioni 6.3."

Alisema ulinzi umeimarishwa katika maeneo yote ya uzalishaji kwenye migodi mikubwa na ya kati kwa kuwaweka Maofisa Madini Wakaazi (MRO).

Alibainisha kuwa lengo la kuweka maofisa hao ni kusimamia na kuwasilisha taarifa za uzalishaji wa kila siku pamoja na kudhibiti mianya ya utoroshwaji madini.

Waziri huyo alisema katika maeneo ya viwanja vya ndege na mipakani, wamewekwa wasimamizi kuhakikisha madini yanayopitishwa, yana vibali husika.

"Nitoe wito kwa Watanzania kufanya shughuli za madini kwa kuzingatia sheria za nchi ikiwamo Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017 pamoja na kanuni zake," alisema.

Waziri Biteko pia alibainisha kuibuka kwa matukio ya baadhi ya watumishi wasio waaminifu kushirikiana na wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wasiowaaminifu kuiibia serikali mapato kupitia kuwasilisha taarifa zisizo sahihi za uzalishaji madini.

"Katika kuhakikisha tunakomesha tabia hii isiyo ya kizalendo inayopelekea serikali kupoteza mapato, serikali imeendelea kuchukua hatua kali za kinidhamu ikiwamo kuwasimamisha kazi ili kupisha uchunguzi na kuwafikisha mahakamani waliobainika kuwa na makosa," alisema.

Akizungumzia migodi ya Mirerani, Biteko alisema baada ya kujengwa ukuta kuzunguka eneo hilo, udhibiti wa madini ya tanzanite umeimarika na hivyo kuongeza ukusanyaji maduhuli yatokanayo na madini hayo.

Alisema wachimbaji wadogo wameitika wito wa kulipa kodi ambapo sasa wanalipa kodi kuliko kipindi chochote kwenye historia ya uchimbaji kwenye eneo hilo.

"Wachimbaji wadogo Mirerani walikuwa wanachangia kwa asilimia sita hadi 10 ya mapato yote, kiasi kikubwa kilikuwa kikichangiwa na Mgodi wa TanzaniteOne.

"Mwaka 2017, Sh. bilioni moja zilikusanywa. Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 930 zilikusanywa kutoka mgodi huo kama mrabaha wa ada ya ukaguzi ikiwa ni sawa na asilimia 85 ya mapato yatokanayo na uzalishaji wa Tanzanite na Sh. milioni 164.1, sawa na asilimia 15 zilikusanywa kutoka kwa wachimbaji.

"Mwaka 2018, wachimbaji wadogo pekee wamechangia Sh. bilioni 1.4 na uzalishaji umeongezeka kutoka kilo 147.7 hadi kilo 781.204," Biteko alibainisha.

Ili kutekeleza majukumu ya wizara hiyo, Biteko aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 49.4 kwa ajili ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.

### NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI,** Tunahitaji Fundi wa COMPUTER na CCTV CAMERA Awe na Uzoefu wa mwaka mmoja Awe na Diploma. Mawasiliano: 0713 164462/ 2110836


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311



### KUPOTEA KWA CHETI



**Hassan B. Hassan** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1741/0429** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Chamazi. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **SRB/RB/4625/018**

115250102


### KUPOTEA KWA CHETI



**Samli S. Shaibu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S. 0831-0141** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika shule ya Sekondari Nangwanda. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **ILE/RB/455/2019**

115249302


### TAMASHA



Mwandaaji Robert Sakaya wa Platinum Promotions anawaalika watanzania wote kwa nyazifa zao zmabalozi wan chi za Arab, China, Uingereza, Marekani na Ulaya katika Tamasha la Music na Vijana, Uhamasishaji na burudani litakalofanyika mwishoni mwa mwezi Juni, Mwisho wa kutoa michango ya Tamasha hilo ni 22th Juni kiingilio shilingu 25000 na 50000 kwa VIP.

215249002


### KUPOTELEWA NA HATI YA MUDA MFUPI YA KIWANJA



**MARWA MBUSIRO MKALE** wa Butimba MWANZA anatangaza kupotelewa na Hati ya Muda mfupi ya Kiwanja. Namba ya hati ya Kiwanja ni namba 11 Block C.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MW/RB/4409/2019**

215249502

### KUPOTEA KWA PASSPORT



**Gasto Lemunge** anatangaza kupotelewa na Passport au Hati ya kusafiria yenye namba **AB 777509** iliyotolewa na ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2015. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MLA/IR/1437/17**

115250102

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Claude Luicerodrigoes** anatangaza kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T742 CKF** aina ya **TOYOTA RAV4,** Yenye chasis namba **35FE07052.** Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Polisi Taarifa: **KMR/RB/7172/2019**

115248902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo KIBAKWE**

**Usimamizi wa mirathi 2/2019**

**Ombi la GEORGE RASHID GAILANGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu PASCHAL RASHID GAILANGA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 12/6/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huy upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 21/5/2019

215249402

### JAM COMPANY LTD

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Sifa Saccos Iringa tutauza nyumba ya Patrick Komba na mkewe Christina Daniel nyumba ipo eneo la Kihesa Mwang'ingo Mlimani. Mnada tarehe 30/5/2019 saa 4:00 asubuhi.

Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku hiyo ya mnada na salio la 75% lilipwe ndani ya siku 14 tokea siku ya mnada.

Mnunuzi akishindwa kulipa salio ndani ya mda huo wa siku 14 atakuwa amepoteza pesa aliyolipa na nyumba itauzwa tena.

Gharama za kubadilisha jina ni za mnunuzi.

**Wasiliana nasi kwa:**
**0754 558799/0764 782526**

115249602

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
27/05/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe **29/05/2019** Kampuni ya **Musa holding** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Holili **Rombo- Moshi -Boma ng'ombe –Hai** gari lenye namba za usajili **T277ALQ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   **Urefu** - **9.7**
   **Upana** - **3.0**
   **Kimo** - **3.0**
3. NJia itakayotumika ni Holili Rombo Moshi mpaka Bomang'ombe - Hai

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215249702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**VINCENT WILLIAM PAZZIA** anatangazakupotelewanakad iyagariainayaSUZUKI CARRYyenyenambazausajili **T 541 DBY .** Chassis namba **DA52T105396.** Engine namba. **F6AEAA5396.** Yeyoteatakayeionaatoetaarifa kituo cha polisi.Taarifayapolisi: **DOM/TR/RB/ 898/2019**

215249802

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**LAND APPEAL NO. 7 OF 2015**
***(C/F Arusha District Land and Housing Tribunal, Application No. 2/2011)***

**JOSEPHINE EMMANUEL MLAY**
**W/O EMMANUEL ELIFATAO MLAI ...............APPELLANT**

**VERSUS**

1. **EMANUEL ELIFATAO MLAI**
2. **OMARY FRANK MSHANA**
3. **GLADY FRANK MSHANA.................RESPONDENTS**
4. **ANNE FRANK MSANA**
5. **M/S MAJEMBE AUCTION MARTH LTD.**

**NOTICE FOR HEARING**

1. **TO : OMARY FRANK MSHANA**
   **ARUSHA.**

**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for Hearing in the High Court of Tanzania at Arusha on the 28th day of May, 2019 at 08:3 day of May, 2019, at 08:30 a.m . o'clock in the forenoon.

YOU may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT:** In default of your appearance on that day and time before hearing the court may proceed in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and the **SEAL** of the COURT this 13th day of May, 2019.

DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

215249202

**Katika mahakama ya mwanzo mjini Tanga usimamizi wa mirathi namba 72/2019**
**Ombi la Ally Amri Bakari kuteuliwa**

**Msimamizi wa mirathi ya marehemu Amiri Juma Bakari**
**Kwa yoyote anaye husika**

Watu wote wanaodaiwa kuwa wana uhusiano wowote na mirathi marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 05/06/ 2019 kabla huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/05/2019


***KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO***

***Tupigie 0767 223311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MILNER: MESSI KANIITA PUNDA




**LONDON,** England

KIUNGO wa Liverpool, James Milner, amesema mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi alimwita punda wakati wa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo walipoteza kwa kufungwa 3-0.

Milner ameliambia Gazeti la Daily Mail kuwa Messi alimwambia maneno mengi ya Kihispaniola na yeye anaifahamu vizuri lugha hiyo.

"Aliniita 'burro', ambayo ukitafsiri inakuwa punda, lakini nadhani pia hutumiwa katika soka la Hispania kama neno la kawaida kwa mtu anayempiga mateke.

"Nilimuuliza ikiwa ni sawa, lakini hakuwa na hilo. Sidhani yeye alitambua nilielewa Kihispania chake. Alisema: "Uovu huo ulifanya, kwa sababu nimekutaja."

Milner alikiri kwamba ujuzi wa Messi ulitolewa, njia hiyo ya kimwili inahitajika ili kumsaidia kumtoa mchezo wake.

Hata hivyo, kiungo huyo pia alibainisha kuwa nia yake hakuwahi kutaka kumdhuru Messi.

"Mambo aliyoyafanya katika mchezo huo, ambayo amefanya kazi yake yote, inafanya kuwa mgumu kucheza dhidi yake," Milner aliongeza. "Ikiwa unajaribu kumzuia, huwezi kuwa na hofu ya kufanywa kuwa wajinga. Nimefanya hivyo.

"Nilikuwa nikichuana naye mara nyingi, sitakuwa wa kwanza na mimi sitakuwa wa mwisho kusema kwamba yeye ni mchezaji wa ajabu.

# Mwenyekiti City adai wanaonewa wivu

**LONDON,** England

MWENYEKITI wa KLabu ya Manchester City, Khaldoon Al Mubarak, amesema baadhi ya wapinzani wao wa Ligi Kuu England wana wivu juu ya mafanikio ya klabu hiyo.

City imekuwa klabu ya kwanza kushinda makombe matatu ya ligi za ndani ya Uingereza baada ya kuifunga Watford 6-0 kwenye fainali ya Kombe la FA.

Mafanikio hayo yamekosolewa na baadhi ya wachambuzi wakisema kocha wa City, Pep Guardiola ametumia kitita kikubwa cha fedha kwenye usajili.

Hata hivyo, kwenye tathmini yake ya mwisho wa msimu, Mubarak ameviambia vyombo vya habari vya klabu hiyo kuwa hatakubali klabu yake "kutumika katika njama za kuhalalisha maamuzi ya kutowekeza vema kwenye mpira."

Mabingwa hao wa Ligi Kuu hawana hata mchezaji mmoja kwenye orodha ya wachezaji ghali 10 wa ligi hiyo.

Wapinzania wao wakuu wana wachezaji wawili Paul Pogba (aliyesainiwa kwa pauni milioni 89) na Romelo Lukaku (aliyesainiwa kwa dau la awali la pauni milioni 75), Liverpool ina mchezaji mmoja kwenye orodha hiyo, Virgil van Dijik, aliyesainiwa kwa pauni milioni 75.

Mchezaji ghali zaidi kusainiwa na City ni Riyad Mahrez, waliyemng'oa Leicester City kwa pauni milioni 60 Julai mwaka jana.

Wachezaji wengine ghali wa City ni Aymeric Laporte (pauni milioni 57), Kevin de Bruyne (pauni milioni 55) na Benjamin Mendy (pauni milioni 52).



Riyad Mahrez ndiye mchezaji ghali zaidi kuwahi kusainiwa na City kwa kitita cha pauni milioni 60.

Kukosolewa kwa City kunakuja wakati huu ambapo inachunguzwa na chombo cha fedha cha Uefa kwa tuhuma za kufanya matumizi mabaya kwenye usajili. City inakanusha vikali tuhuma hizo.

Mubarak amekasirishwa zaidi na matamshi ya Rais wa Ligi ya Hispania, La Liga, Javeir Tebas ambaye hivi karibuni ammeziita Klabu za City na PSG kama 'wanasesere' wa nchi fulani na kuzitaka zitimuliwe kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana na namna wanavyomwaga fedha kwenye usajili.

City, inamilikiwa na Kampuni ya Abu Dhabi United Group kutoka Falme za Kiarabu, huku PSG ikimilikiwa na Kampuni ya Qatar Sports Investments.

"Naamini hili ni jambo baya kuziunganisha timu na kuzikosoa kulingana na rangi na asili ya wamiliki wake," alisema Mubarak.

City wanaamini matamshi ya Tebas hayajazingatia kipindi ambacho Real Madrid walitumia mamilioni ya pauni kuwasajili nyota katika zama zao maarufu kama 'galactico'.

Wachezaji waliosajiliwa kipindi hicho na Madrid kwa madau ya kushtusha ni pamoja na Luis Figo, Zinedine Zidane, Ronaldo na David Beckham kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2000.

Kiwango cha Man United kinaendelea kusuasua licha ya kuwa na mchezaji ghali zaidi wa EPL, Paul Pogba.

Mei 14, City walisema kuwa wanasikitishwa na habari iliyochapishwa na Gazeti la New York Times na kudai kuwa maofisa wa Uefa wanataka klabu hiyo ifungiwe kushiriki mashindano yanayoandaliwa na chombo hicho.

City inadai kuwa na hofu juu ya uwapo wa watu ambao kwa maslahi yao ya kibiashara wanataka timu hiyo ifungiwe na Uefa.

Mubarak amesema kuwa Man City itasafishwa punde tu uchunguzi huo utakapokamilika kwa hoja zilizo wazi.

"Endapo suala hilo halitafanyika kwa misingi ya hoja, basi kwa hakika tutakuwa na maongezi ya namna nyingine kabisa."

## Newcastle United sasa kuuzwa kwa Waarabu

**MANCHESTER,** England

MMILIKI wa Klabu ya Newcastle United, Mike Ashley ameripotiwa kufikia makubaliano ya kuiuza timu hiyo kwa binamu mmiliki wa Manchester City, Sheikh Mansour kwa dau la pauni milioni 350.

Gazeti la The Sun limeripoti kuwa mmiliki huyo mpya anayetarajiwa kuichukua klabu hiyo ya St James' Park anajulikana kwa jina la Sheikh Khaled bin Zayed Al Nehayan.

Sheikh Khaled mwenye umri wa miaka 61, ni miongoni mwa wanafamilia ya Kifalme kutoka Abu Dhabi ambapo mwaka uliyopita alishindwa kuinunua Liverpool baada ya kutakiwa kutoa dau la pauni bilioni mbili.

Mara kadhaa amekuwa akisema kuwa yeye ni shabiki mkubwa wa mchezo wa soka hasa Ligi Kuu England, huku akionekana kutaka kuingia katika orodha ya matajiri wakubwa wanaomiliki Klabu za Uingereza.

Taarifa zinaeleza kuwa tayari mkataba baina ya Ashley na Sheikh umeshasainiwa kwa ajili ya kuichukua klabu hiyo kwa pauni milioni 350 na tayari umeshafikishwa kwa wanaohusika na Ligi Kuu.



# Spalletti: Sijui kama nitaondoka Inter Milan

**MILAN,** Italia

LUCIANO Spalletti hajui kama ataondoka Inter Milan, ingawa taarifa zinaeleza kwamba klabu hiyo ina mipango ya kumchukua Antonio Conte kuwa kocha wao.

Spalletti amefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya pili mfululizo baada ya Jumapili kushinda mabao 2-1 dhidi ya Empoli, lakini majaliwa yake bado hayajulikani.

Kwa mujibu wa uvumi ulioenea ni kwamba kocha wa zamani wa Juventus na Chelsea, Conte ndiye anayetajwa kwenda kurithi mikoba ya Spalletti pale Milan msimu ujao.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Spalletti aliwaambia waandishi wa habari: "Sikushangazwa, tulikuwa na mchezo mzuri.

"Mchezo ulikuwa na presha kubwa na kwa hakika tulicheza vizuri. Uwanja huu unatumika kwa ushindani na kila kitu kilikwenda sawa, lakini tulijikuta kwenye wakati mgumu.

"Bahati mbaya kwa Empoli, nina marafiki pale. Walistahili kubakia juu, lakini sisi tulistahili kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Wakati maamuzi yanapofanyika, kila mmoja anahusika, lakini kwa sasa jambo la msingi ni kwamba tumefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao."






# SANE KURITHI VIATU VYA ROBBEN, RIBERY BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amesema Leroy Sane atakuwa mrithi wa Arjen Robben na Franck Ribery kama akiamua kuondoka Manchester City na kutua kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Sane ambaye mkataba wake wa sasa na City unamalizika mwaka 2021, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Bayern baada ya kushinda mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu ya England akiwa na Manchester.

Huku Bayern ikiwa imewapoteza Robben na Ribery ambao wanaondoka hapo kwenye dimba la Allianz Arena, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani amekuwa akitajwa kutua kwa miamba hao.

Na Rummenigge alizungumzia uhamisho wa Sane, ambaye aliondoka katika klabu yake ya utotoni ya Schalke kwenda City mwaka 2016.

"Huwezi kusahau kwamba bado ana miaka miwili katika mkataba wake na Manchester City, hawawezi kuwauza wachezaji wao kwa sababu wanawahitaji pia," alisema Rummenigge.

"Hii itakuwa ngumu. Lakini nafikiri kwamba mchezaji mwenyewe anahitaji kushawishiwa pia ili aweze kutua hapa Bayern.

"Atakuwa mrithi wa Arjen Robben na Franck Ribery kwa staili ya kufurahisha zaidi. Kama mchezaji atakuwa yupo huru kucheza hapa na kuwa na mafanikio makubwa."

# De Ligt aziweka kiporo Barca, Man U

**AMSTERDAM,** Uholanzi

BEKI Matthijs de Ligt amesisitiza kwamba bado hajaamua hatima yake wakati uvumi ukienea kwamba Barcelona na Manchester United zinapigana vikumbo kuwania saini yake.

Beki huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 19, ni mmoja wa wachezaji wanaowaniwa zaidi Ulaya na sasa anatarajiwa kuondoka hapo Ajax.

Kwa wiki kadhaa klabu za Barcelona na Man United zimetajwa kwamba zinawania saini yake na Barca inapewa nafasi kubwa zaidi ya kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

"Wapi ninapojiona mwenyewe? Ndio Ligi Kuu ya England ina ushindani mkubwa, lakini pia na Hispania," alisema De Ligt akiwaambia waandishi wa habari akiwa kwenye kambi ya timu ya Taifa ya Uholanzi.

"Lakini tuna mashindano mengine, ni suala la wote wawili na wapi nitaweza kuelekea.

"Sijui chochote kuhusu majaliwa yangu ya baadaye, hivyo nitaona namna gani mambo yatakavyotokea. Kwanza tunatakiwa kucheza mechi mbili halafu baada ya hapo tutaona nini kitatokea."

De Ligt kwa sasa yupo na kikosi cha timu ya Taifa ya Uholanzi kinachojiandaa na mchezo wa Kombe la Ligi ya Uefa ambapo kitacheza na England Juni 6, kabla ya kuwavaa Uswisi na Ureno.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL: SINA UHAKIKA KWA NEYMAR, MBAPPE KUBAKI

●●● Nia yangu ipo wazi, siwezi kuahidi kwa sababu itakuwa kukosa busara, ninataka wachezaji wote kubaki ila...

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR na Kylian Mbappe wanaweza kuondoka Paris Saint-Germain baada ya Kocha Mkuu, Thomas Tuchel, kusema hawezi kujihakikishia kuendelea kubaki kwa wawili hao kwa mabingwa hao wa Ligue 1.

Wakati mustakabali wa Tuchel ukiwa salama kufuatia kusaini mkataba mpya, nyota wa zamani wa Barcelona, Neymar ameendelea kuhusishwa na kurudi La Liga, huku kinara wa ufungaji Mbappe akigusia anaweza kujaribiwa na "mradi mpya".

Tuchel aliulizwa kuhusu Neymar na Mbappe juzi Jumapili na kocha huyo Mjerumani aliiambia Sky Sports: "Ninatumika kwa hili. Sasa ni Mei, mambo ambayo ninasema sasa yanaweza yasiwe kweli mwezi ujao.

**"Mambo ni kama yalivyo, kuna uvumi mwingi ambao unamaanisha kwamba tuna ubora na vipaji.**

"Nia yangu kama meneja na kama kocha ni wazi, ninataka wachezaji wangu wote kubaki hapa PSG na kubaki na mradi wetu. Kazi bado haijamalizika, ndiyo kwanza imeanza.

"Nia yangu ipo wazi, lakini siwezi kuahidi kwa sababu itakuwa ni kukosa busara na sitaki kukosa busara katika biashara hii."

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia, Mbappe alifunga mabao 33 Ligue 1 wakati PSG ikitetea ubingwa wake, huku katika mashindano yote msimu huu akicheka na nyavu mara 39.

Aidha, kwa Neymar alitupia mabao 15 Ligue 1 na katika mashindano yote akicheka na nyavu mara 23 kwa PSG ambayo ilitolewa katika hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Manchester United.

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE SASA KUUZWA

MMILIKI wa Newcastle United, Mike Ashley, amekubali kuiuza klabu hiyo kwa pauni milioni 350 kwa binamu wa mmiliki wa Manchester City, Sheikh Mansour. ***(Sun)***

### AZISUBIRISHA UNITED, BARCA

WAKATI Barcelona ikimuwinda Matthijs de Ligt, 19, beki huyo atafanya uamuzi wa mustakabali wake wa baadaye baada ya kuitumikia Uholanzi katika michuano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya - na beki huyo wa Ajax amesema anaipenda Premier League. ***(ESPN)***

### KANE FITI KUIVAA LIVER UEFA

STRAIKA wa Spurs, Harry Kane anatarajiwa kukwea pipa na wachezaji wenzake kwenda Madrid tayari kwa mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumamosi dhidi ya Liverpool. ***(Mail)***

### KANTE KUIKOSA ARSENAL

KIUNGO wa Chelsea, Mfaransa N'Golo Kante, 28, anaweza kuikosa mechi ya fainali ya Europa League dhidi ya Arsenal kesho Jumatano kufuatia kusumbuliwa na majeraha ya goti wakati wa mazoezi. ***(Guardian)***

### MILNER AJADILIWA PSG

PSG imejadili uwezekano wa kwenda kumsajili kiungo wa Liverpool, James Milner, 33, ambaye mkataba wake na 'Wekundu' hao unamalizika mwaka ujao. ***(Le Parisien, via Metro)***

### TIELEMANS AIVUTIA MAN CITY

MANCHESTER City imeingia katika mbio za kumsajili kiungo wa Monaco, Youri Tielemans, 22, ambaye anathaminishwa na pauni milioni 40. ***(Sun)***

### BOATENG RUKSA KUONDOKA

RAIS wa Bayern Munich, Uli Hoeness, amemwambia beki wa zamani wa Ujerumani na Manchester City, Jerome Boateng, 30, kwamba anaweza kuondoka kwa mabingwa hao wa Bundesliga. ***(Bild - in German)***

### ZIDANE KUZUIA RAMOS KUSEPA

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anataka kumbakisha kwenye La Liga beki wa Hispania, Sergio Ramos, licha ya kuwapo na kuvutiwa kutoka kwa Liverpool, Manchester United na timu kutoka China. ***(Marca - in Spanish)***

### CANCELO LULU UNITED, CITY

Manchester City na Manchester United zitashindana katika mbio za kuiwania saini ya beki wa Ureno, Joao Cancelo kama kocha mpya wa Juventus ataamua kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ataondoka kwa mabingwa hao wa Serie A. ***(Tuttosport, via Mirror)***

### YATAJIWA DAU LA CLARKE

Tottenham imeambiwa itapaswa kulipa pauni milioni 20 kwa Leeds United ili kumpata kiungo Muingereza Jack Clarke, 18. ***(Mirror)***

### ROJO AHAKIKISHIWA ULAJI UTD

BEKI Muargentina Marcos Rojo, 29, amesema amekuwa akihakikishiwa kuwa mustakabali wake wa baadaye bado upo Manchester United. ***(Express)***

## HABARI MICHEZO



## Kabwili akaribia kutimkia Sudan

**Na Mwandishi Wetu**

KIPA wa Yanga, Ramadhan Kabwili amepata dili na klabu moja ya Sudan na tayari wamefikia mahali pazuri katika mazungumzo na uongozi wa timu ya hivyo, imefahamika.

Kabwili alimwambia mwandishi wetu kuwa mkataba wake na Yanga unakamilika Mei 30, mwaka huu na kwamba mbali na ofa hiyo ya Sudan bado anatazama kwingineko.

"Mkataba wangu na Yanga unamalizika mwezi huu, hivyo nina ofa ambazo zipo mkononi tunaendelea kufanya mazungumzo kabla ya kusaini na kuna ni timu moja ya Sudan ambayo tumefika sehemu nzuri," alisema na kuongeza:

"Mazungumzo yakikamilika kila kitu nitaweka wazi ikiwa ni pamoja na timu yenyewe, ila bado sijaikatia tamaa timu yangu ya Yanga kwa kuwa ni sehemu yangu ya kazi na wamenilea pia lazima nitoe kipaumbele kwao."

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 37 | 29 | 5 | 3 | 77 | 15 | 92 |
| 2. Yanga | 37 | 27 | 5 | 5 | 56 | 25 | 86 |
| 3. Azam | 37 | 20 | 12 | 5 | 52 | 21 | 72 |
| 4. Kinondoni MC | 37 | 12 | 16 | 9 | 38 | 25 | 52 |
| 5. Mtibwa Sugar | 37 | 14 | 7 | 16 | 36 | 34 | 49 |
| 6. Lipuli | 37 | 12 | 13 | 12 | 31 | 37 | 49 |
| 7. Ndanda | 37 | 12 | 12 | 13 | 24 | 34 | 48 |
| 8. Mbeya City | 37 | 13 | 8 | 16 | 38 | 39 | 47 |
| 9. Alliance | 37 | 12 | 11 | 14 | 33 | 41 | 47 |
| 10. Coastal Union | 37 | 11 | 14 | 12 | 32 | 42 | 47 |
| 11. Singida United | 37 | 11 | 12 | 14 | 30 | 39 | 45 |
| 12. Biashara United | 37 | 11 | 11 | 15 | 30 | 35 | 44 |
| 13. JKT Tanzania | 37 | 10 | 14 | 13 | 26 | 34 | 44 |
| 14. Stand United | 37 | 12 | 8 | 17 | 38 | 48 | 44 |
| 15. Mbao | 37 | 11 | 11 | 15 | 26 | 40 | 44 |
| 16. TZ Prisons | 37 | 10 | 13 | 14 | 27 | 30 | 43 |
| 17. Kagera Sugar | 37 | 10 | 13 | 14 | 32 | 42 | 43 |
| 18. Ruvu Shooting | 37 | 10 | 12 | 15 | 34 | 43 | 42 |
| 19. Mwadui | 37 | 11 | 8 | 18 | 44 | 51 | 41 |
| 20. African Lyon | 37 | 4 | 11 | 22 | 23 | 52 | 23 |

# SAMATTA AMULIKWA KILA KONA LIGI KUU ENGLAND

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kung'ara kwa kuipa timu yake ya KRC Genk ubingwa wa Ligi Daraja la Kwanza A nchini Ubelgiji, mshambuliaji wa Kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, nyota yake sasa inang'ara vilivyo Klabu za Ligi Kuu England (EPL), imeelezwa.

**Tayari Samatta, ameweka wazi kwamba kuna klabu nyingi za EPL zimeonyesha nia ya kuipata huduma yake kwa msimu ujao.**

Alisema: "Siwezi kuzitaja kwa sasa, ila si England tu bali kuna klabu nyingine mbili kutoka Hispania ambazo zimekuwa zikinihitaji, lakini ndoto zangu ni kucheza katika Ligi Kuu ya England.

"Katika soka huwezi kujua nini kitatokea, naweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu, kuna klabu ambayo imekuwa ikiwasiliana sana na wakala wangu."

Hii si mara ya kwanza kuwapo kwa tetesi za Samatta kutakiwa EPL, kwa kuwa wakati wa usajili wa dirisha dogo, Januari mwaka huu, Klabu ya Cardiff ambayo sasa imeshuka daraja, ilidaiwa kutoa ofa kwa KRC Genk kabla ya mchakato huo kukubwa kukamilika.

Ingawa Samatta, 26, hakuwa tayari kutaja klabu zinazohitaji saini yake, tetesi zinaeleza kuwa Everton, West Ham na Burnley ni miongoni mwa zinazohusishwa na huduma yake.

Akiwa na mabao 23 kwenye ligi hiyo msimu huu na tisa katika michuano ya Europa League, Samatta alikuwa lulu kwa mashabiki wa timu hiyo wakati wakihitimisha msimu na kukabidhiwa ubingwa wao msimu huu.

"Genk haijacheza Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 2011 enzi za kina (Kevin) De Bruyne, najua wanataka niichezee msimu ujao ila Ligi Kuu ya England ina heshima yake, ni ligi ambayo tayari imepiga hatua kubwa sana ukilinganisha na Ligi Kuu ya Ubelgiji. Ni ligi ambayo inapendwa na watu wengi duniani, ligi inayoonekana sehemu kubwa duniani, ipo mbali vitu vingi."



Neymar akiwa mazoezini na wachezaji wenzake wa Brazil juzi, kujiandaa na mechi ya kuwania kufuzu Copa America dhidi ya Bolivia Juni 15, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# *Jabir aenguliwa kugombea urais ZFF*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imemuengua mgombea urais wa shirikisho hilo, Suleiman Mahmoud Jabir, katika orodha ya wagombea wa nafasi hiyo kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Juni 2, mwaka huu, imeelezwa.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Juma Msafiri alisema mgombea huyo ameenguliwa baada ya kubainika kukiuka taratibu za uchaguzi na kukosa maadili.

Alisema katika nafasi ya urais ilikuwa na wagombea wanne, hivyo kuondolewa kwake kutafanya kubaki wagombea watatu ambao ni Khamis Abdalla Said, Seif Pandu na Ame Abdallah.

Msafiri alisema kamati hiyo ina jukumu la kufuatilia wagombea ili kuhakikisha wanapata kiongozi ambaye ataweza kuleta mabadiliko katika soka la Zanzibar.

Alisema baada ya kufuatilia wagombea hao, kamati ilibaini na kujiridhisha kuwa mgombea huyo alianza kufanya kampeni za kimakundi na kukosa maadili.

"Kama tunavyojua hali halisi ya mpira wetu tunahitaji mabadiliko na kunako mabadiliko lazima kuwapo na maumivu," alisema.

Alifafanua kuwa mgombea huyo ana vigezo vinavyomruhusu kugombea na na ni mzuri, lakini kuna mambo mengine ya kimaadili ambayo ndiyo yamemwondoa ingawa hakuwa tayari kuyataja.

Alisema kuondolewa kwake hakumaanishi kwamba tayari wana mgombea wao ambaye wameshamchagua kama ambavyo imekuwa ikizungumzwa.

Aidha, alisema katika nafasi ya umakamu wa rais, jina la mgombea Hussein Ahmada Vuai, limeondolewa kutokana na kuandika barua mwenyewe ya kuomba kuenguliwa na kwamba kuanzia sasa wagombea wote wapo huru kuanza kampeni huku akisisitiza ziwe za kistaarabu na si za kuchafuana.

# Michezo

Jumanne Mei 28, 2019
Nipashe




Tuchel: Sina uhakika Neymar, Mbappe kubaki UKURASA 30



Mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala, akijaribu kufunga huku kiungo wa Sampdoria, Gaston Ramirez akijiandaa kuuzuia mpira kwenye mechi ya funga msimu wa Serie A iliyopigwa juzi na Juve kulala kwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Sababu Mazembe kuachana na Ajibu

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni siku chache zimepita baada ya Klabu ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kuonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Yanga, Ibrahim Ajibu, imefahamika kwamba mchakato huo umesitishwa na sababu kuanikwa.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinameeleza kuwa TP Mazembe wamesitisha nia yao baada ya kushindwa kufikia makubaliano binafsi na mshambuliaji huyo ambaye mkataba wake na Yanga unatarajiwa kumalizika Juni 30, mwaka huu. Chanzo chetu kimeeleza kuwa TP Mazembe wamekumbana na ugumu huo baada ya kuwapo kwa taarifa kwamba Ajibu alishaingia makubaliano ya awali na Simba, hivyo kama vigogo hao wa Congo watamhitaji wanatakiwa wafanye kwanza mazungumzo na mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mazembe walikuwa tayari kumsajili Ajibu kama mchezaji huru baada ya kuwa na uhakika kuwa Yanga bado hawajamsajili, ila haya yaliyokuwa chini ya pazia, yamewafanya wabadilishe uamuzi wao," kilisema chanzo chetu.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, bado amekataa kusema lolote kuhusiana na usajili wa Ajibu na kiungo wa Gor Mahia Mkenya Francis Kahata ambaye tayari ameshawaaga wachezaji wenzake wa kikosi hicho cha mabingwa wa Ligi Kuu Kenya.

"Kahata yeye amemaliza mkataba wake na Gor Mahia ndio maana ameamua kuwaaga wachezaji wenzake, kuhusu kutua Simba mimi sijui, nasema subirini kwanza, naona wenzetu (Yanga) wameanza moto na usajili, " alisema Magori.

# Simba, Yanga heshima leo

## Vita kufa kupona kwa wakushuka daraja

## Mbao vs Kagera Sugar, Mwadui FC vs Ndanda...

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

PAZIA la Ligi Kuu Tanzania Bara linatarajiwa kufungwa leo wakati timu zote 20 zitakaposhuka kwenye viwanja 10 tofauti kusaka pointi tatu za kumaliza msimu huu wa 2018/19 ambao tayari Simba imeshatangazwa kuwa bingwa na vita sasa ikionekana kuhamia kwa timu zinazowania kuepuka kushuka daraja.

**Mabingwa Simba ambao wana pointi 92 sasa, walifanikiwa kutetea ubingwa waliokuwa wanaushikilia Mei 21, mwaka huu, baada ya kupata ushindi ugenini wa mabao 2-0 dhidi ya Singida United, huku wakiwa na mechi mbili mkononi.**

Simba wanatarajiwa kukabidhiwa kombe na medali zao za ubingwa wa Ligi Kuu leo baada ya shughuli hiyo kuahirishwa katika mechi yake dhidi ya Biashara United iliyochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema anatarajia kumaliza ligi hiyo kwa ushindi ili kuwapa furaha mashabiki wa timu hiyo ambao wamekuwa wakiisapoti tangu msimu ulipoanza.

Hata hivyo, Simba leo itamkosa mshambuliaji wake Mganda Emmanuel Okwi ambaye ameenda kwao kuungana na kikosi cha Uganda Cranes kinachojiandaa na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) zitakazopigwa mwezi ujao nchini Misri.

"Tunahitaji kushinda, tunajua sisi tayari tumeshakuwa mabingwa na Mtibwa Sugar pia wako mahali salama, tunatarajia utakuwa ni mchezo wa kuweka heshima kwa kila upande, nimewaambia wasahau ushindi tulioupata katika mechi ya kwanza," alisema Aussems.

Zuberi Katwila, Kocha wa Mtibwa Sugar ameliambia gazeti hili kuwa ameyafanyia kazi makosa waliyofanya katika mchezo wa kwanza na sasa wataingia kusaka ushindi.

"Tunafahamiana, ila tumejipanga kuwavurugia sherehe zao, hatutaki kuona tunafungwa mechi zote mbili, najua haitakuwa mechi rahisi ingawa tayari wameshachukua ubingwa," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema mechi dhidi ya Azam FC itakuwa na ushindani kwa sababu kila timu inahitaji kuona inamaliza ligi kwa ushindi na kuanza kujipanga kwa ajili ya msimu mpya.

"Sina wasiwasi na mechi ya kesho (leo), ninajua Azam na wao wanajua Yanga, tumekaa na kuyaona makosa yetu, tumeyafanyia kazi ili tuingie uwanjani kufanya kazi moja ya kutafuta pointi tatu, si mechi ndogo ingawa haibadilishi nafasi ya ubingwa," Zahera alisema.

Hata hivyo, timu nyingine ambazo leo hazina presha ya aina yoyote kwa sababu ziko nafasi salama katika msimamo wa ligi mbali na Mtibwa Sugar yenye pointi 49 sawa na Lipuli FC, ni Ndanda FC ambayo ina alama 48 na Alliance FC, Mbeya City pamoja na Coastal Union ambazo kila moja imejikusanyia pointi 47.

Mechi nyingine ya kukamilisha ratiba itakuwa ni kati ya African Lyon ambayo imeshashuka daraja dhidi ya KMC FC ambayo iko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo iliyochezwa bila ya mdhamini mkuu.

Timu ambazo leo zinahitaji kushinda ili kuwa salama kabla ya kuangalia matokeo mengine ni Mwadui FC, Ruvu Shooting, Kagera Sugar, Tanzania Prisons, Biashara United, Mbao FC na JKT Tanzania.

Michezo ya timu hizo ambazo tunaweza kuziita za "kufa ama kupona" leo itakuwa ni kati ya Mbao dhidi ya Kagera Sugar, JKT Tanzania dhidi ya Stand United, Ruvu Shooting vs Alliance FC, Mwadui FC vs Ndanda FC, Tanzania Prisons vs Lipuli FC, Coastal Union vs Singida United na Mbeya City itakaowakaribisha Biashara United kwenye Uwanja wa Ihefu.

Katika tuzo ya ufungaji bora, mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere mwenye mabao 23 ndiye anaongoza akifuatiwa na mshambuliaji mwenza, John Bocco aliyecheka na nyavu mara 17 sawa na Heritier Makambo wa Yanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >